**12 FEBRUARI, 2025**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 12 Februari, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2024 *(The Environmental Management (Amendments) Bill, 2024)*.

**MHE. MOHAMED SULEIMAN OMAR K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya

Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2024 *(The Environmental Management (Amendments) Bill, 2024)*.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Maswali Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Aleksia Asia.

Na. 196

### Uhitaji wa Vifaa Tiba na Watumishi katika Vituo vya Afya Morogoro Vijijini

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Watumishi na Vifaa Tiba katika Vituo vya Afya vya Kasanga, Kisemo na Kisaki Morogoro Vijijini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 na 2024/2025, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro imepokea jumla ya shilingi bilioni 1.65 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaatiba. Kiasi cha shilingi milioni 266 kimetumika kununua vifaatiba katika Kituo cha Afya Kasanga shilingi milioni 43, Kituo cha Afya Kisemo shilingi milioni 13 na Kituo cha Afya Kisaki shilingi

milioni 210. Aidha, shilingi bilioni 1.4 zilipelekwa katika hospitali ya wilaya na vituo vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuajiri wataalam wa kada za afya, ambapo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2023/2024, Serikali imeajiri jumla ya watumishi 25,917 wa kada za afya kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ilipangiwa jumla ya wataalam wa kada za afya 1,108 ambao wamepelekwa katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya vikiwemo Vituo vya Afya vya Kasanga, Kisemo na Kisaki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aleksia.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, ninaomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali langu la kwanza; katika hiyo Halmashauri ya Morogoro Vijijini kuna upungufu wa wodi za wanawake na watoto, hazijakamilika. Je, ni lini Serikali itachukua juhudi za makusudi kwenda kupeleka hizo fedha ili wakamilishe hiyo sehemu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, katika Kituo cha Afya cha Kisemo hakuna Daktari wa Dawa ya Usingizi, Madaktari wa Operesheni wapo lakini wa dawa ya usingizi hawapo inasikitisha sana. Pia katika Kituo cha Kasanga kuna wahudumu wawili tu wa afya, *CO* ni mmoja na *EN* mmoja. Je, ni lini Serikali itachukua juhudi za makusudi, ukifikiria kwamba....

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa nenda kwenye swali, nenda kwenye swali.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukizingatia kwamba wanawake na watoto wanakufa kwa kukosa huduma ya upasuaji kutokana na kukosekana kwa dawa ya usingizi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Aleksia Kamguna kwa kupambania na kupaza sauti kwa ajili ya Sekta hii muhimu ya Afya. Kuhusiana na maswali yake mawili, Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika Sekta ya Afya Msingi na katika kipindi cha miaka minne ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali ya Awamu ya Sita imefanya uwekezaji wa zaidi ya trilioni 1.29 katika kuimarisha hii Sekta ya Afya Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama vile Serikali ilivyoanza kutoa fedha kwa ajili ya kuhakikisha inaboresha miundombinu katika Sekta hii muhimu ya Afya Msingi. Ukizingatia kwamba, 75% ya Watanzania wote wanategemea kupata huduma ya afya kutoka kwenye hivi vituo vya kutolea huduma ya afya msingi, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea na awamu zijazo kuhakikisha kwamba inafika katika hiki kituo cha afya, kuhakikisha kwamba wodi hii ya wanawake na watoto, wodi muhimu kabisa inajengwa, inakamilishwa na inaanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo, kwenye swali lake la pili amezungumzia kuhusiana na mtaalam wa dawa ya usingizi ambayo inasababisha kwamba, kituo kushindwa kutoa huduma muhimu sana ya upasuaji. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali katika huu mwaka wa fedha imetangaza na kibali kimetoka kwa ajili ya kuajiri watumishi wa kada ya afya 9,483. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika watumishi hawa watakapoajiriwa basi watakuja kupangwa na watafika katika hivi vituo vya afya alivyovitaja ili waweze kutoa huduma bora, iliyodhamiriwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Kituo cha Afya cha Hezya na Ndolezi vina upungufu mkubwa sana wa watumishi pamoja na vifaatiba. Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba inapeleka watumishi wa kutosha na vifaatiba? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake hili lenye maslahi mapana katika kuimarisha na kuhakikisha Jimboni kwake wananchi wake wanapata huduma bora za afya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie kwamba, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha inaendelea kufanya uwekezaji mkubwa kuimarisha hii Sekta ya Afya Msingi. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge kwa muktadha huo, ninaomba ukae mkao wa kupokea kwa maana Serikali itafika kuja kuimarisha hivi vituo vya afya, pia kuhakikisha inaleta wataalam wa hii kada ya afya ili waweze kutoa huduma iliyo bora. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa *Engineer* Samweli.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Kituo cha Afya Endasak, tulikipandisha hadhi kutoka zahanati na kina upungufu mkubwa wa vifaatiba na watumishi. Je, kwa watumishi watakaoajiriwa kituo hiki kitapewa kipaumbele?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Hhayuma Xaday kwa swali lake lenye maslahi mapana ya kuhakikisha anawasemea wananchi wake kwenye hii sekta muhimu ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha inaimarisha huduma hii ya afya msingi kwa kuboresha miundombinu, kununua vifaatiba na kuleta wataalam wa kutoa huduma hizi muhimu kabisa za afya. Nimhakikishie, Serikali itaendelea kufanya hivyo na itafika katika Jimbo lake kwa ajili ya kuleta vifaa na vifaatiba pia kuleta watumishi wa hii kada muhimu ya afya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula.

Na. 197

**Kurejesha Mikopo ya Asilimia 10**

**MHE. SYLVIA F. SIGULA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itarejesha mikopo ya 10% iliyokuwa ikitolewa kwa Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu inayotolewa kutokana na 10% ya mapato ya ndani ya halmashauri, ilisitishwa na Serikali tarehe 13 Aprili, 2023 ili kupisha maandalizi ya utaratibu mpya wa utoaji wa mikopo hiyo. Kufuatia kukamilika kwa mfumo mpya wa utoaji wa mikopo, Serikali ilitangaza tarehe Mosi Julai, 2024 mikopo hiyo itaanza kutolewa tena kwa mujibu wa sheria na kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha zinatoa mikopo kwa mujibu wa sheria, ambapo tangu mikopo kurejeshwa hadi Disemba, 2024, halmashauri 64 zimetoa mikopo ya shilingi bilioni 22.07. Kati ya hizo shilingi bilioni 27.76 ziliombwa na vikundi 2,726 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kati ya

fedha hizo shilingi billioni 21.88 zimetolewa kutokana na michango ya Halmashauri (10% ya mapato ya ndani) na shilingi milioni 194.3 ni mikopo iliyotokana na fedha za marejesho.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa mikopo hii ya vikundi imekumbwa na changamoto ya wanakikundi kutokuwa na malengo ya Pamoja, lakini tuna vijana wengi ambao wana ujuzi wa biashara, wana elimu nzuri na hawana mitaji. Je, Serikali iko tayari kutoa mikopo hii kwa mtu mmoja mmoja na kuacha sharti la vikundi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; tunazo Halmashauri 184, kati ya hizo ni halmashauri 64 tu ndiyo zimerejesha hii mikopo tayari zimetoa tangu mwaka jana ambapo dirisha lilifunguliwa, bado halmashauri 120. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa hizi halmashauri 120 kuhusu mikopo hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Sylvia Sigula kwa hili swali lake lenye maslahi mapana kwa ajili ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ambao pia ni wanufaika wa hii mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza kwamba, mikopo hii iweze kutolewa kwa mtu mmoja mmoja tofauti na utaratibu wa vikundi. Ninaomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa mujibu wa maboresho ya kanuni zinazosimamia utoaji wa hii mikopo ya 10% ya mapato ya ndani. Kikundi kitaomba mkopo na kitakopeshwa kama kikundi, lakini wale wanakikundi wao wenyewe wanaruhusiwa kufanya shughuli zao wao wenyewe kama kuwekeza katika miradi binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatambua kwamba kuna vijana ambao wanataka wafanye shughuli zao au miradi yao wao wenyewe binafsi, ndiyo maana kwenye kanuni kipengele hicho kimetolewa na kwamba mikopo ile ya kikundi itakuwa kama dhamana, lakini kwenye kikundi wao wenyewe wanakikundi wanaweza kuweka utaratibu na kila mwanakikundi akawa na mradi wake yeye mwenyewe unaojitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kutoa msisitizo kwa Kamati zote zile ambazo zimeundwa za usimamizi wa mikopo hii ya 10% ya mapato ya ndani, waweze kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa kanuni. Kwa sababu, kwa mujibu wa utaratibu na kanuni inatoa mwongozo ndani ya miezi miwili tangu kikundi kimeomba mkopo, ni lazima wawe wamekamilisha taratibu zote za ndani na kile kikundi kimeweza kupatiwa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nitoe msisitizo, viongozi wetu wote waliopo katika ngazi za mikoa, ngazi ya halmashauri na mpaka katika ngazi ya kata. Kwa sababu kuna Kamati ya kutoa huduma ya mikopo hii kuanzia katika ngazi ya kata, halmashauri kuja mpaka katika ngazi ya wilaya, ngazi ya mkoa, waweze kusimamia wajibu wao ili hizi fedha nyingi ambazo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhamiria, ziweze kwenda kunufaisha makundi haya maalum, ziweze kufanya hivyo na wananchi waweze kupata mitaji kwa ajili ya shughuli zao za kiuchumi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri nikuombe, kuna malalamiko mengi sana kwa wananchi, baadhi ya Watendaji wa Kata, baadhi ya Maafisa Maendeleo hawatendi haki kwa baadhi ya vikundi, aidha kwa makusudi, kwa upendeleo au kutokujua. Hebu jaribuni kulifuatilia hili suala na mtoe tahadhari kwa yeyote atakayehusika na kuonea kikundi bila sababu, kwa maana hizi pesa ni za mama kwa watoto wake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Ng'wasi Kamani.

Na. 198

**Kuendelea Kuwezesha Mikopo kwa Makundi Maalum**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI** aliuliza:-

Je, upi mkakati wa kuendelea kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa Makundi ya Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu inatolewa kutokana na 10% ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa mujibu wa kifungu 37A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa na Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu za mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuboresha na kuhakikisha mfumo wa kutolea mikopo isiyo na riba kwa makundi haya ikiwa ni pamoja na maboresho ya sheria na kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo ya 10% ya mwaka 2024; pamoja na kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa utoaji na usimamizi wa mikopo ili kuongeza ufanisi katika utambuzi wa walengwa, usimamizi wa mikopo na urejeshaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na makundi haya ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kunufaika na mikopo ya 10% isiyo na riba, bado wanaweza kunufaika na mikopo yenye riba nafuu katika taasisi za fedha zilizopo nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamani.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwanza nianze kwa kuishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa mapitio makubwa yaliyofanywa katika mfumo wa kutoa mikopo hii ya 10% iliyolenga kuleta ufanisi, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; pamoja na marekebisho ya kikanuni ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyazungumza mbele yetu hapa, ambayo yanalenga kuonesha kwamba pamoja na maombi kufanywa kwa njia ya vikundi, lakini bado kijana au mwanamke mmoja mmoja wana uwezo wa kutumia fedha hizo binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado vijana na wanawake wameendelea kupata changamoto ya kupata watu ambao wanaendana kimalengo, wakaunda kikundi na kwenda kuomba mikopo hii. Je, Serikali haioni haja ya kurekebisha tena kanuni hizi ili kuruhusu uombaji wa mikopo hii kwa vijana na wanawake kwa mtu mmoja mmoja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; pamoja na hizi fedha za 10% zinazotolewa kama uwezeshaji wa mitaji kwa makundi maalum, tunayo Mifuko ya Uwezeshaji wa Vijana ambayo imekuwa ikikumbwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya changamoto za vijana hawa. Je, ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba inaongeza fedha katika Mifuko hii ili vijana wengi zaidi waweze kunufaika na fedha hizi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaomba nianze kumpongeza Wakili Msomi, Mheshimiwa Ng'wasi Damasi Kamani kwa maswali yake haya ambayo yana maslahi mapana kwa ajili ya vijana wa Tanzania, lakini pia wanawake na watu wenye ulemavu ambao na wenyewe ni

wanufaika wa mikopo hii ya 10% ya mapato ya ndani katika halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza, ninaomba niendelee kutoa ufafanuzi kwamba kwa maboresho ya kanuni ambazo zinasimamia utoaji wa mikopo hii, kikundi kitaomba mkopo kama dhamana, lakini ndani ya kikundi kile wanakikundi wanaruhusiwa kukaa na kukubaliana wao wenyewe kila mmoja kuwa na mradi wake, lakini kwa maana ya uombaji wa mkopo, mkopo utaombwa na kikundi kama dhamana lakini haizuii mwanakikundi kuwa na mradi wake yeye mwenyewe ndani ya hicho kikundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni hizi hizi pia zinaruhusu mtu mwenye ulemavu aweze kukopa yeye mwenyewe, tofauti na utaratibu uliokuwepo awali ambao ulilazimu hadi kundi hili la watu wenye ulemavu waunde makundi. Kwa hiyo, Serikali inatambua mahitaji ya wanufaika wa mikopo hii na kila siku inaendelea kuboresha taratibu ili kuweza kufikia ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Mbunge; Serikali inatambua na ndio maana kuna jitihada hizi, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya uwekezaji mkubwa kuhakikisha anatengeneza mazingira ya kuwawezesha vijana pia na makundi haya mengine maalum kimtaji ili waweze kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuimarisha, siyo tu kwenye upande huu wa mikopo ya 10% ya halmashauri, bali pia Mifuko mingine ambayo ipo na ambayo inawezesha haya makundi maalum kupata mitaji. Mathalani kuna Mfuko huu wa Maendeleo ya Vijana ambao mwaka huu umeweza kuwekewa mtaji wa bilioni moja; hizi ni jitihada za makusudi kabisa. Pia kuna Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambao umeweza kutoa mikopo ya zaidi ya bilioni 2.7. Vivyo hivyo kuna Mfuko Maalum wa Watu Wenye Ulemavu ambao unatoa mikopo ya kufikia bilioni 1.14.  Zote hizo ni jitihada kwa ajili ya kuhakikisha mitaji inapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna fursa nyingine ambazo zinatengenezwa kwa ajili ya makundi mengine ya…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante ameshakuelewa…

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano *mining for better tomorrow* upo kwa ajili ya kuwawezesha wachimbaji wadogo waweze kupata mitaji. *Building for better tomorrow* kwa ajili ya kuwawezesha vijana kuingia katika kilimo. Serikali itaendelea na jitihada hizi kwa sababu ni dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwawezesha vjana, wanawake, watu wenye ulemavu na Watanzania wote kuweza kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali. Kwa kuwa mikopo hii 10% inatokana na mapato ya ndani ya halmashauri na kuna baadhi ya halmashauri ambazo mapato yake ni kidogo mfano Halmashauri ya Momba. Ni upi mbadala wa mikopo ya 10% ambao utafanana kwa sura hiyo hiyo ili kuzisaidia halmashauri ambazo hazina kipato kwa sababu baadhi ya wananchi wamekosa mikopo hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, ukiacha fursa tu hii ambayo inapatikana kwenye 10% ya mapato ya ndani ya halmashauri bado kuna fursa nyingine nyingi. Nimetoka kutolea mfano hapa, kwamba kuna Mifuko mingine ya kuwawezesha wananchi kimitaji. Kwa mfano, mitaji ya huu Mfuko wa Maendeleo ya Vijana wenye mtaji wa bilioni moja, nimetaja pia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambao mpaka sasa

umeweza kutoa zaidi ya bilioni 2.7 kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna makundi mengine pia ambayo nimeyataja. Kwa mfano, kuna Mfuko Maalum wa Watu Wenye Ulemavu ambao ni bilioni 1.14 kwa ajili ya kuwawezesha wananchi ambayo yote hii inaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kutoa fursa mbalimbali zitakazowawezesha kupata mitaji na kufanya shughuli za uzalishaji mali.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Mwanaisha Ng'anzi.

Na. 199

**Mtandao Mpya wa Barabara Mkoa wa Tanga**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itasajili na kutangaza rasmi barabara mpya ili kuongeza Mtandao wa Barabara za Mkoa wa Tanga zilizo chini ya *TARURA*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tanga umekamilisha taratibu za ndani za kujadili na kupitisha maombi ya kupandishwa hadhi/kusajiliwa barabara ambazo hazikuwa katika mtandao wa barabara za *TARURA*. Maombi hayo tayari yamewasilishwa Wizara ya Ujenzi kwa ajili ya taratibu zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanaisha.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa mujibu wa Sheria ya Barabara ya Mwaka 2007 sehemu ya tatu, kifungu cha 11(1) ambacho kinampa mamlaka Waziri wa Ujenzi kuweza kuzipandisha hadhi au kuzishusha hadhi; na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema ameshapeleka Wizara ya Ujenzi, ninaomba sasa tumsikilize kwa ridhaa ya kiti chako, Waziri wa Ujenzi kama wameweza kupokea hayo ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge kwa maoni yake. Sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutaendelea kufanya mawasiliano kwa karibu kabisa na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi ambao kwa mujibu wa Sheria ya Barabara *(The Road Act)* ya mwaka 2007, Wizara ya Ujenzi wamepewa mamlaka ya upandishaji wa hizi barabara. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kufanya uratibu na mawasiliano ndani ya Serikali ili kuweza kufuatilia kwa ukaribu upandishaji wa barabara hizi ambazo maombi yake wao kama Mkoa wa Tanga wameshawasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Barabara za Barikiwa - Mkutano, Nabuu ya Tepetepe, Mlembwe- Barikiwa, Mkutano - Kimambi na Makinda - Ngorongopa zote hizi tumeshaziombea ili ziweze kusajiliwa kuongeza mtandao wa barabara kwenye Halmashauri yetu ya Liwale. Je, ni lini Serikali itatusajilia hizo barabara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Kuchauka kwa swali lenye maslahi

mapana ya kuhakikisha wananchi wake wanapata barabara ambazo zinahudumiwa na *TARURA*. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Serikali kwa pamoja tutafanya mawasiliano ya ndani ili kuweza kupata muafaka wa maombi yao haya ya kuzitambua barabara hizi alizozitaja na kuziingiza katika mtandao unaohudumiwa na *TANROADS*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Mwambe.

Na. 200

**Ujenzi wa madaraja Wilaya ya Masasi**

**MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kujenga Madaraja ya Chikundi katika Wilaya ya Masasi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kujenga madaraja mbalimbali yaliyo katika Kata ya Chikundi, Wilayani Masasi, ambapo katika mwaka wa fedha 2023/2024, Daraja la Nasindi lilitengewa shilingi milioni 13.7 kwa ajili ya kukarabati nguzo ya daraja. Kazi hiyo bado inaendelea kutekelezwa na mkandarasi yuko eneo la kazi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imetenga milioni 16.833 kwa ajili ya kuweka kifusi cha changarawe kilomita moja katika Barabara ya Mbaju – Litamwa kwenye maingilio ya daraja ambapo tayari kazi hii imeshaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali imeweka katika mipango yake ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026, shilingi milioni 20 kwa ajili ya kuweka kifusi kilomita moja kwenye maingilio ya Daraja la Lukuledi katika Barabara ya Mtunungu – Lukuledi.

Serikali inaendelea kuihudumia miundombinu ya Barabara ya Wilaya ya Masasi ikiwemo ujenzi wa madaraja kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ni kweli kazi hizo zinaendelea. Niliweke sawasawa, ni Kata ya Chikundi, siyo kama vile ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri ameitamka. Tunalo pia Daraja la Liputu – Ng'uni, tunalo pia Daraja la Nango'o – Ng'uni. Pia tushukuru kwa sababu ya Daraja la Litama Mbaju. Nataka kufahamu ni lini Daraja la Liputu ambalo wakazi wa Ndanda wamekuwa wanalitumia kuvuka kwa ajili ya kwenda kwenye masuala ya kilimo, upande wa pili wa upande wa Ruangwa kupitia Kivuko cha Nguni na Kivuko cha Nangoo. Je, ni lini madaraja haya yatajengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Cecil Mwambe kwa maswali yake yanayolenga kuwasemea wananchi wake kupata miundombinu bora kabisa ya barabara hizi za wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TARURA* kwenye mpango wa kukabiliana na dharura imetenga bilioni 2.5 kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Ng'uni. Tayari usanifu umeshafanyika na taratibu za manunuzi zinaendelea na zinatarajia kwisha; mwezi wa tatu zitakuwa zimekamilika kwa ajili ya ujenzi kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ujenzi au uboreshaji wa Daraja la Ng'uni, daraja hili litakuwa ni lile daraja la chuma ambalo kwa jina la kitaalam wanasema ni *mabey bridge*. Litakuwa lina urefu wa mita 30 na litakuwa na madaraja mawili saidizi. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa

miundombinu hii ya barabara na madaraja haya kwa sababu wananchi wanajishughulisha na shughuli za kilimo pia wanatumia barabara hizi kufikia huduma muhimu kabisa za kijamii. Nimhakikishie kwamba Serikali itaendelea kuhudumia barabara hizi za wilaya katika jimbo lake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kijiji cha Buriashi na Mwamagingo hakuna daraja kabisa na daraja lile ni muhimu kwa sababu kuna wanafunzi wanaotoka Mwamagingo kwenda Buriashi Sekondari hakuna Daraja. Je, ni lini Serikali itajenga daraja ili kurahisisha mawasiliano kwa wakazi wa Wilaya ya Meatu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Minza kwa swali lake lenye lengo la kuhakikisha wananchi wa Meatu wanapata miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa barabara hizi za wilaya kwa sababu ya barabara hizi ndio zinazosaidia wananchi katika shughuli zao za uzalishaji mali na ndizo hizi zinazowawezesha wananchi kufikia huduma muhimu kabisa za kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie kwamba Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hizi na ndiyo maana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika uongozi wake wa miaka minne amepandisha bajeti ya kuhudumia barabara hizi kutoka bajeti ya bilioni 275 kwa mwaka hadi sasa kila mwaka bajeti ni milioni 710. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kufika maeneo mbalimbali nchini ili kuunganisha mawasiliano katika maeneo yale ambayo

mawasiliano yamekatika ikiwemo maeneo haya yenye vivuko na madaraja. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itafika Meatu na itakuja kujenga daraja hilo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Barabara ya Kapanga – Bujombe ipo hatarini kutokupitika baada ya mkandarasi kushindwa kujenga madaraja. Je, ni lini Serikali itamsimamia mkandarasi huyu ili aweze kukamilisha ujenzi wa madaraja haya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri anataka kujua ni lini tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Selemani Kakoso kwa swali lake zuri lenye maslahi mapana kwa ajili ya wananchi wake, wapiga kura wake.

Ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwagiza Meneja wa *TARURA* wa mkoa kufika na kufuatilia changamoto inayokabili ujenzi wa daraja hili ili tuweze kusimamia kwa ufanisi na daraja hili liweze kukamilika kwa mujibu wa mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Nchi amekuwa akitoa maagizo mara kwa mara na akisisitiza, kwamba wakandarasi wanapopatiwa kazi hizi za ujenzi wa barabara wazingatie mkataba na wafanye kazi kwa ufanisi kwa viwango na wakati. Kwa hiyo, Meneja wa *TARURA* wa mkoa aweze kusimamia maelekezo haya ambayo yametolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Anton Mwantona.

Na. 201

**Kuweka Mifumo ya Gesi kwenye Taasisi Kuokoa Mazingira**

**MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Taasisi zinazohudumia watu wengi zinaweka mifumo ya majiko ya gesi ili kuokoa mazingira?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha taasisi zinazohudumia watu wengi zinaweka mifumo ya majiko ya gesi ili kuokoa mazingira, Serikali imetekeleza jitihada mbalimbali za kuhamasisha matumizi ya nishati safi nchini. Baadhi ya jitihada hizo ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa Katazo la matumizi ya kuni na mkaa kwa taasisi za umma na binafsi zinazoandaa chakula na kulisha watu zaidi ya mia moja; ambapo jumla ya Taasisi 551 zimeanza matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa nishati safi ya kupikia; na kusaini makubaliano ya awali na wawekezaji mbalimbali wa makampuni ikiwemo Kampuni ya *Oryx, Taifa Gas, Lake Gas na Manji's gas* kuhusu kutoa ruzuku ya shilingi Bilioni 8.64 kwenye nishati safi ya kupikia ili kupunguza mzigo wa gharama kwa watumiaji wa nishati safi ambapo jumla ya majiko 452,455 yamepata ruzuku. Aidha, Serikali inaendelea na ukamilishaji wa taratibu za kuanzisha Mfuko wa Nishati Safi ya Kupikia ili kuweka ruzuku itakayowawezesha wananchi wa kipato cha chini kumudu bei ya gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha uandaaji wa Kanuni ya Katazo la Matumizi ya Kuni na Mkaa kwa Taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa siku. Kanuni

hizo zitajumuisha taasisi za umma na taasisi za watu binafsi. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwantona.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niipongeze Serikali kwa kuweka ruzuku kwenye majiko ya gesi. Wamesema wameweka bilioni 8.64 na majiko zaidi ya laki nne na hamsini na mbili yamekwishagawiwa, hiyo ni hatua mojawapo nzuri zaidi. Pia kwenye jimbo langu nimeshapata majiko zaidi ya 1,600, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; hizi taasisi zinatumia kuni nyingi sana, maelfu ya tani kwa mwaka. Sasa, ninaona, kwa sababu wamekwishaweka ruzuku kwa watumiaji wadogo wadogowadogo. Je, Serikali ina mpango gani kuweka ruzuku kwenye taasisi hizi kubwa hasa kwenye ujenzi wa miundombinu ili majibu haya yasaidie ku-*save* mazingira katika maeneo mbalimbali ya nchi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Rungwe kuna mgodi wa makaa ya mawe wa Kiwira, wameanzisha mradi pale wa kutengeneza mkaa kwa matumizi ya nyumbani. Je, Serikali itakuwa tayari kwenda kutembelea huu mradi kwa lengo la kusaidia uzalishaji uwe mkubwa zaidi na bei ya makaa iweze kupungua kwa sababu sasa hivi wanauza kilo moja kwa shilingi 1,000 kiasi kwamba wananchi wengi hawawezi ku-*afford* hiyo bei?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali tayari imeshatoa maelekezo ya taasisi zote zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa siku zitumie nishati safi ya kupikia na kwa kuwa Serikali hiyo hiyo, tayari

imeshatoa maelekezo ya wananchi Tanzania nzima tufanye jitihada katika kupanda ili tunusuru mazingira yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kwa kuwa Serikali imeshaanza hatua za kufanya punguzo, angalau wananchi waweze ku-*afford* matumizi ya nishati safi ya kupikia, nimwambie tu kwamba Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira na Wizara ya Nishati tuko katika hatua ya mwisho kuhakikisha kwamba tunakamilisha utaratibu wa kukamilisha uwepo wa Mfuko wa Nishati ambao unaitwa *CookFund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko huu utawezesha mtu mmoja mmoja, taasisi, kampuni hata vikundi vya watu. Lengo na madhumuni kuweza ku-*afford* matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari Serikali imekwishaandaa mkakati wa miaka 10 kuanzia 2024 mpaka 2034 kwa ajili kuhakikisha kwamba kwanza wananchi wanaweza kuhimili matumizi ya nishati safi ya kupikia na kusaidia kuendelea kutoa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa siyo mkaa wa mawe tu, lakini hata makaa mengine hapa, ambao ni mkaa mbadala ikiwemo mikaa ya kutumia miti, majani, makaratasi na hata vinyesi vya wanyama, nimwambie tuko tayari na tutapanga muda wa kwenda kutembelea katika mgodi huo ili kuendelea kuwaelimisha wananchi na pia kuendelea kujaribu kukaa na taasisi mbalimbali kuona namna ambavyo tunaweza tukashauri kama Serikali kuweza kupunguza hizo gharama za upatikanaji wa huu mkaa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tuendelee na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Tendega.

Na. 202

**Magari ya Serikali kuwa na Mfumo wa Nishati ya Gesi**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Magari ya Serikali yanakuwa na mfumo wa nishati ya gesi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha Serikali kuanza kutumia magari yanayotumia gesi Serikali katika imejikita kuweka miundombinu ya kuwezesha matumizi ya *CNG* kwenye magari ya Serikali kwa urahisi. Serikali kupitia *GPSA (The Government Procurement Services Agency*) imekwishaanza taratibu za kuweka miundombinu kwa ajili ya magari ya Serikali yatakayotumia gesi ikiwemo kufanya tathmini za athari za kijamii na mazingira pamoja na uandaaji wa michoro ya kina ya kihandisi na usimamizi wa ujenzi. Taratibu hizi ni kuweka miundombinu rafiki kwa magari ya Serikali kuanza kutumia gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ili kuboresha upatikanaji wa *CNG* kwa mikoa iliyo katika barabara kuu kuelekea Dodoma, Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TPDC)* ipo kwenye hatua za manunuzi za mradi wa kuagiza na kusimika vituo vya *CNG* vinavyohamishika; ambapo kwa kuanzia vituo vitatu vitasimikwa Dar es Salaam, kimoja kitasimikwa Morogoro na viwili vitasimikwa Dodoma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ninashukuru kwa majibu ya Serikali lakini kuna changamoto nyingi sana zilizopo. Ili kuvutia Watanzania walio

wengi kuweka mfumo wa gesi kwenye magari ni lazima Serikali iwe imejipanga. Je, Serikali haioni haja ya kushirikiana na Sekta Binafsi kuhakikisha kwamba magari yanayotumia gesi yanaweza kuingizwa moja kwa moja hapa Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kufunga mfumo wa gesi kwenye magari ni gharama kubwa sana, ni takriban shilingi milioni mbili hadi tatu ambazo Watanzania wengi wanashindwa ku-*afford*. Je, Serikali haioni haja ya kupunguza kodi kwenye vipuri ambavyo vinatumika kufungia magari hayo kwa sababu hatuna kiwanda cha vipuri hapa Tanzania? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhamasisha matumizi ya magari yanayotumia nishati ya gesi asilia na katika kuhakikisha tunaweka mazingira rafiki kwa Sekta Binafsi kushiriki, Bunge litakumbuka, mwaka 2023/2024 Serikali ilifuta kodi ya ushuru wa bidhaa kwa magari yote yanayoingizwa nchini yakiwa na mfumo unaotumia gesi asilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili tayari taasisi mbalimbali za Serikali na sekta binafsi zimeanza kunufaika. Mwanzoni mwa mwezi Januari, taasisi yetu ya magari yaendayo kasi pale Dar es Salaam imeidhinishiwa magari 755 yaweze kuagizwa kuingia nchini yakiwa na mfumo wa gesi asilia na tayari zabuni hiyo imekwishatangazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuona uwezekano wa kupunguza bei kwenye vipuri, ninapenda kulifahamisha Bunge kwamba kwa sasa Serikali, kwa maana ya Wizara ya Fedha na taasisi yake ya *TRA* na *TPDC* na Wizara ya Nishati wapo katika mapitio ya maeneo ambayo yanaweza kupata msamaha kwa ajili ya vipuri hivi ili viweze kupatikana kwa urahisi. Vilevile, *TPDC* ipo katika mkakati wa kutafuta wawekezaji watakaoweza kuwekeza viwanda hivi hapa nchini ili vipuri hivi viweze kuzalishwa kwa bei rahisi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Nollo.

Na. 203

**Kasi ya Usambazaji wa Umeme**

**MHE. KENNETH E. NOLLO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani kuhuisha zaidi kasi ya usambazaji wa umeme nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuongeza kasi ya usambazaji umeme nchini kupitia miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya kupeleka umeme vijijini ambapo imeweza kufikisha umeme katika vijiji vyote 12,318 Tanzania Bara na vitongoji 33,657 kati ya vitongoji 64,359, sawa na 52.3%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kasi hiyo ya usambazaji wa umeme nchini idadi ya wateja imeongezeka kutoka wateja 4,689,024 waliokuwepo mwezi Januari, 2024 hadi kufikia wateja 5,276,679 mwezi Desemba, 2024, sawa na ongezeko la 12.5%. Aidha, kupitia Mpango Mahususi wa Taifa wa Nishati, Serikali imelenga kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme nchini kutoka 78.4% hadi 100% ifikapo mwaka 2030.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nollo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri. Vilevile, ninaishukuru Serikali kwa jitihada za kufikisha umeme katika maeneo ya wananchi. Swali langu la kwanza; pamoja na kwamba katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 nimepata vitongoji 15, lakini Bahi ina

vitongoji 520. Je, nini ahadi ya Serikali katika kuongeza kasi ya kuweka umeme zaidi katika vitongoji vingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Kitongoji cha Mgondo kilichopo katika Kijiji cha Kongogo katika Kata ya Babayu ni kitongoji chenye sura ya kijiji. Vilevile, Kitongoji cha Majengo kilichopo Kata ya Mpalanga Kijiji cha Chidilo nacho kina sura ya kuwa kijiji. Vitongoji hivi vikubwa bado havijapata umeme. Ni nini mkakati wa Serikali katika kufanikisha vitongoji hivi viwili vya Mgondo na Majengo viweze kupata umeme? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kupeleka umeme katika jimbo la Mheshimiwa Mbunge. Katika mwaka huu wa fedha, Serikali imejipanga kuhakikisha inakuja na mpango mwingine wa kupeleka umeme kwenye vitongoji. Mpango huu utatangazwa hivi karibuni na tunatarajia katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge vitongoji visivyopungua 70 vitapatiwa umeme. Katika maeneo yale ambayo ameyataja basi yatazingatiwa katika huu mradi mpya ambao unakusudiwa kutangazwa hivi karibuni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ishengoma. Eeh wewe au wewe siyo dokta? Basi kaa chini kama wewe siyo dokta. *(Kicheko)*

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali. Je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye Kijiji cha Madudumizi B ambacho hakina umeme kwenye Kata ya Zombo, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, tayari tumekamilisha kupeleka umeme kwenye vijiji, kazi iliyopo sasa ni kupeleka kwenye vitongoji. Kwa sasa, kila jimbo linapelekewa vitongoji 15, lakini hivi karibuni tutatangaza mpango mwingine ambao unatarajiwa kupeleka umeme kwenye vitongoji vingine zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Chikota.

Na. 204

**Ujenzi Awamu ya Pili Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Je, lini awamu ya pili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa awamu ya pili wa Hospitali ya Kanda ya Kusini, Mtwara unaojumuisha ujenzi wa jengo la mama na mtoto, ujenzi wa nyumba za watumishi, ujenzi wa kichomea taka, ujenzi wa jengo la kufulia na tayari usanifu wa michoro umeshakamilika na taratibu za kumpata mkandarasi zimekwishaanza na zabuni imeshatangazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kulithibitishia Bunge lako kuwa mpaka kufikia mwezi Aprili 2025, awamu ya pili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini utakuwa umeanza. Ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa zabuni ya awali imetangaza majengo mawili; jengo la kichomea taka na majengo ya watumishi nyumba nne; je, ni lini Serikali itatangaza zabuni ya jengo la mama na mtoto ambalo ni muhimu sana katika hospitali hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; hospitali hii ina upungufu mkubwa wa watumishi. Mahitaji ya watumishi ni zaidi ya 600, lakini waliopo sasa ni 277 tu. Serikali ina mpango gani wa kuleta watumishi katika Hospitali hii ya Kanda ya Kusini? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge, kaka yangu Chikota, kwa sababu amekuwa siyo mtu wa kupigania masuala ya jimbo lake tu, lakini amekuwa mtu anayepigania masuala ya Kanda ya Kusini na ndiyo maana hapa anaizungumzia Hospitali yao ya Kanda ya Kusini, Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza kwamba ni lini tenda nyingine ya mama na mtoto itatangazwa? Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutatangaza ndani ya wiki mbili na ninaomba tukitoka hapa mchana tukutane pale Wizarani, ataona *process* ambazo zinaendelea kwa ajili ya kutangaza hicho alichokisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili amesema suala la watumishi kwamba wako 270, lakini wanatakiwa zaidi ya 600. Ni kweli kwamba kwa ikama na ilivyo kwenye miongozo kwa kila hospitali ya kanda inatakiwa iwe na watumishi wangapi, kwa kweli hospitali ya Mtwara inaonesha kuwa na watumishi wachache. Hata hivyo, nimkumbushe kwamba hospitali hiyo ni mpya kama yeye mwenyewe anavyojua, wao ndiyo wameipigania mpaka ikaanza. Kwa sasa inatibu wagonjwa 102 kwa siku, wa ndani wanakuwa 40 na wengine kama 60 ndiyo

wanatoka nje. Unaweza ukaona hata idadi ya watumishi ni wengi kuliko idadi ya wagonjwa wanaokuja kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tutaendelea kuongeza idadi ya watumishi jinsi ambavyo mahitaji yatakavyoendelea kujionyesha. Mpaka sasa ninataka kumhakikishia kweli kuna vitengo ambavyo vinahitaji kuwekewa watumishi, lakini idadi ya wagonjwa bado ni ndogo sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Ni nini mkakati wa Serikali wa kuongeza jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Dodoma kwani lililopo halitoshelezi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo amekuwa akipigania masuala ya Mkoa wa Dodoma. Ninamhakikishia kwamba kama mnavyojua tumekubaliana kuna ujenzi ambao unaanza karibuni kwa ajili ya hospitali zote za mikoa kujenga wodi za mama na watoto na wodi za watoto njiti ambao ni wale akinamama wanaojifungua watoto kabla ya muda wake na Dodoma siyo muda mrefu nayo itafikiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuena.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza ninaishukuru Serikali ya Mama Samia kwa kazi nzuri iliyofanya ya kupeleka vitanda katika Vituo vya Afya vya Miamba pamoja na Ntii. Vitanda hivyo vimepelekwa lakini hakuna wodi za kulaza wagonjwa. Je, ni lini Serikali itajenga wodi hizo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake makini. Nimemwona, siyo kwamba anazungumzia ambacho hajatembelea eneo husika, nimemwona akitembea kwenye kila kituo, kila wilaya kwenye Mkoa wa Kilimanjaro na hospitali yetu ya mkoa na *KCMC* akiangalia matatizo mbalimbali yanayosibu wanawake na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwambia Mheshimiwa Mbunge, kuna mkakati maalum ambao wenzetu wa TAMISEMI na sisi tunaendelea kuufanyia kazi ili kuhakikisha hayo matatizo yanakwenda kwisha moja kwa moja na kutakuwa na mambo makubwa sana yatatokea kwenye bajeti ya mwaka huu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na kabla sijauliza swali langu, nilitaka likae sawa. Nilimaanisha kutoa huduma na dawa kwa wagonjwa wa kifafa bure. Baada ya masahihisho hayo, ninaomba swali langu namba 205 lipate majibu ya Serikali.

Na. 205

**Huduma ya Dawa za Kifafa**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja kwa sasa kutoa huduma na dawa kwa wagonjwa wa kifafa bure?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitoa matibabu kwa wagonjwa wa kifafa katika ngazi zote za huduma nchini. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 takribani wagonjwa 199,324 walipatiwa huduma za matibabu katika vituo

vya kutolea huduma za afya hapa nchini. Kwa mujibu wa mwongozo wa matibabu yaani *Standard Treatment Guidelines (STG)* kuna takribani aina nane za dawa za msingi za matibabu ya kifafa ambazo hutolewa kuanzia ngazi ya msingi ambapo dawa hutolewa kulingana na hali ya ugonjwa. Huduma za matibabu ya kifafa hutolewa kwa mujibu wa Sera ya Afya ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kulithibitishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itaendelea kutoa huduma za dawa kwa wagonjwa wa kifafa na kuhakikisha huduma hizo zinapatikana katika ngazi zote za vituo vya kutolea huduma. Ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia majibu ya Serikali, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; mwaka 2023 Shirika la Afya Duniani lilitoa tathmini yake kwamba wagonjwa milioni 50 walibainika kuwa na kifafa, lakini kila mwaka walibainika wagonjwa milioni tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi zenye kipato cha kati na cha chini tukiwemo Tanzania, kati ya watu 100,000, watu 139 wamebainika wana kifafa. Ni ipi programu maalum ya Taifa ya kuweza kutoa elimu kulingana na ukubwa wa tatizo hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; amezungumzia matibabu wanayoyatoa. Changamoto zinazopelekea idadi kubwa ya wagonjwa wa kifafa ni pamoja na ajali, watoto wanapozaliwa, wanawake wanapojifungua na sababu nyingine nyingi. Wizara haioni kwamba ni muda muafaka wa kuanza kutoa matibabu haya mapema kwa sababu kifafa kinatibika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza dada yangu, Mheshimiwa Khenani, ameuliza swali la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ni mojawapo ya magonjwa ambayo wakati mwingi watu wengi wamekuwa hawajui kwamba yapo. Watu wengi wapo mtaani na hawapelekwi hospitalini kwa hiyo, ni sehemu moja kubwa muhimu ya hamasa kuhusu ugonjwa huo na watu waweze kutuletea watu hospitalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ya Jumatatu sikuwepo hapa Bungeni, ilikuwa ni siku maalum kwa ajili ya wagonjwa wa kifafa. Kwa hiyo, ninamwambia Mheshimiwa katika maswali yake haya mawili; moja, kwamba wako wengi tunawatambuaje mapema?

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, tumeanza kampeni kwa kutumia madaktari wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, moja ya ajenda yetu ya kudumu kwa madaktari wale ni pamoja na kutambua wagonjwa wa kifafa na kuwaleta pale na kuanza kuwatibu *on site* ili na wataalam walioko pale wajifunze hizo *knowledge* walizonazo *specialists* wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, pia ameshatoa maelekezo kwamba kuanzia sasa haya magonjwa mengi, siyo kifafa tu, mtoto aanze kufuatiliwa toka mimba inavyotunga, anapozaliwa a-*screen*-iwe magonjwa yote mpaka upofu na mambo mengine kuhakikisha kila ugonjwa unajulikana mapema, yale yenye tiba tuweze kutibu mapema. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Shabani Ng'enda kwa niaba yake, Mheshimiwa Joseph.

Na. 206

**Kuanzisha Ufugaji wa Samaki kwa Kutumia Vizimba Ziwa Tanganyika**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI K.n.y. MHE. KILUMBE S. NG'ENDA** aliuliza:-

Je, lini wananchi wanaozunguka Ziwa Tanganyika watapata elimu na nyenzo za kuanzisha ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo wameendelea kujenga uwezo wa kufuga samaki kwa njia ya vizimba kwa wananchi wanaozunguka Ziwa Tanganyika ambapo, jumla ya wananchi 302 wamepatiwa mafunzo kuhusu mbinu bora za ufugaji samaki kwa njia ya vizimba. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB)* inaendelea na zoezi la ugawaji wa nyenzo za ufugaji wa samaki ambapo jumla ya vizimba 29, vifaranga na chakula vyenye thamani ya shilingi milioni 602 vimetolewa kwa mikopo ya masharti nafuu isiyokuwa na riba kwa wanufaika katika Mikoa ya Kigoma, Rukwa na Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa, jumla ya vizimba 16 vimesanikishwa katika eneo la Katabe, Mkoani Kigoma na zoezi la upandikizaji wa vifaranga linaendelea. Aidha, Wizara itaendelea na zoezi la ugawaji wa pembejeo kwa wanufaika wengine kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali. Kwa kuwa, elimu hii ni muhimu sana si kwa Ziwa Tanganyika tu, lakini kwa maeneo yote ya ziwa hasa Ziwa Victoria ambako sehemu kubwa ya wananchi wanategemea uvuvi. Je, ni nini mkakati wa Serikali kutoa elimu hii kwenye eneo lote la Ziwa Victoria hasa maeneo ya Ukerewe ambako shughuli kubwa ya kiuchumi ni uvuvi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi, tumeanza kutoa elimu kwenye Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, lakini pia Ziwa Nyasa na kwenyewe tayari tumeshatuma wataalam kwenda kuainisha maeneo ambayo tunaweza kuweka vizimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwondoa wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba, maeneo yote yanayozunguka Ziwa Victoria, tayari tuna wataalam wetu kupitia Maafisa Ugani, Maafisa Uvuvi waliokuwa kwenye maeneo hayo, wanaendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuanzisha vizimba katika maeneo yao yanayowazunguka. Kwa hiyo, hilo tayari tumeanza katika maeneo mbalimbali ya maziwa yote makubwa yaliyoko ndani ya nchi yetu, lakini pia katika mabwawa ambayo yanazunguka maeneo ya vijiji vyetu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Chege.

Na. 207

**Kuwa na Zao la Kimkakati - Mara**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itahimiza kuwa na zao la kimkakati Mkoa wa Mara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na ikolojia ya Mkoa wa Mara, mazao ya kimkakati yanayohimizwa ni pamoja na pamba, kahawa, tumbaku, alizeti, muhogo na mazao ya jamii ya mikunde ikiwemo dengu na choroko. Wakulima wanashauriwa kufuata kanuni bora za kilimo ili kuhakikisha wanazalisha mazao hayo kwa tija kwa lengo la kuongeza usalama wa chakula na kipato kwenye kaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kufanya jitihada mbalimbali kuhakikisha mazao hayo yanapewa kipaumbele na kuzalishwa kwa tija kwa kuimarisha huduma za ugani, kuhamasisha wawekezaji katika miundombinu ya umwagiliaji, uhifadhi, uchakataji na kuimarisha masoko ya mazao hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, mazao makuu matatu yanayolimwa Mkoa wa Mara kwa ajili ya chakula na sehemu ndogo kibiashara, ni pamoja na mahindi, mtama na muhogo; na kwa kuwa, mpaka sasa Mkoa wa Mara haujawa na mazao ya kimkakati na kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka kuchukua mazao haya matatu, kuyaingiza kwenye Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ili kuendelea kuongeza thamani, kuimarisha soko na tija kwa mazao haya kwa wakulima wa Mkoa wa Mara?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; ni kuhusiana na vipimo vya afya ya udongo vinavyoendeshwa nchi nzima ikiwemo Mkoa wa Mara na Wilaya ya Rorya. Nataka kujua, je, ni lini Serikali itakamilisha mfumo huu ili kutengeneza *road map* na kutengeneza mfumo mzuri kwa wakulima? Kujua aina ya mazao wanayopaswa kulima kwenye maeneo yao ili kuendelea kuongeza tija kwa mazao ya kibiashara kwenye maeneo wanayolima hasa Mkoa wa Mara na Wilaya ya Rorya kwa ujumla wake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri ambayo pia ni kuonesha namna ambavyo anawasimamia wananchi wake. Kwenye suala la kwanza kuhusu

stakabadhi ghalani kwa mazao ambayo ameyatamka, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge. Kinachofanyika hivi sasa tunaangalia uwepo wa miundombinu muhimu ikiwepo maghala na upatikanaji wa masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge hili, natoa maelekezo kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mazao Mchanganyiko na Mazao ya Bustani *(COPRA)* iweze kufanya tathmini endapo muhogo na mtama yanaweza kuingizwa katika masuala ya stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili la kuhusiana na ikolojia, ni kweli Serikali imejipanga kuhakikisha inapima afya ya udongo nchi nzima na mpaka hivi sasa tumeshafikia mikoa karibu yote nchi nzima, imebaki mikoa nane ukiwemo Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hatua ya kwanza iliyofanyika ni ugawaji wa vifaa vya upimaji wa afya ya udongo ikiwemo Halmashauri ya Rorya na yenyewe wamepata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri hivi sasa Wilaya ya Rorya wanafahamu mazao ya kuanzia kwa sababu ardhi ya Wilaya ya Rorya ni ya kitifutifu, yenye mchanga na mfinyanzi mweusi ambayo ina uwezo ku-*support* mazao kama pamba, muhogo na mtama. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ifikapo mwaka 2026, tutakamilisha ramani ya nchi nzima ya afya ya udongo ili tuwaongoze vizuri wananchi kujua mazao gani ya kulima katika eneo husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maboto.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Je, Serikali sasa haioni ni muda muafaka wa kurasimisha zao la mahindi kuwa zao la kibiashara katika Mkoa wa Mara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika kitabu cha bajeti cha zao la kilimo, tumeainisha mazao kulingana na mahitaji yake na vilevile umuhimu wake. Kutokana na mahitaji makubwa hivi sasa ya zao la mahindi kama alivyosema, Serikali iko mbioni kuona namna ambavyo pia tutalifanya zao hili kuwa kama sehemu ya zao kubwa la kibiashara kwa sababu ya mahitaji yake makubwa nje ya Tanzania na mahitaji makubwa yaliyopo katika Bara letu la Afrika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Mafuwe.

Na. 208

**Ujenzi wa *Common Use Facility* - Hai**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa *Common Use Facility* utaanza kwa kuwa ilishawekwa kwenye bajeti?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ilitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo Jumuishi cha Kuhifadhi Mazao ya Bustani *(Common Use Facility)* kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Hai. Hata hivyo, baada ya kufanyika tathimini, ilibainika kuwa hitaji kubwa la halmashauri hiyo ni soko kwa ajili ya kuuzia mazao yao. Hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Hai walibadili na kuanza ujenzi wa soko unaoendelea katika eneo la Mula katika halmashauri hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Wizara inaendelea na ujenzi wa vituo viwili vya kuhifadhi mazao ya bustani katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi Mkoani Iringa na Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Mkoani Mbeya ambazo zilitoa maeneo

yenye umiliki wa hati pacha. Aidha, Wizara itaendelea na ujenzi wa vituo hivyo, kwenye maeneo mengine yenye uhitaji na yatakayokidhi vigezo vya kuwa na vituo vya kuhifadhi mazao ya bustani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; Soko hili la Mula lilitangazwa na mkandarasi akapatikana, lakini hivi karibuni tumeambiwa kuna makosa ya kitaalam yalifanyika ambayo yanazuia soko hili lisianze kutangazwa, nami waliniambia siku ya Jumamosi tunaenda kukabidhi mkandarasi aanze ujenzi. Je, ni lini sasa mkandarasi huyo ataanza kujenga Soko letu la Mula?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Chama cha Mroso Sangi kwa maana ya Shamba lile la Kibo na Kikafu, tuliingia mkataba na Kampuni ya MackJaro kwamba ajenge kiwanda cha parachichi, mpaka sasa hivi hajaanza ujenzi wa kiwanda hiki wakati kwenye *workplan* tulikubaliana mwaka 2024 aanze ujenzi. Je, ni lini sasa kiwanda hiki cha parachichi kitaanza kujengwa kwenye Shamba la Kibo Kikafu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MADINI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza, ni kweli ilitokea changamoto katika Mfumo wa *Nest,* ilivyopandishwa ile zabuni, ilionekana kuna *details* nyingi sana zinakosekana. Hivyo natumia fursa hii, kumuarifu Katibu Mkuu na kumtaka Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo chini ya Idara ya Masoko, kuhakikisha kwamba wanapitia na ku-*address* changamoto zilizojitokeza ili zabuni hii itangazwe kwa haraka, wananchi wa Hai waanze kunufaika na Soko hilo la Mula kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusu ujenzi wa kiwanda cha parachichi katika eneo lile la Mroso Sangi ambapo yaliingiwa makubaliano na *workplan* iko pale, ni kweli ilipaswa itekelezwe na haijatekelezwa mpaka hivi sasa. Hivyo natumia fursa hii

kumwelekeza Mrajisi wa Tume ya Ushirika kuhakikisha anasimamia utekelezaji wa *workplan* hii ili ujenzi wa kiwanda hiki uanze mara moja, wananchi wa Hai wanufaike na mradi huu mkubwa wa parachichi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Pondeza, kwa niaba yake, Mheshimiwa Mtaturu.

Na. 209

**Hitaji la Huduma za Kubadilisha Fedha Karibu na Hoteli za Kitalii – Zanzibar**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU K.n.y. MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Je, Serikali imechukua hatua gani za kuhakikisha huduma za kubadilisha fedha zinapatikana karibu na Hoteli za kitalii Zanzibar?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali kuwezesha upatikanaji wa huduma za kubadilisha fedha za kigeni kwa urahisi nchini ikiwemo Zanzibar, ni kurekebisha Kanuni za Maduka ya Kubadilisha Fedha za Kigeni za Mwaka 2019 na kutoa kanuni mpya za mwaka 2023 na kutangazwa kwenye gazeti la Serikali Na. 42 la Oktoba, 2023 ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za kubadilisha fedha za kigeni nchini. Katika utoaji wa leseni, kanuni zimeweka madaraja matatu ya maduka (Daraja A, B na C) na kupunguza mtaji unaohitajika katika kuanzisha maduka hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko hayo yametoa fursa kwa hoteli zenye hadhi ya nyota tatu au zaidi kuomba leseni za kufanya biashara ya maduka ya kubadilisha fedha za kigeni kupitia dirisha la daraja C. Kufuatia marekebisho haya, idadi ya

maduka ya kubadilisha fedha za kigeni Zanzibar imeongezeka kutoka maduka 4 yenye matawi 11 hadi kufikia maduka 15 yenye matawi 35. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kanuni mpya zimesaidia kwa kiasi gani uendeshwaji wa maduka ya kubadilishia fedha za kigeni?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; mwaka 2017/2018, kulikuwa na utaratibu wa kuzuia leseni au kusitisha leseni za hawa wafanyabiashara wanaofanya biashara hii ya fedha za kigeni katika Mikoa ya Arusha na Dar es Salaam. Je, maduka yalikuwa mangapi na sasa hali ikoje ili shughuli ziendelee kama kawaida kwa wananchi hao? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mtaturu kama ifuatavyo, lakini kabla ya kujibu maswali hayo, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Mtaturu kwa ufuatiliaji mkubwa wa suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii imesaidia kwa kiasi kikubwa sana na ndiyo maana kwenye jibu langu la msingi nikasema, kwamba hata ongezeko la maduka ya ubadilishaji wa fedha za kigeni yameongezeka kutoka nne hadi kufikia 15. Hii ni kwa sababu pia ya punguzo lililopo kwenye mtaji ambao umegawiwa katika madaraja matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja A gharama yake ya mtaji ni shilingi 1,000,000,000, Daraja B ni shilingi 500,000,000 na Daraja C shilingi 200,000,000. Kwa hiyo, imeongeza idadi ya huduma hii ya maduka ya kubadilisha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, ni kweli mwaka alioutaja ilitokea kufutwa leseni kwa baadhi ya maduka na alitaka kujua idadi. Idadi ya maduka hayo yalikuwa ni 65 lakini kwa bahati nzuri maduka 61 tayari yamesharejeshewa gharama zao na yamepewa leseni huduma inaendelea. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Ikupa.

Na. 210

**Miundombinu Rafiki kwa Watu wenye Ulemavu katika Treni ya *SGR***

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha miundombinu na mazingira ya usafiri kwa watu wenye ulemavu inakuwa rafiki katika treni ya *SGR*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y. WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miundombinu ya reli pamoja na majengo umezingatia uwepo wa miundombinu wezeshi kwa watu wenye mahitaji maalumu ikiwa ni pamoja na uwekaji wa alama maalum zinazowasaidia kuwaongoza ndani ya majengo pamoja na huduma ya maliwato kwa kuweka vyoo maalum. Vilevile, katika mabehewa tumezingatia uwepo wa sehemu maalum kwa ajili ya kuwawezesha watu wenye mahitaji maalum kuweka viti vyao *(wheel chair)* pamoja na uwepo wa nukta nundu kuwasaidia kuona.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Shirika la Reli limenunua na litaendelea kununua na kuweka viti maalum *(wheel chairs)* katika majengo ya stesheni kwa lengo la watu wenye mahitaji maalum kutopata changamoto za utumiaji wa huduma za treni. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ikupa.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuipongeza na kuishukuru sana Serikali, pamoja na kwamba *SGR* ina muda mfupi katika utendaji wake, lakini mambo mengi yamekwishafanyika kwa kundi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; Serikali inaonaje sasa ikachukua ule utaratibu ambao umekuwa ukitumika na viwanja vya ndege kote duniani, kwa kuwa na watumishi maalum wa kulihudumia kundi hili pale wanapofika kwenye vituo, mpaka kuwawezesha kuingia kwenye treni. Tofauti na ilivyo sasa hivi, wamekuwa wakipata shida wanapofika kwa sababu kila mtu anaona siyo jukumu lake kuhudumia mtu kama huyu yaani ni mpaka mtu ajitolee.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ninaishukuru Serikali kuna ngazi mserereko kwenye *SGR* lakini ngazi mserereko hizi ni *too steep*. Ninaomba Serikali iweze kuzibadilisha na ziwekwe ngazi mserereko ambazo zinakuwa zina *gentle slope*. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu mambo mengi yameendelea kuboreshwa kutokana na maombi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwamba maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni kuhakikisha kwamba safari za treni na hasa *SGR* zinakuwa bora na rafiki lakini pia kuwa na viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kuboresha kadri tutakavyokuwa tunapata maoni. Kwa maswali yake yote mawili, moja la kuwa na wasaidizi, lakini pia kuwa na ngazi mserereko rafiki *(ramp)*, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba

Serikali tumelichukua na tutahakikisha kwamba katika kurekebisha hizo ngazi mserereko, tutahitaji pia tuweze kuwashirikisha wanufaika ikiwa ni pamoja na mambo mengine kuhakikisha kwamba usafiri wa *SGR* unakuwa ni rafiki. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Zedi.

Na. 211

**Kuwawezesha Wajasiriamali Wanaoongeza Thamani ya Mazao**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kutoa mafunzo ya utaalam, mitaji, kuwaunganisha na masoko wajasiriamali wanaoongeza thamani ya mazao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo Tanzania *(SIDO)* inaendelea na utekelezaji wa mpango wake wa kuwawezesha wajasiriamali katika shughuli zao ikiwa ni pamoja na uongezaji thamani mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji huo hufanywa kwa kutoa mafunzo, ushauri, uwezeshaji upatikanaji wa teknolojia za usindikaji wa mazao ya kilimo na uchakataji wa bidhaa mbalimbali, kuwawezesha Wajasiriamali kupata mitaji ambapo *SIDO* imekuwa ikitoa mikopo midogo pamoja na kuwaunganisha wajasiriamali wenye mahitaji ya mikopo mikubwa na Taasisi za kifedha ambazo Shirika limeingia nazo makubaliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwaunganisha pia wajasiriamali kushiriki katika maonesho yanayoandaliwa na wadau mbalimbali kitaifa na kimataifa kwa lengo la kutangaza bidhaa na kupata soko la bidhaa zao. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zedi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amejibu, Jimbo la Bukene lina fursa za kiuchumi nyingi sana kupitia uchakataji na uongezaji thamani ya mazao kama kusindika mafuta ya alizeti, kuchakata mchele, kuchakata unga wa sembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali inaweza kuwaleta wataalam wake Jimboni Bukene ili wakae na hao wajasiriamali wawafundishe namna ya kupata mitaji? Namna ya kuboresha bidhaa zao na kuwaunganisha kwenye masoko makubwa ili bidhaa zao ziweze kupata masoko?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Selemani Zedi kwa jitihada kubwa anazozifanya kuwasaidia wananchi wa Bukene ambao ni wajasiriamali kwenye sekta ya uongezaji thamani mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu ameweka nguvu kubwa katika Sekta ya Kilimo na sasa hatua inayofuata ni kuona namna gani haya anayosema Mheshimiwa Mbunge, moja, kuwasaidia wajasiriamali kusindika, kuongeza thamani mazao ya kilimo ikiwemo mahindi mchele na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, sisi kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, kupitia shirika letu la Maendeleo ya Viwanda Vidogo *(SIDO)* lakini pia kupitia *TBS*, tumeshaweka mpango na kuna bajeti mahususi ambayo moja inasaidia kutoa mafunzo, lakini pili kuwasaidia hata kujenga mabanda kwa maana sehemu nzuri za kutayarishia bidhaa zao za kilimo, lakini kuwasaidia teknolojia rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba wataalam hawa kutoka *SIDO* na

*TBS* ambako tayari tuna mpango huu wa kuwasaidia wajasiriamali wadogo, watakuja ili washirikiane na Mheshimiwa Mbunge kukaa na wananchi na wajasiriamali hawa ambao Mheshimiwa Mbunge anawasemea ili wapate mafunzo na teknolojia rahisi na mikopo, lakini zaidi kutafuta masoko kupitia maonesho na mipango mingine. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Janeth Mahawanga.

Na. 212

**Mafunzo kwa Wasindikaji Wadogo wa Vyakula Nchini**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza:-

Je, lini *TBS* itaweka utaratibu wa kutoa elimu kwa Wajasiriamali wadogo wanaojihusisha na biashara ya kusindika vyakula?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kupitia Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)*, imekuwa na utaratibu wa kutoa mafunzo kwa Wajasiriamali wadogo na wa kati wanaojihusisha na biashara ya kusindika bidhaa mbalimbali ikiwemo bidhaa za vyakula. Mafunzo hayo hutolewa kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Shirika na Mpango Kazi wa Mafunzo kwa Wajasiriamali unaoandaliwa kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mpango huo, mafunzo hayo ambayo yamekuwa yakitolewa kwa kushirikiana na *SIDO* na utaratibu huo umesaidia, si tu kusindika vyakula, bali na kupata teknolojia sahihi zinazosaidia kuzalisha bidhaa zenye viwango, lakini pia kupata mikopo, majengo na elimu ya biashara na masoko. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janeth.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. *TBS* inawasaidiaje wajasiriamali wadogo wanaoishi nje ya Dar es Salaam kupata huduma kwa njia rahisi badala ya kusafiri umbali mrefu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Ni kwa namna gani *TBS* inashughulikia changamoto ya upatikanaji wa vyeti vya ubora kwa wajasiriamali wadogo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninampongeza dada yangu Mbunge, Mheshimiwa Janeth Mahawanga kwa ufuatiliaji katika kuhakikisha wajasiriamali hapa nchini wanafanikiwa. Hii siyo mara ya kwanza na amekuwa akifuatilia, ninamshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, sisi kama Wizara kupitia *TBS* tuna ofisi za kanda katika kanda saba ambazo hizo zinasaidia kuhakikisha wajasiriamali hawalazimiki kuja au kwenda Dar es Salaam ili kupata huduma ya kupata ubora. Pili, katika kanda hizo hata kwenye mikoa pia tunao wawakilishi. Kwa hiyo, hii inawasaidia wajasiriamali hao kuhakikisha hawalazimiki kusafiri kwenda mpaka Dar es Salaam. Watatumia kwenye kanda hizo; tuna Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam), Kanda ya Magharibi, Kaskazini, Kusini, Kati (Dodoma), Nyanda za Juu Kusini na Mwanza. Pia, katika mikoa tunao wawakilishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, ni kweli kumekuwa na changamoto wakati mwingine kupata hati au vyeti vya ubora na ndiyo maana sasa tumeanza kutoa au kuhudumia wajasiriamali kupitia njia za kimtandao (kielektroniki). Kwa hiyo, mjasiriamali kwenye mtandao ana dirisha ambapo atatoa maelezo ya bidhaa; yale maelezo yatatusaidia sisi au afisa wa *TBS* kupitia na

kuona nini kinahitajika. Kama kuna masuala ya kumweleza kwenye mtandao atamweleza lakini kama ni kwenda kumfundisha atamfuata yeye, siyo mteja aje ofisini. Hii inapunguza ule usumbufu au kuchelewesha kutoa vyeti kwa wajasiriamali ambao wanataka nembo ya ubora kwa kuwafuata pale walipo. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Kanyasu.

Na. 213

**Malipo ya Fidia Wananchi wa Kata za Kasamwa na Nyankumbu Geita Mjini**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza:-

Je, lini Wananchi wa Kata za Kasamwa na Nyamkumbu - Geita Mjini watalipwa fidia kutokana na alama za barabara kuwekwa katika maeneno yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Kata ya Kasamwa na Nyankumbu waliowekewa alama za *X* ya kijani ni wale ambao wamo katika eneo la hifadhi ya barabara lililoongezwa kutoka meta 22.5 hadi mita 30 kila upande kulingana na Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa uchambuzi wa kina unafanyika ili kubaini ni barabara zipi kweli zinahitaji upana wa eneo la hifadhi ya barabara wa mita 60 kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na hapo baadaye ya kuzipanua kulingana na ongezeko la wingi wa magari. Zoezi hili likikamilika taarifa ya Serikali itatolewa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ingawa majibu haya pia niliyapata miaka mitatu iliyopita na sijajua zoezi litakamilika lini. Ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; Sheria ya Fidia inatoa fidia kulipia maendelezo ambayo yamekutwa pale *site,* kwa sababu muda unakuwa mwingi, *assest* zilizopo zinabomoka na zinapotea. Je, Waziri haoni kwamba wakati Serikali inakamilisha uchunguzi itakuta maeneo yale tayari yameshakuwa wazi na hivyo yatakuwa hayana thamani ya mwanzo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Barabara ya kutoka Mwanza kwenda Bukoba ambayo inapita katikati ya Mji wa Geita ilijengwa bila mitaro. Kwa hiyo, kila mvua inaponyesha inasababisha mafuriko kwenye Mji wa Geita. Je, ni lini Wizara itawapatia *TANROADS* fedha waweze kuweka mitaro kwenye Mji wa Geita? Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Fidia iko wazi sana, pale ambapo inakuwa imepita miezi sita tunalipa riba, kwa miaka miwili maana yake lazima turudie kufanya tathmini ya ulipaji wa fidia. Hili litafanyika kama itaonekana kwamba kwenye hili eneo hawa watu wanatakiwa kulipwa fidia na kuondolewa ili kupisha ujenzi. Hii ni sambamba na maeneo yote katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, siyo mara ya kwanza, aliliuliza na ameliuliza tena. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunavyoongea sasa hivi tulishatenga fedha na tumeshampata mkandarasi; na utekelezaji wa kutengeneza mitaro upya katika Mji wa Geita likiwepo lile eneo la karibu na stendi, mkataba uko kwa mwanasheria ili mkandarasi huyo aanze utekelezaji katika mwaka huu wa bajeti tunaoendelea nao.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Mheshimiwa Shally Raymond.

Na. 214

**Vituo vya Umahiri vya Sayansi na Teknolojia**
***(Centres of Excellence)***

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

Je, vituo vingapi vya umahiri vya sayansi na teknolojia na Akili Mnemba katika Taasisi za Elimu ya Juu vimeanzishwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanzisha jumla ya vituo vya umahiri 13 kati ya vituo 13, sawa na 100% ya lengo la miaka mitano katika Taasisi za Elimu ya Juu. Lengo la kuanzishwa kwa vituo hivyo ni kuimarisha uwezo katika utoaji wa elimu ya juu na utafiti katika maeneo ya afya na baiolojia ya molekuli; TEHAMA; kilimo na mifugo; maji na nishati jadidifu. Aidha, Serikali itaendelea kuanzisha vituo vipya vya umahiri kulingana na mahitaji, hususan katika kuimarisha mchango wa utafiti na ubunifu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza la nyongeza; ningependa kufahamu kuhusu TEHAMA katika hivyo vituo 13, je, matumizi ya Akili Mnemba *(Artificial Intelligence)* yako kwa kiwango gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; taasisi binafsi za elimu ya juu zinawezeshwa vipi na Serikali kwa kuanzisha vituo vya umahiri vya sayansi na teknolojia? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shally Raymond, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya Akili Mnemba (Akili Unde/*Artificial Intelligence)* lengo kuu la hii *AI* inatumika kama kiwezeshi. Sasa ninaomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu lengo la matumizi ya akili hizi ni kuimarisha ubora pamoja na teknolojia katika bidhaa mbalimbali. Tumekuwa tukitumia karibu katika vituo vyetu vyote hivi. Kwa hiyo, hakuna *separation* kwamba kituo hiki kinatumia Akili Mnemba au kituo hiki hakitumii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vituo vyetu hivi vya umahiri vyote 13 tumeweza kutumia masuala haya ya Akili Unde au Akili Mnemba kwa namna moja au nyingine. Chuo chetu cha *DIT* pale Dar es Salaam chenyewe hasa kimejikita kwenye masuala hayo ya TEHAMA kama ni kituo cha umahiri kinachofanya utafiti katika masuala ya TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la pili, Serikali kupitia Tume yetu ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)* ndiyo ambayo imepewa mamlaka ya kuratibu masuala haya ya ubunifu na imekuwa ikitoa mafunzo ya mara kwa mara kwenye taasisi zetu za elimu ya juu zile za binafsi na zile za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunavisaidia vituo vyetu hivi vya elimu ya juu vya binafsi kwa kupitia Tume yetu ya Sayansi na Teknolojia pale Dar es Salaam kwa kutoa mafunzo ya mara kwa mara. Hata hivyo, kwenye vituo hivi 13 vya umahiri nilivyovitaja, hata hizi taasisi binafsi zinaruhusiwa kwenda kufanya utafiti na kutumia vifaa vilivyopo kwenye vituo hivi vya umma kwa ajili ya kuendeleza tafiti zao hata zile taasisi zetu binafsi zinaruhusiwa kwenda. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa muda wetu umekwisha na maswali yamekwisha.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Tunao wageni wa Spika ambao ni wageni wawili kutoka Nchini Kenya *(Friends of Samia)*. Wageni hawa ni vijana wanaovutiwa sana na maendeleo yanayotekelezwa kwa kasi na ufanisi mkubwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wanaziona juhudi za Mheshimiwa Samia kama mfano bora wa Uongozi na Dira ya Maendeleo kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Wageni hao ni Ndugu Vincent Azrone Atonga na Ndugu Kevin Onyango Odhiambo, karibuni. *(Makofi)*

Vilevile tunao wageni waliokaa Jukwaa la Spika; wageni nane wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha ambao ni Viongozi na Wasaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG);* Ndugu George Haule - Naibu Mkaguzi Mkuu Ufanisi; Ndugu Wendy Massoy - Naibu Mkaguzi Mkuu Serikali Kuu; Ndugu Salhina Mkumba - Naibu Mkaguzi Mkuu Mashirika ya Umma; Ndugu Kubela Mwakatunda - Naibu Mkaguzi Mkuu Serikali za Mitaa; Ndugu Benja Majura - Naibu Mkaguzi Mkuu Hesabu za Taifa; Ndugu Seleman Mwamba - Mkurugenzi wa Mipango; Ndugu Nsia Maiko - Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa Kimataifa na Ndugu Elibariki Lyatuu - Mratibu wa Shughuli za *CAG* Bungeni, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira; Mhandisi Cyprian Luhemeja - Katibu Mkuu na Dkt. Immaculate Sware Semesi - Mkurugenzi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Dkt. Sware alikuwa Mbunge makini sana hapa, hongera sana. *(Makofi)*

Vilevile tunao wageni wengine 29 wa Mheshimiwa Masauni ambao ni watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais kutoka Makao Makuu, Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Aidha, tunao wageni sita wa Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo ambao ni wafanyakazi wa Kampuni ya Isuzu Tanzania,

wakiongozwa na Meneja wao, Ndugu Anurup Chatterjee kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa kuhudhuria maonesho ambayo yanafanywa na kampuni hii pale *opposite* na *Shoppers Plaza*. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge; mgeni wa Mheshimiwa Deogratus Ndejembi, Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maendeleo ya Makazi ambaye ni Ndugu Goodluck Lukumay kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu, Kazi Maalum ambaye ni Mwalimu Deo Mandanda, mjukuu wake kutoka Mkoa wa Mtwara. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Hamza Khamisi Hamza - Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Ndugu Aloyce Kamando, Balozi wa Mazingira, Ofisi ya Makamu wa Rais, kutoka Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao vilevile wageni watatu wa Mheshimiwa Maryprisca Winfred Mahundi - Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni 41 wa Mheshimiwa Khalifa Salum ambao ni viongozi wa dini (Maimamu na Wachungaji) kutoka Tunguu Zanzibar, karibuni. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Suma Fyandomo, Ndugu Hassan Ally Yassin, Mwenyekiti wa UVCCM, Kata ya Mikocheni A, Wilaya ya Kinondoni, Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Aidha, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Sylvia Sigula ambao ni wafanyabiashara wa Kampuni ya *Kengele Printers* na *Lwama Construction* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo ambao ni wapiga kura wake kutoka Arumeru Mashariki wanaoishi Jijini Dodoma, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Ghati Chomete, ndugu zake kutoka Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Ravia Idarus Faina ambao ni viongozi wa Tawi la CCM Kijini, Makunduchi, Mkoa wa Kusini Unguja, karibuni sana. (*Makofi)*

Tunao wageni 28 wa Mheshimiwa Mrisho Gambo, viongozi wa Kata ya Themi kutoka Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Esther Matiko ambao ni viongozi wa Bunge la Jumuiya ya Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)*. *(Makofi)*

Vilevile, tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo wanafunzi 75 wa Taasisi ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM),* karibuni. *(Makofi)*

Pia tunao wanafunzi watano wa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo kutoka Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Tunaye pia Ndugu Omary Magidi kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Tangazo lingine; Mheshimiwa Rashid Shangazi - *MNEC* Katibu wa Wabunge wa CCM Bungeni, anaomba kuwatangazia kikao muhimu sana Wabunge wa Viti Maalum wa CCM, leo tarehe 12 Februari saa 8.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Wote mfike bila kukosa, ahsanteni sana.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA ZA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2024 *(The Environmental Management (Amendments) Bill, 2024)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa ninamwita mwenye Muswada, Mheshimiwa Waziri na Mwenyekiti jiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2024, (*The Environmental Management (Amendments) Bill, 2024),* katika Bunge lako Tukufu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa uzalendo wa hali ya juu. Ninaomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumwombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjaalie kila la heri katika kuliongoza Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninapenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Kassim Majaliwa majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa shukurani kama sitomshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Spika; wewe binafsi Mheshimiwa Naibu Spika; pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ya ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia sheria na kanuni zinazoliongoza Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali. Kwa nafasi ya kipekee ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Kabudi kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Mheshimiwa Jerry William Silaa kuwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro kuwa Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Waziri wa Mifugo na Uvuvi; Mheshimiwa Abdallah Ulega, kuwa Waziri wa Ujenzi; Mheshimiwa Innocent Bashungwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; na bila kujisahau mimi mwenyewe kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena ninaendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kunipatia majukumu zaidi ya kumsaidia katika sekta hii mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa niaba ya Ofisi ya Makamu wa Rais, ninawatakia kila la heri katika kutekeleza majukumu yao mapya Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa na ninaahidi kuendelea kuwapa ushirikiano wa kutosha katika kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bwana Baraka Leonard na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kukuahidi kwamba mimi na Ofisi yangu tutaendelea kutoa ushirikiano kwa Bunge lako Tukufu katika kutekeleza majukumu yake. Ninawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Mheshimiwa Hamza Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Bwana Samwel Maneno, kwa kuendelea kutekeleza vema majukumu yao ya kazi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninampongeza Ndugu Onorius Njole, Mwandishi Mkuu wa Serikali ambaye alitoa ushirikiano wa karibu kwa Ofisi ya Makamu wa Rais wakati wa maandalizi ya Muswada huu. Kipekee, ninaomba kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira inayoongozwa na Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Mbunge wa Kalenga pamoja na Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua Muswada huu mbele ya Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa makini na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta jedwali la marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2024 *(The Environmental Management (Amendment) Bill, 2024)* unaopendekeza kufanya marekebisho katika vifungu mbalimbali vya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura Na. 191.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura Na. 191, ilitungwa na Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwaka 2004, ili kuweka Mfumo wa Kisheria na Kitaasisi wa Usimamizi Endelevu wa Mazingira. Kuweka msingi wa usimamizi, tathimini na kuchukua tahadhari kuhusu madhara ya mazingira. Kinga na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira; usimamizi wa taka, ubora wa viwango vya mazingira;

ushirikishwaji umma; utekelezaji wa sheria; kuweka misingi ya utekelezaji wa makubaliano ya kimataifa; kutekeleza Sera ya Kitaifa ya Mazingira tangu kutungwa kwake. Sheria hiyo imefanyiwa marekebisho mara tatu kupitia Sheria Na. 13 ya mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Na.4 ya mwaka 2020/2021 na Sheria Na.5 ya mwaka 2020/2021 ilikuwa ni kuhakikisha uzingatiaji wa viwango vya kitaifa na kimataifa katika usimamizi wa mazingira. Lengo la jumla la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha Sheria hiyo kuendana na Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2020/2021 na kutatua baadhi ya changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu Masharti ya Utangulizi na Sehemu ya Pili inabainisha Marekebisho katika Vifungu Mbalimbali vya Sheria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 2 ya Muswada inapendekeza Marekebisho katika Kifungu cha 3 cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekeza kurekebishwa kwa kuboreshwa tafsiri ya msamiati "*solid wastes*", ili kutoa maana yake sahihi. Kifungu hiki kinafanya marekebisho kwa kuweka tafsiri mpya ya msamiati "*water source*", ili kutoa tafsiri sahihi ya neno, kama ilivyokusudiwa, kutumika katika Sheria na kuongeza tafsiri ya maneno "*climate change, climate change management, climate system, climate change impact and vulnerability assessment emission, energy transitions, greenhouse gases and vulnerability*" ili kuweza kutoa maana yake sahihi, hususan katika eneo la mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 3 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 13. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kujumuishwa masuala yanayohusiana na mabadiliko ya tabianchi katika masuala ambayo yanasimamiwa na Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya mapendekezo haya ya marekebisho ni kumpa Waziri mamlaka ya kudhibiti na kusimamia masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Pia, kuhakikisha kuwa, Waziri mwenye dhamana ya masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi anapata wasaa wa kutoa maoni yake kabla ya mipango ya kitaifa ya maendeleo haijapitishwa na mamlaka husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 4 ya Muswada inapendekeza marekebisho ya kifungu cha 13 cha Sheria kwa kuongeza vifungu vidogo vya (5) na (6) kwa lengo la kuhakikisha kuwa, pale ambapo mipango ya maendeleo ya kitaifa kabla haijapitishwa, Waziri mwenye dhamana ya mazingira anatoa maoni yake. Pia, kuhakikisha kuwa, Waziri mwenye dhamana ya fedha kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya mazingira wanahamasisha upatikanaji wa fedha, kwa ajili ya shughuli za mabadiliko ya tabiachi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, Serikali inapendekeza Marekebisho kifungu cha 15 cha Sheria kwa kuongeza aya nyingine, ili kuhakikisha kuwa, masuala ya uratibu na tathimini za mabadiliko ya tabianchi zinafanyika. Pia, kuweka mikakati ya kukabiliana na kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwa sekta zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 18(2) kinapendekezwa kurekebishwa, ili kuongeza maneno "*and climate change system*" baada ya neno "*environmental*", ili kuhakikisha kuwa, masuala ya mabadiliko ya tabianchi yanaingizwa kwenye masuala ya viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya 3 ya Sheria inapendekezwa kurekebishwa na kuongezwa Sehemu Ndogo (e) inayoanzisha Kituo cha Taifa cha Kuratibu *Carbon (NCMC),* Kubainisha malengo ya kuanzishwa kituo na majumuku yake, pamoja na kuweka masharti kuhusu uongozi na vyanzo vya fedha za kituo. Kituo hiki tayari kipo Mkoani Morogoro na kimeendelea kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kutokana na kutokutambuliwa kisheria kituo hiki kinashindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ikiwa ni pamoja na kushindwa kuingia mikataba ya kitaifa na kimataifa na hivyo, kukosa fedha nyingi zinazohusiana na masuala ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na biashara ya *carbon*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kituo kinashindwa kusimamia kwa karibu masuala ya uuzaji na ununuzi wa viwango vya *carbon,* kwani hakitambuliki kisheria. Pia, kituo hiki kimekuwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais tangu kuanzishwa kwake na hivyo, kinategemewa kuendelea kuwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, ili kuendelea kutoa huduma kwa ufanisi zaidi, hususan katika eneo la mabadiliko ya tabianchi na biashara ya *carbon* kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vifungu vya 30 na 31 vinapendekezwa kurebishwa na kuviongezea Vitengo vya Usimamizi wa Mazingira vinavyoanzishwa katika Wizara na Taasisi mbalimbali kwa jukumu la kushughulikia pia, masuala ya mabadiliko ya tabiachi. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa, Wizara ya Kisekta inatekeleza masuala ya mabadiliko ya tabianchi kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 5 ya Muswada inapendekeza Marekebisho ya kifungu cha 36 cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa, ili kuondoa sifa na vigezo vya kitaaluma kwa Maafisa Usimamizi wa Mazingira na badala yake kuwa na vigezo stahiki vya elimu. Lengo la marekebisho haya ni kuruhusu masuala kuhusu kiwango cha elimu inayohitajika kushughulikiwa katika muundo wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kifungu kinapendekezwa kurekebishwa pia, ili kujumuisha tathimini nyingine zinazoibuka za mazingira zitakazofuatiliwa, kuhakikiwa na kuidhinishwa na Afisa Mazingira. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuwa na Maafisa wenye vigezo, kwa ajili ya utekelezaji bora wa malengo ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 6 ya Muswada inapendekeza Marekebisho katika Kifungu cha 42 cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kutoa muda ambao Mamlaka ya Serikali za Mitaa inatakiwa kuandaa na kuwasilisha mpango kazi wa mazingira kwa Waziri. Lengo la marekebisho haya ni kubainisha muda maalum wa kuandaa na kuwasilisha mpango kazi kwa Waziri kwa lengo la kuchambuliwa na kupitishwa, kama mpango wa Ofisi ya Makamu wa Rais na kuwekewa utaratibu wa kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kifungu cha 42 kinapendekezwa kurekebishwa, ili kuongeza aya zinazohusika na mabadiliko ya tabianchi katika upangaji wa mipango ya maendeleo. Lengo ni kuhakikisha kuwa, mipango ya maendeleo inazingatia masuala ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 7 na Muswada inapendekeza Marekebisho ya Kifungu cha 51(1). Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa, ili kuweka sharti la Waziri kushauriana na Wizara za Kisekta kabla ya kutangaza maeneo muhimu kwa mazingira. Lengo la marekebisho haya ni kumuwezesha Waziri kupata ushauri wa kitaalam kutoka Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 8 ya Muswada inapendekeza Marekebisho ya Kifungu cha 55 cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurebishwa ili kujumuisha bahari kama miongoni mwa eneo linalohifadhiwa. Madhumuni ya marekebisho haya ni kulipa Baraza na Serikali za Mitaa mamlaka ya kutoa miongozo na kuainisha hatua za kuchukua katika kulinda Bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 9 ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Kifungu cha 56(1) cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti yanayomtaka Waziri wakati wa kutangaza ardhi oevu kushauriana na Mawaziri wa Kisekta badala ya kushauriana na Waziri wa Ardhi pekee. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa, Waziri anapata ushauri wa kitaalam kutoka kwa Mawaziri wa Sekta husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 10 ya Muswada inapendekeza Marekebisho katika Kifungu cha 57(1) cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurebishwa, ili kutambua bahari au ziwa asilia, mwambao, ukingo wa mto au bwawa, kama vyanzo vya maji, ili kuendana na mapendekezo ya marekebisho chini ya Kifungu cha 3. Lengo la marekebisho haya ni kuvitambua na kuvilinda vyanzo vyote vya maji nchini, chini ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali ya Maji, Sura Na. 331.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 11 ya Muswada inapendekeza Marekebisho katika Kifungu cha 60C cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurebishwa, ili kumwondolea Afisa Maji jukumu la kujiridhisha na hatua za tahadhari zinazochukuliwa na mmiliki wa kibali kutumia maji na kumweka Mkurugenzi wa Bonde la Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho haya ni kuzingatia matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali ya Maji, Sura Na. 331, ambayo yanahitaji kazi zinazohusiana na kuchukua tahadhari kufanywa na Mkurugenzi wa Bonde la Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Jedwali la Marekebisho, Serikali inapendekeza kuongeza Marekebisho ya Kifungu cha 64 cha Sheria. Kifungu hicho kinafanyiwa marekebisho, ili kuwezesha kuwepo kwa kipindi cha mpito kutoka katika matumizi ya nishati chafu na kuingia katika nishati safi, kuhamasisha sera na teknolojia kuelekea matumizi ya nishati safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 12 ya Muswada inapendekeza Marekebisho ya Kifungu cha 75 cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurebishwa, ili kuanzisha mfumo ambao Sekta Binafsi inaweza kushiriki katika kuandaa na kutekeleza Sera ya Mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kwamba, Sera itakayotungwa ni bora na inatekelezeka kwenye kupambana na kuzuia mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Kifungu hicho kinapendekeza kurekebishwa pia, ili kuhakikisha mikakati na mipango ya mabadiliko ya tabianchi

inaendana na mipango ya Taifa na matakwa ya mikataba ya Kimataifa. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kwamba, nchi inaungana na juhudi za Kimataifa za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza kuongeza Kifungu cha 75A katika Sheria kwa lengo la kuimarisha mfumo wa kitaasisi kwa kuratibu masuala ya mabadiliko ya tabianchi, ambapo Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira inatambulika na pia, Kamati ya Taifa ya Mabadiliko ya Tabianchi kama ilivyobainishwa katika Muswada. Miongoni mwa majukumu yatakayotekelezwa na Kamati hii ni pamoja na kutoa ushauri kwa Waziri kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi kwa upana wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 80(3) cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa, ili kujumuisha udongo katika orodha ya masuala ambayo Waziri anaweza kuainisha mpango na hatua za kifedha, kwa ajili ya ulinzi wa mazingira. Madhumuni ya marekebisho haya ni kulinda ardhi dhidi ya utiririshaji wa maji taka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 104(7) kinapendezwa kurekebishwa na Kifungu cha 105 kinapendekezwa kuongezwa kwa kujumuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika tathmini za kimkakati za mazingira. Lengo la kujumuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika tathmini hiyo ni kubaini maeneo ambayo yanaweza kuathiriwa zaidi na mabadiliko ya tabianchi ili kuchukua tahadhari zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 15 ya Muswada inapendekeza Marekebisho ya kifungu cha 109 cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta neno “mkondo” na badala yake kuweka maneno “chanzo cha maji”. Lengo la marekebisho haya ni kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sura Na. 331, ambayo inajumuisha mkondo kama miongoni mwa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 16 ya Muswada inapendekeza marebisho ya kifungu cha 129(3) cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurebishwa, ili kujumuisha masharti yanayomtaka Waziri kushauriana na Wizara ya Kisekta katika kutengeneza Kanuni zitakazosimamia maji ya mvua. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa, Waziri anapata ushauri wa kitaalam kutoka katika Wizara za Kisekta zinazohusika wakati wa kuandaa Kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 17 ya Muswada inapendekezwa Marekebisho ya kifungu cha 140 cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kutambua Kamati za Kifundi na Waziri anayehusika na viwango katika uundaji wa uidhinishwaji wa viwango vya ubora na mazingira. Lengo la marekebisho haya ni kuzingatia Sheria ya Viwango, Sura Na. 130, ambayo ni sheria mahususi inayodhibiti viwango. Vilevile, Kifungu hiki kinarekebishwa pia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, twende kwenye Ibara za mwisho halafu utoe hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna mabadiliko katika Ibara ya 18 ambayo inafanya mabadiliko kwenye kifungu cha 168, Ibara ya 19 ambayo inafanya mabadiliko kwenye kifungu cha 169 na Ibara ya 20 ambayo inafanya mabadiliko katika kifungu 170(1).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jedwali la Marekebisho pia kuna marekebisho katika Ibara ya 100 kwa kuongeza Ibara ya 174A, pamoja na Jedwali na kifungu cha 179, ambapo kinarebishwa, ili kuimarisha mfumo wa ushirikishwaji wa Wizara ya Kisekta. Pia Ibara 21 na 25 za Muswada zinapendekeza kuboresha mfumo wa utatuzi wa malalamiko na wadau mbalimbali. Ibara ya 26 ya Muswada na yenyewe vilevile kuna marekebisho madogo, pamoja na Ibara ya 27 na 28, hizi vilevile zina mabadiliko madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2020/2023 kutoa hoja kwamba, huu Muswada wa Sheria ya Marebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2024 ujadiliwe na Kupitishwa na Bunge kwa hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na Tatu. Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2024 *(The Environmental Management (Amendments) Bill, 2024),* ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya Kusoma kwa Mara Pili na Mara ya Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja.

**MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA WA MWAKA 2024 *(THE ENVIRONMENTAL MANAGEMENT (AMENDMENTS) BILL, 2024)* - KAMA ULIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuingoza Nchi yetu kwa uzalendo wa hali ya juu. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumuombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, nitakuwa mchoyo wa shukrani kama nisipokushukuru na kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali.

**Mheshimiwa Spika** kwa nafasi ya pekee napenda kumpongeza Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mh. Rais kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mh. Jerry William Silaa kuwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mh. Dkt Damas Daniel Ndumbaro kuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mh. Mhandisi Hamadi Yussuf Masauni kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ashatu Kachwamba Kijaji kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mh. Abdallah Hamisi Ulega kuwa Waziri wa Ujenzi na Mh. Innocent Lugha Bashungwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa niaba ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Ninawatakia heri katika kutekeleza majukumu yenu mapya na ninaahidi kuendelea kuwapa ushirikiano wa kutosha katika kulitumikia Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, Ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bw. Baraka Ildiphonce Leonard na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Makamu wa Rais katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukuahidi kwamba mimi na Ofisi yangu tutaendelea kutoa ushirikiano kwa Bunge lako Tukufu katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, ninawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Bw. Samwel Marco Maneno kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vilevile, ninampongeza Ndg. Onorius John Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria ambaye alito

ushirikiano wa karibu kwa Ofisi ya Makamu wa Rais wakati wa maandalizi ya Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee naomba kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira inayoongozwa na Mhe. Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, pamoja na Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua Muswada huu mbele ya Kamati hiyo. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa makini na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2024 (The Environmental Management (Amendment) Bill, 2024) unaopendekeza kufanya marekebisho katika vifungu mbalimbali vya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 ilitungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2004 ,ili kuweka mfumo wa kisheria na kitaasisi wa usimamizi endelevu wa mazingira; kuweka misingi ya usimamizi, tathmini na kuchukua tahadhari kuhusu madhara kwa mazingira, kinga na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira, usimamizi wa taka, ubora wa viwango vya mazingira, ushirikishwaji umma, utekelezaji sheria; kuweka misingi ya utekelezaji wa makubaliano ya kimataifa; kutekeleza Sera ya Taifa ya Mazingira. Tangu kutungwa kwake, Sheria hiyo imefanyiwa marekebisho mara tatu kupitia Sheria Na. 13 ya 2016, Sheria Na. 4 ya 2021 na Sheria Na. 5 ya 2021 kwa nia ya kuhakikisha uzingatiaji wa viwango vya kitaifa na kimataifa katika usimamizi wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** lengo la jumla la marekebisho yanayopendekezwa ni kuiwezesha Sheria hiyo kuendana na Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 na kutatua baadhi ya changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi na Sehemu ya Pili inabainisha marekebisho katika vifungu mbalimbali vya Sheria kama ifuatavyo:

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 2 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 3 cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha tafsiri ya msamiati "solid waste" ili kutoa maana yake sahihi. Aidha, kifungu hiki kinafanyiwa marekebisho kwa kuweka tafsiri mpya ya msamiati "water source" ili kutoa tafsiri sahihi ya neno kama lilivyokusudiwa kutumika katika Sheria na kuongeza tafsiri za maneno: "climate change", "climate change management", "climate system", "climate change Impacts and vulnerability assessment", "emissions", "energy transition", "greenhouse gases" na "vulnerability" ili kuweza kutoa maana zake sahihi hususan katika eneo la mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 3 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 13. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kujumuisha masuala yanayohusiana na mabadiliko ya tabianchi katika masuala ambayo yanasimamiwa na Waziri. Madhumuni ya mapendekezo ya marekebisho hayo ni kumpa Waziri mamlaka ya kudhibiti na kusimamia masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Pia kuhakikisha kuwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi anapata wasaa wa kutoa maoni yake kabla mipango ya kitaifa ya maendeleo haijapitishwa na mamlaka husika.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 4 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 13 cha Sheria kwa kuongeza vifungu vidogo vya (5) na (6) kwa lengo la kuhakikisha kuwa pale ambapo mipango ya maendeleo ya kitaifa kabla haijapitishwa Waziri mwenye dhamana na Mazingira anatoa maoni yake na pia kuhakikisha kuwa Waziri mwenye dhamana na Fedha kwa kushauriana na waziri mwenye dhamana na Mazingira wanahamasisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli za mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,** kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, Serikali inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 15 cha Sheria kwa kuongeza aya zingine ili kuhakikisha kuwa masuala ya uratibu wa tathmini za mabadiliko ya tabianchi zinafanyika na pia kuweka mikakati ya kukabiliana na kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwa sekta zinazohusika.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 18(2) kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza maneno "and climate system" baada ya neno "Environmental" ili kuhakikisha kuwa masuala ya mabadiliko ya tabianchi yanaingizwa kwenye masuala ya viwango.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tatu ya Sheria inapendekezewa kurekebishwa kwa kuongeza sehemu ndogo ya (e) inayoanzisha Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni (NCMC), kubainisha malengo ya kuanzishwa Kituo na majukumu yake pamoja na kuweka masharti kuhusu uongozi na vyanzo vya fedha za Kituo.

**Mheshimiwa Spika**, Kituo hiki tayari kipo Mkoani Morogoro na kimeendelea kutekeleza majukumu yake. Aidha kutokana na kutokutambuliwa kisheria Kituo hiki kinashindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria ikiwa ni pamoja na kushindwa kuingia mikataba ya kitaifa na kimatifa na hivyo kukosa fedha nyingi zinazohusiana na masuala ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na biashara ya kaboni.

Vilevile kituo kinashindwa kusimamia kwa karibu masuala ya uuzaji na ununuzi wa viwango vya kaboni kwani hakitambuliki kisheria. Pia kituo hiki kimekuwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais tangu kuanzishwa kwake na hivyo kinategemewa kuendelea kuwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais ili kuendelea kutoa huduma kwa ufanisi zaidi hususan katika eneo la mabadiliko ya tabianchi na biashara ya Kaboni kwa ujumla wake.

**Mheshimiwa Spika,** vifungu vya 30 na 31 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuviongezea vitengo vya usimamizi wa mazingira vinavyoanzishwa katika wizara na taasisi mbalimbali jukumu la kushughulikia pia masuala ya mabadiliko ya tabianchi.

Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa Wizara za kisekta zinatekeleza masuala ya Mabadiliko ya tabianchi kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika** Ibara ya 5 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 36 cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa sifa ya vigezo vya kitaaluma kwa maafisa wa usimamizi wa mazingira na badala yake kuwa na vigezo stahiki vya elimu. Lengo la marekebisho haya ni kuruhusu masuala kuhusu kiwango cha elimu inayohitajika kushughulikiwa katika muundo wa Wizara. Aidha, kifungu kinapendekezwa kurekebishwa pia ili kujumuisha tathmini nyingine zinazoibuka za mazingira zitakazofuatiliwa, kuhakikiwa na kuidhinishwa na afisa mazingira. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuwa na maafisa wenye vigezo kwa ajili ya utekelezaji bora wa malengo ya Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 6 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 42 cha Sheria Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kutoa muda ambao mamlaka ya serikali za mitaa zinatakiwa kuandaa na kuwasilisha mpango kazi wa mazingira kwa Waziri.

Lengo la marekebisho haya ni kubainisha muda maalum wa kuandaa na kuwasilisha mpango kazi kwa Waziri kwa lengo la kuchambuliwa na kupitishwa kama mipango ya Ofisi ya Makamu wa Rais na kuwekewa utaratibu wa kutekelezwa. Vilevile, Kifungu cha 42(2) kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza aya inayohusika na mabadiliko ya tabianchi katika upangaji wa mipango ya maendeleo. Lengo ni kuhakikisha kuwa mipango ya maendeleo inazingatia masuala ya mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 7 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 51(1). Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka sharti la Waziri kushauriana na Wizara za kisekta kabla ya kutangaza maeneo muhimu kwa mazingira. Lengo la marekebisho haya ni kumwezesha Waziri kupata ushauri wa kitaalamu kutoka Wizara husika.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 8 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 55 cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kujumuisha bahari kama miongoni mwa eneo lililohifadhiwa. Madhumuni ya marekebisho haya ni kulipa Baraza na serikali za mitaa mamlaka ya kutoa miongozo na kuainisha hatua za kuchukua katika kulinda bahari.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 9 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 56(1) cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti yanayomtaka Waziri wakati wa kutangaza ardhi oevu kushauriana na mawaziri wa kisekta badala ya kushauriana na Waziri wa ardhi pekee. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa Waziri anapata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa mawaziri wa sekta husika.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 10 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 57(1) cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kutambua "bahari au ziwa asilia, mwambao, ukingo wa mto au bwawa" kama vyanzo vya maji ili kuendana na mapendekezo ya marekebisho chini ya kifungu cha 3. Lengo la marekebisho haya ni kuvitambua na kuvilinda vyanzo vyote vya maji chini ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sura ya 331.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 11 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 60(1) cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kumuondolea Afisa Maji jukumu la kujiridhisha na hatua za tahadhari zilizochukuliwa na mmiliki wa kibali cha kutumia maji na kumuweka Mkurugenzi wa Bonde la Maji. Lengo la marekebisho haya ni kuzingatia matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sura ya 331 ambayo yanahitaji kazi zinazohusiana na kuchukua tahadhari kufanywa na Mkurugenzi wa Bonde la Maji.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia Jedwali la Marekebisho Serikali inapendekeza kuongeza marekebisho ya kifungu cha 64 cha Sheria. Kifungu hicho kufanyiwa marekebisho ili kuwezesha kuwepo na kipindi cha mpito kutoka katika matumizi ya nishati

chafu na kuingia katika nishati safi na kuhamasisha Sera na teknolojia kuelekea matumizi ya nishati safi**.**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 12 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 75 cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kuanzisha mifumo ambayo sekta binafsi inaweza kushiriki katika kuandaa na kutekeleza sera ya mabadiliko ya tabianchi. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kwamba sera itakayotungwa ni bora na inatekelezeka kwenye kupambana na kuzuia mabadiliko ya tabianchi. Aidha, kifungu hicho kinapendekezwa kurekebishwa pia ili kuhakikisha mikakati na mipango ya mabadiliko ya tabianchi inaendana na mipango ya taifa na matakwa ya mikataba ya kimataifa. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kwamba nchi inaungana na juhudi za kimataifa za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza kuongeza kifungu cha 75A katika Sheria kwa lengo la kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa kuratibu masuala ya mabadiliko ya tabianchi ambapo Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira itatambulika pia kama Kamati ya Taifa ya Mabadiliko ya Tabianchi. Kama ilivyobainishwa katika Muswada, miongoni mwa majukukumu yatakayotekelezwa na Kamati hii ni pamoja na kutoa ushauri kwa Waziri kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi kwa upana wake.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 80(3) cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kujumuisha udongo katika orodha ya masuala ambayo Waziri anaweza kuainisha mpango na hatua za kifedha kwa ajili ya ulinzi wa mazingira. Madhumuni ya marekebisho haya ni kulinda ardhi dhidi ya utiririshaji wa maji taka.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 104(7) kinapendekezwa kurekebishwa na kifungu cha 105 kinapendekezwa uongezwa kwa kujumuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika tathmini za kimkakati za Mazingira. Lengo la kujumuisha masuala

ya mabadiliko ya tabianchi katika tathmini hiyo ni kubaini maeneo ambayo yanaweza kuathiriwa zaidi na mabadiliko ya tabianchi ili kuchukua tahathari zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 15 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 109 cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta neno "mkondo" na badala yake kuweka maneno "chanzo cha maji". Lengo la marekebisho haya ni kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sura ya 331, ambayo inajumuisha mkondo kama miongoni mwa vyanzo vya maji.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 16 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 129(3) cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kujumuisha masharti yanayomtaka Waziri kushauriana na Wizara za kisekta katika kutengeneza kanuni zinazosimamia maji ya mvua. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa Waziri anapata ushauri wa kitaalamu kutoka katika Wizara za kisekta zinazohusika wakati wa kuandaa kanuni.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 17 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 140 cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kutambua Kamati za Kiufundi na Waziri anayehusika na viwango katika uundaji na uidhinishaji wa viwango vya ubora wa mazingira. Lengo la marekebisho haya ni kuzingatia Sheria ya Viwango, Sura ya 130, ambayo ni sheria mahususi inayodhibiti viwango. Vilevile, kifungu hiki kinarekebishwa pia ili kujumuisha masuala ya uzalishaji wa gesijoto miongoni mwa maeneo ambayo yatawekewa viwango vya ubora.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 18 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 168 cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa neno "Wakala" na badala yake kuweka neno "Mamlaka" ili kutambua mabadiliko ya hadhi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Lengo la marekebisho haya ni kuendana na mabadiliko ya kisheria na kimuundo.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 19 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 169 cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kumjumuisha Waziri mwenye dhamana ya mawasiliano kuwa miongoni mwa Mawaziri watakaoshauriana na Waziri kabla ya kutunga kanuni zinazoeleza namna ya ushirikiano kati ya baraza na vyombo vilivyoanzishwa chini ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kwamba, Waziri anapata ushauri wa kitaalam kutoka katika Wizara ya mawasiliano kama mdau muhimu.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 20 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 170(1) cha Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa ili kuendana na mabadiliko ya majina ya Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu, na Wakala wa Maabara ya Mifugo Tanzania. Aidha, marekebisho yanafanyika pia kwa kuongeza taasisi za Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania, Shirika la Viwango Tanzania na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, ili waweze kutoa taarifa kwa Baraza kwa majukumu ambayo yana athari katika mazingira. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kwamba Baraza linapata taarifa ya majukumu yenye madhara katika mazingira ili kuchukua hatua stahiki za kulinda mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, kupitia Jedwali la Marekebisho Serikali inapendekeza kuongeza katika Sheria kifungu kipya cha 174A ili kumpa Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Taifa cha kuratibu Kaboni jukumu la kuanzisha mfumo wa tathmini za uzalishaji wa gesijoto, uandaaji wa taarifa za gesijoto na kuzitaka Wizara za kisekta kuandaa na kuwasilisha taarifa za gesijoto kwa Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni. Lengo la mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa tathmini ya uzalishaji wa gesijoto inafanyika kwa wakati na taarifa za uzalisha wa gesijoto kisekta zinawasilishwa kwa Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni kwa wakati kwa mujibu wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 179 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuimarisha mfumo wa ushirikishwaji wa wizara za kisekta katika mikataba ya kimataifa. Marekebisho haya

yanalenga kuwezesha Wizara za Kisekta kuhusishwa katika majadiliano yanayohusu mikataba ya kimataifa hususan ile ya mabadiliko ya tabianchi kabla ya kuridhiwa na mamlaka zinazohusika

**Mheshimiwa Spika,** Ibara za 21 hadi 25 za Muswada zinapendekeza kuboresha mfumo wa utatuzi wa malalamiko ya wadau mbalimbali yanayoweza kuibuka wakati wa utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Hata hivyo, baada ya majadiliano na Kamati na kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, Ibara hizi sasa zinapendekezwa kufutwa katika Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 26 ya Muswada inapendekeza kurekebisha viwango vya uzalishaji gesijoto kutolewa na Waziri mwenye dhamana ya viwango. Lengo ni kuhakikisha kuwa uzalishaji wa gesijoto vinatolewa na Wizara ya kisekta ili kuzingatia utaalamu katika eneo la viwango.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 27 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Jedwali la Kwanza la Sheria. Jedwali hili linapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha muda wa vikao vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Mazingira kwa kuwa hapakuwa na muda uliowekwa hapo awali. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa Kamati inafanya vikao vyake kadri itakavyoelekezwa katika Sheria na kuwezesha masuala ya mazingira kujadiliwa ndani ya muda unaofaa.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 28 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Jedwali la Pili la Sheria. Jedwali hili linapendekezwa kurekebishwa kwa kutoa neno Baraza na kuweka neno Bodi ili kurekebisha makosa yaliyokuwepo kwenye Jedwali. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa mikanganyiko.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa mwaka 2024 (the Environmental

Management (Amendments)Bill, 2024) ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu.

**Mheshimiwa Spika,** NINAOMBA KUTOA HOJA.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, hoja imeungwa mkono. Ahsante Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. AGNES E. HOKORORO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na uhai na kuweza kukutana siku ya leo. Naomba taarifa hii yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2020/2024 *[The Environmental Management (Amendment) Bill, 2024]* kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2020/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira iliupokea Muswada huu Mwezi Novemba, 2024, baada ya kusomwa Bungeni Mara ya Kwanza, Tarehe 8 Novemba, 2024 katika Mkutano wa Kumi na Saba, Kikao cha Tisa cha Bunge na Mheshimiwa Spika kuuelekeza kwenye Kamati yetu ili tuufanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata muda wa kuupitia Muswada na kupata ufafanuzi kutoka kwa Sekretarieti kwa

maeneo yaliyohitaji Utaalam wa Sheria. Baada ya kuupitia Kamati ilimualika Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ili aipitishe Kamati kwenye madhumuni na sababu za Muswada aliouwasilisha. Waziri alifafanua kifungu kwa kifungu akieleza sababu na madhumuni ya kila Ibara iliyomo katika Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ilitoa matangazo katika vyombo vya habari na kuwaalika wadau mbalimbali, ili waweze kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu. Mwaliko uliotolewa ulikusudia kuwapa wadau fursa ya kutoa maoni yao kuhusu Marekebisho ya Sheria katika Muswada husika. Wadau 21 walifika mbele ya Kamati, Tarehe 15 Januari, 2025 na kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo na Madhumuni ya Muswada. Muswada huu unapendekeza kurekebisha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, subiri kidogo.

Ninamwita Mwenyekiti wa Bunge aje mara moja kuchukua nafasi ya kukalia kiti. Mwenyekiti wa Kamati wewe endelea.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, endelea.

**MHE. AGNES E. HOKORORO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unapendekeza kurekebisha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 ili kukabiliana na baadhi ya changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada uliowasilishwa na Serikali una Ibara 28 zenye marekebisho madogo. Aidha, Serikali iliwasilisha Jedwali la Marekebisho katika maeneo mbalimbali ya Muswada. Baadhi ya mambo yaliyobainishwa katika Muswada na Jedwali la Marekebisho ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuzitaka Wizara za Kisekta kuwa na ama Sehemu au Kitengo kinachohusika na Usimamizi wa Mazingira;

(b) Kuboresha tafsiri za maneno "*solid waste*" na kuongeza tafsiri ya maneno "*water sources, climate change, climate change management, climate system, climate change vulnerability assessment, emissions, energy transition, greenhouse gases* na *vulnerability*";

(c) Kumwongezea Waziri Mamlaka ya kushughulikia masuala ya mabadiliko ya tabianchi, kudhibiti gesijoto, kushirikisha wadau katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kumwezesha kutunga kanuni juu ya masuala hayo;

(d) Kubadili sifa za Kitaaluma za Afisa Usimamizi wa Mazingira ngazi ya Halmashauri na kumwongezea majukumu na utaratibu wa kutoa taarifa za utekelezaji wa Sheria;

(e) Kuweka muda mahsusi wa miaka mitano kwa kila Halmashauri kuwasilisha kwa Waziri Mpango Mkakati wa mazingira;

(f) Kumtaka Waziri anayehusika na Mazingira kushauriana na Mawaziri wa Kisekta kabla ya kutangaza kanuni au maeneo yanayolindwa katika Gazeti la Serikali; *(Makofi)*

(g) Kuwapa Halmashauri jukumu la usimamizi wa mazingira katika Bahari;

(h) Kumtoa Afisa Maji na kumuweka Mkurugenzi wa Bonde kwa jukumu la kujiridhisha na hatua za tahadhari zilizochukuliwa na mmiliki wa kibali cha kutumia maji; *(Makofi)*

(i) Kuiongezea majukumu Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Mazingira ili iweze kutoa Ushauri kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi;

(j) Kulinda udongo;

(k) Kuliweka suala la utangazaji wa viwango chini ya Waziri husika;

(l) Kurekebisha majina ya taasisi na kuongeza nyingine ambazo zinahusika kimazingira;

(m) Kulipa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* uwezo wa kupokea maombi ya marejeo juu ya amri zake ilizotoa na Waziri kuwa na Mamlaka ya kufanya mapitio au kusikiliza rufaa;

(n) Kumtaka Waziri anayehusika na mazingira kwa kushirikiana na Waziri anayehusika na masuala ya fedha au Wizara ya Kisekta inayoguswa na jambo husika kwenye masuala yanayohusu uwezeshaji wa kifedha kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

(o) Kumtaka Waziri anayehusika na Mazingira kutoa ushauri kwa Mamlaka inayohusika na Mipango ya Kitaifa kabla ya kuidhinishwa kwake ili kuhakikisha masuala ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi yanazingatiwa kwa ukamilifu; na

(p) Kuanzishwa kwa Kituo cha Uratibu wa Biashara ya Kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa ujumla wa Muswada. Kamati inapongeza Serikali kwa kuleta Muswada wa Sheria ya Marekebisho madogo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Aidha, Kamati ilikuwa na matarajio ya kuleta Bungeni Muswada uliosheheni marekebisho makubwa ambayo Serikali na Kamati imekubaliana kwa nyakati tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia Maazimio mbalimbali ya Bunge na kufanya uchambuzi wa Muswada huu,

Kamati ilibaini kuwa bado yapo maeneo muhimu yanayohitaji kufanyiwa marekebisho na hayajahusishwa katika Muswada huu. Baadhi ya maeneo hayo ni:

(a) Kulifanya Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* kuwa Mamlaka; na

(b) Kuzingatia masuala ya Uchumi wa Bluu katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala hayo na mengine mengi ambayo hayakuzingatiwa katika Muswada huu yalijadiliwa katika kikao baina ya Kamati na Wizara ili kuona uwezekano wa kuyaingiza katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukubwa wa marekebisho ambayo Kamati ilihitaji, ilionekana ni vizuri marekebisho hayo kufanyika kwa Muswada mpya ambao utashirikisha wadau katika ngazi ya Serikali na kutangazwa katika Gazeti la Serikali ili Kamati itakapoushughulikia Muswada iweze kupata idadi kubwa ya wadau wa kutoa maoni katika Mswada huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifahamishwa kuwa Serikali ilihitaji muda zaidi ili kuandaa marekebisho makubwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira yatakayojumuisha maeneo muhimu. Kutokana na ahadi hiyo, Kamati iliendelea kufanyia kazi Muswada huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maoni na ushauri wa Kamati. Kwa ujumla Kamati ina ushauri kwenye Ibara ya 8 ambazo ni Ibara ya 4, 5, 21, 22, 23, 24, 25 na Ibara ya 29D iliyowasilishwa katika jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ibara ya 4 inayorekebisha Kifungu cha 13(1). Kamati ilibaini kuwa neno tabianchi limeongezwa katika sehemu moja tu ya kifungu cha 13(1) na hivyo kutofikia lengo lililokusudiwa. Aidha, Kamati iliona umuhimu wa Waziri kupewa pia Mamlaka ya kushughulikia mabadiliko ya

tabianchi kwa kujumuisha katika sera masuala ya upunguzaji wa gesijoto na mikakati ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Hivyo, Kamati ilipendekeza Kifungu hiki kisomeke kama ifuatavyo; kifungu cha 13(1); *The Minister shall be overall responsible for matters relating to the environment, climate change and shall, in that respect, be responsible for the articulation of Policy Guidelines necessary for the promotion, protection, sustainable management of the environment and the integration of climate change mitigation and adaptation strategies into Policy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekubaliana na mapendekezo ya Kamati na yamezingatiwa katika Jedwali la Marekebisho ya Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ibara ya 5 inayorekebisha kifungu cha 36, Muswada ilipendekeza kurekebisha kifungu cha 36(2), ili kuondoa sifa ya *Diploma* kwa Afisa Usimamizi wa Mazingira na kubakisha sifa ya Shahada pekee. Kamati ilishauri kuwa Ibara hiyo irekebishwe ili sifa za kielimu zisitajwe katika sheria na kubakia katika Muundo wa Utumishi. Kifungu hicho sasa kisomeke kama ifuatavyo; *A person designated or appointed by the City, Municipal, District or Town Environment Management Officer shall possess requisite academic qualifications and has competence in environmental management*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekubaliana na ushauri uliotolewa na Kamati. Kamati ilishauri kufutwa kwa Ibara ya 5B ya Muswada iliyopendekeza kurekebisha Kifungu cha 36(3)(h) kilichohusu uwasilishaji wa Taarifa ya Utekelezaji wa Sheria unaofanywa na Afisa Usimamizi wa Mazingira wa Halmashauri. Kamati iliona marekebisho haya yafanyiwe kazi katika marekebisho makubwa ya kimuundo na kimfumo yanayotarajiwa kuwasilishwa na Serikali. Ushauri wa Kamati umeridhiwa na kuzingatiwa na Serikali katika jedwali la marekebisho ya Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ibara za 21,22,23,24 na 25 katika ibara hizo zilipendekeza vifungu vya 195, 196,197,198 na 199, lengo la marekebisho hayo ni kutoa nafasi kwa *NEMC*

kupokea maombi na kufanya marejeo ya amri ilizotoa na kumruhusu mtu asiyeridhishwa na uamuzi wa Baraza hilo katika marejeo kuomba mapitio au rufaa kwa Waziri ndani ya siku thelathini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilishauri Ibara hizo zifutwe kwa kuwa Serikali imeahidi kuleta marekebisho makubwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura Na. 191. Marekebisho hayo pamoja na mambo mengine yatahusiana na masuala ya utoaji haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekubaliana na ushauri wa Kamati na Ibara hizo kufutwa kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri kuhusu mambo yaliyoongezwa kwenye jedwali la marekebisho. Katika eneo hili, naomba kutanguliza maelezo yafuatayo:

(a) Tangu awali Kamati ilipopitia jumla ya Ibara 28 za Muswada, ilibaini kusahaulika kwa jambo muhimu miongoni mwa mengine lililohusu usimamizi wa Biashara ya Kaboni;

(b) Utaratibu wa Kamati kushughulikia Miswada ya Sheria umewekewa masharti yaliyobainisha pamoja na mambo mengine, wigo wa jukumu na Madaraka ya Kamati. Kwa mujibu wa Kanuni ya 97(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, uwezo wa Kamati kufanya marekebisho kwenye Muswada ni wa kumshauri mtoa hoja. Aidha, kwa desturi za Kibunge ushauri huo unagusa yale tu yaliyomo kwenye Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikuwa na maoni kwamba, si jambo jema kukosa masharti ya kisheria yanayohusu usimamizi mzuri wa biashara ya kaboni. Kwa msingi huo, ili kuhakikisha kuwa manufaa ya kiuchumi yanapatikana huku mazingira yakihifadhiwa kwa kizazi cha sasa na kijacho, marekebisho ya sheria yanayoweka masharti ya usimamizi wa biashara ya kaboni ni jambo muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inamshukuru mtoa hoja ambaye alizingatia maoni hayo na kuongeza kwenye jedwali la marekebisho mapendekezo yanayogusa usimamizi wa biashara hiyo. Hata hivyo, katika Ibara ya 29D (1) ya jedwali ilipendekeza kuwepo kwa Mkurugenzi na Bodi ya Wakurugenzi wa Kituo cha Uratibu wa biashara ya kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, muda wa ukomo kwa Wajumbe wa Bodi haukutajwa katika marekebisho hayo. Kwa muktadha huo, Kamati ilishauri kurekebishwa kwa Ibara hiyo ili kuonesha namna ambavyo Mkurugenzi wa Kituo hicho atapatikana pamoja na ukomo wa Wajumbe wa Bodi. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na kuuzingatia kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hitimisho, kwa kuzingatia uchambuzi wa Kamati, madhumuni na sababu za kutungwa kwa Sheria hii, Kamati imeridhishwa na marekebisho madogo yaliyofanywa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ili kukidhi matarajio ya Bunge, wananchi na maudhui ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021, Kamati inaona kuwa ipo haja kwa Serikali kuleta Miswada ya Sheria mipya itakayowezesha kutungwa kwa Sheria ya kulifanya Baraza la Taifa la Mazingira kuwa Mamlaka pamoja na Sheria ya Masuala ya Uchumi wa Buluu. Ni matarajio ya Kamati kwamba Serikali italeta Miswada hiyo mapema wakati wa Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge kama ilivyoahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana wewe kwa kutoa kibali ili Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira iweze kuufanyia kazi Muswada huu na kuipa fursa ya kuwasilisha maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Spika kwa kutoa kibali ili Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira iweze kuufanyia kazi Muswada huu na kuipatia fursa ya kuwasilisha maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yusuf Masauni, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Naibu Waziri Mheshimiwa Mbunge Khamis Hamza Khamis, Mheshimiwa Hamza Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wataalam kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano wao wakati wa kuwasilisha maelezo ya Muswada huu na kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwashukuru kwa dhati wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao ya kitaalam katika Muswada huu ambayo kwa kiasi kikubwa yamezingatiwa na Kamati. Naomba kutambua mchango wa wadau kama ifuatavyo:-

(i) Chama cha Washauri Elekezi wa Mazingira Tanzania;
(ii) Akili *Platform* Tanzania;
(iii) *Living way Limited* Dar es Salaam;
(iv) Tanzania *Traditional Energy and Development Organization*;
(v) Tanzania *Recyclers Association;*
(vi) Mazingira ni Uhai;
(vii) Mufindi *Environmental Trust;*
(viii) *Human Dignity and Environmental Care Foundation;*
(ix) Balozi wa Mazingira;
(x) Chuo cha Mwalimu Nyerere; na
(xi) Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kwa weledi na umahiri wao waliouonesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa maoni, ushauri na mapendekezo ya kuuboresha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, Kamati inamshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Pia, ninakushukuru na wewe ambaye unatuongozea Kikao chetu leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI, NA MAZINGIRA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA WA MWAKA 2024 (THE ENVIRONMENTAL MANAGEMENT (AMENDMENT) BILL, 2024) – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2024(*The Environmental Management (Amendment) Bill, 2024*).

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, iliupokea Muswada huu Mwezi Novemba, 2024 baada ya kusomwa Bungeni mara ya kwanza tarehe 8 Novemba, 2024 katika Mkutano wa 17, Kikao cha Tisa cha Bunge na wewe kuuelekeza kwenye Kamati yetu ili tuufanyie kazi.

## 2.0 JINSI KAMATI ILIVYOUFANYIA KAZI

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata muda wa kuupitia Muswada na kupata ufafanuzi kutoka kwa Sekretarieti kwa maeneo yaliyohitaji utaalamu wa Sheria. Baada ya kuupitia Kamati ilimwalika Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ili

aipitishe Kamati kwenye madhumuni na sababu za Muswada aliowasilisha. Waziri alifafanua Kifungu kwa Kifungu akieleza sababu na Madhumuni ya kila Ibara iliyomo katika Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 97 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, Kamati ilitoa matangazo katika vyombo vya habari na kuwaalika Wadau mbalimbali ili waweze kufika mbele ya Kamati na kutoa Maoni yao kuhusu Muswada huu. Mwaliko uliotolewa ulikusudia kuwapa wadau fursa ya kutoa maoni yao kuhusu Sheria ya marekebisho ya Sheria inayokusudiwa kutungwa na hatimaye kuisaidia Kamati kupata ufahamu wa namna wadau wanavyouchukulia Muswada huo. Wadau 21 walifika mbele ya Kamati tarehe 15 Januari, 2025 na kutoa maoni yao.

## 3.0 MALENGO NA MADHUMUNI YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu unapendekeza kurekebisha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 ili kukabiliana na baadhi ya changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada uliowasilishwa na Serikali una Ibara 28 zenye marekebisho madogo. Aidha, Serikali iliwasilisha jedwali la marekebisho katika maeneo mbalimbali ya Muswada. Baadhi ya mambo yaliyobainishwa katika Muswada na jedwali la marekebisho ni kama ifuatavyo:-

a) Kuzitaka Wizara za Kisekta kuwa na ama Sehemu au Kitengo kinachohusika na Usimamizi wa Mazingira;

b) Kuboresha tafsiri za maneno "*solid waste*" na kuongeza tafsiri ya maneno "*water sources, climate change, climate change management, climate system, climate change vulnerability assessment, emissions, energy transition, greenhouse gases* na *vulnerability*";

c) Kumwongezea Waziri Mamlaka ya kushughulikia masuala ya mabadiliko ya tabianchi, kudhibiti gesijoto, kushirikisha

wadau katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kumwezesha kutunga Kanuni juu ya masuala hayo;

d) Kubadili sifa za Kitaaluma za Afisa Usimamizi wa Mazingira ngazi ya Halmashauri na kumwongezea majukumu na utaratibu wa kutoa taarifa za utekelezaji wa Sheria;

e) Kuweka muda mahsusi wa miaka mitano (5) kwa kila Halmashauri kuwasilisha kwa Waziri Mpango Mkakati wa mazingira.

f) Kumtaka Waziri anayehusika na Mazingira kushauriana na Mawaziri wa Kisekta kabla ya kutangaza Kanuni au maeneo yanayolindwa katika Gazeti la Serikali;

g) Kuwapa Halmashauri jukumu la usimamizi wa mazingira katika Bahari;

h) Kumtoa Afisa Maji na kumweka Mkurugenzi wa Bonde kwa jukumu la kujiridhisha na hatua za tahadhali zilizo chukuliwa na mmiliki wa kibali cha kutumia maji;

i) Kuiongezea majukumu Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Mazingira ili iweze kutoa Ushauri kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi;

j) Kulinda udongo;

k) Kuliweka suala la utangazaji wa viwango chini ya Waziri husika;

l) Kurekebisha majina ya Taasisi na kuongeza nyingine ambazo zinahusika kimazingira;

m) Kulipa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) uwezo wa kupokea maombi ya marejeo juu ya amri zake ilizotoa na Waziri kuwa na Mamlaka ya kufanya mapitio au kusikiliza rufaa;

n) Kumtaka Waziri anayehusika na Mazingira kwa kushirikiana na Waziri anayehusika na masuala ya Fedha au Wizara ya Kisekta inayoguswa na jambo husika kwenye masuala yanayohusu uwezeshaji wa kifedha ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

o) Kumtaka Waziri anayehusika na Mazingira kutoa ushauri kwa Mamlaka inayohusika na Mipango ya Kitaifa kabla ya kuidhinishwa kwake ili kuhakikisha masuala ya Mazingira na Mabadiliko ya tabianchi yanazingatiwa kwa ukamilifu; na

p) Kuanzishwa kwa Kituo cha Uratibu wa Biashara ya Kaboni

## 4.0 UCHAMBUZI WA JUMLA WA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada wa Sheria ya Marekebisho madogo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Aidha, Kamati ilikuwa na matarajio ya kuletwa Bungeni Muswada uliosheheni marekebisho makubwa ambayo Serikali na Kamati imekubaliana kwa nyakati tofauti. Baada ya kupitia Maazimio mbalimbali ya Bunge na kufanya uchambuzi wa Muswada huu, Kamati ilibaini kuwa bado yapo maeneo muhimu ambayo yalihitaji kufanyiwa marekebisho na hayajahusishwa katika Muswada huu. Baadhi ya maeneo hayo ni:-

a) Kulifanya Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuwa Mamlaka;na

b) Kuzingatia masuala ya Uchumi wa Bluu katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, masuala hayo na mengine mengi ambayo hayakuzingatiwa katika Muswada huu yalijadiliwa katika kikao baina ya Kamati na Wizara ili kuona uwezekano wa kuyaingiza katika Muswada huu. Kutokana na ukubwa wa marekebisho ambayo Kamati ilihitaji, ilionekana ni vizuri marekebisho hayo

ikufanyika kwa Miswada mipya ambayo itashirikisha wadau katika ngazi ya Serikali na kutangazwa katika Gazeti la Serikali ili Kamati itakapoishughulikia iweze kupata idadi kubwa ya wadau wa kutoa maoni katika Miswada hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifahamishwa kuwa Serikali ilihitaji muda zaidi ili kuandaa marekebisho makubwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira yatakayojumuisha maeneo muhimu. Kutokana na ahadi hiyo, Kamati iliendelea kufanyia kazi Muswada huu wenye marekebisho machache.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kamati inaushauri kwenye ibara 8 ambazo ni Ibara ya 4, 5,21,22,23,24, 25 pamoja na Ibara ya 29D iliyowasilishwa katika jedwali la marekebisho. Maoni ya Kamati kwa kila Ibara ni kama ifuatavyo;

### 5.1 Ibara ya 4 inayorekebisha Kifungu cha 13(1)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa neno tabianchi limeongezwa katika sehemu moja tu ya Kifungu cha 13(1) na hivyo kutofikia lengo lililokusudiwa. Aidha, Kamati iliona umuhimu wa Waziri kupewa pia Mamlaka ya kushughulikia mabadiliko ya tabianchi kwa kujumuisha katika Sera masuala ya upunguzaji wa gesijoto na mikakati ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Hivyo Kamati ilipendekeza Kifungu hiki kisomeke kama ifuatavyo: -

13.-(1) The Minister shall be overall responsible for matters relating to the environment, climate change, and shall, in that respect, be responsible for the articulation of Policy Guidelines necessary for the promotion, protection, sustainable management of the environment, **and the integration of climate change mitigation and adaptation strategies into Policy.** Serikali imekubaliana na mapendekezo ya Kamati na yamezingatiwa katika Jedwali la Marekebisho ya Muswada.

### 5.2 *Ibara ya 5 inayorekebisha Kifungu cha 36*

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 5 ya Muswada ilipendekeza kurekebisha Kifungu cha 36(2) ili kuondoa sifa ya Diploma kwa Afisa Usimamizi wa Mazingira na kubakisha sifa ya Shahada pekee. Kamati ilishauri kuwa Ibara hiyo kurekebishwa ili sifa za kielimu zisitajwe katika Sheria na kubakia katika Muundo wa Utumishi. Marekebisho yaliyopendekezwa yalikusudia Kifungu cha 36(2) kisomeke kama ifuatavyo:-

"(2) A person designated or appointed by the City, Municipal, District or Town Environment Management Officer shall possess **requisite academic qualifications** and has competence in environmental management".

Serikali imekubaliana na ushauri wa Kamati na kuzingatia katika Jedwali la Marekebisho ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilishauri kufutwa kwa Ibara ya 5(b) ya Muswada iliyopendekeza kurekebisha Kifungu cha 36(3) (h) kilichohusu uwasilishaji wa Taarifa ya Utekelezaji wa Sheria unaofanywa na Afisa Usimamizi wa Mazingira wa Halmashauri. Kamati iliona marekebisho haya yafanyiwe kazi katika marekebisho makubwa ya Kimuundo na Kimfumo yanayotarajiwa kuwasilishwa na Serikali. Ushauri wa Kamati umeridhiwa na kuzingatiwa na Serikali katika jedwali la marekebisho ya Muswada.

### 5.3 Ibara za 21,22,23,24 na 25

**Mheshimiwa Spika,** Ibara za **21, 22, 23, 24 na 25** zilipendekeza kurekebisha Vifungu vya **195, 196,197,198** na **199.** Lengo la marekebisho hayo ni kutoa nafasi kwa NEMC kupokea maombi na kufanya marejeo ya amri ilizotoa na kumruhusu mtu asiyeridhishwa na uamuzi wa Baraza hilo katika Marejeo kuomba mapitio au rufaa kwa Waziri ndani ya siku thelathini. Kamati ilishauri Ibara hizo zifutwe kwa kuwa Serikali imeahidi kuleta marekebisho makubwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191. Marekebisho hayo pamoja na mambo mengine yatahusiana

na masuala ya utoaji haki. Serikali imekubaliana na Ushauri wa Kamati na Ibara hizo kufutwa kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Muswada.

**5.4 Ushauri kuhusu mambo yaliyoongezwa kwenye jedwali la marekebisho**

**Mheshimiwa Spika**, katika eneo hili, naomba kutanguliza maelezo yafuatayo:-

1. Tangu awali Kamati ilipopitia jumla ya Ibara 28 za Muswada, ilibaini kusahaulika kwa jambo muhimu miongoni mwa mengine lililohusu usimamizi wa Biashara ya Kaboni.

2. Utaratibu wa Kamati kushughulikia Miswada ya Sheria umewekewa masharti yanayobainisha pamoja na mambo mengine wigo wa jukumu na Madaraka ya Kamati. Kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari,2023, uwezo wa Kamati kufanya marekebisho kwenye Muswada ni wa kumshauri mtoa hoja. Aidha, kwa desturi za Kibunge ushauri huo unagusa yale tu yaliyomo kwenye Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikuwa na maoni kwamba si jambo jema kukosa masharti ya Kisheria yanayohusu usimamizi mzuri wa Biashara ya Kaboni. Kwa msingi huo, ili kuhakikisha kuwa manufaa ya kiuchumi yanapatikana huku mazingira yakihifadhiwa kwa kizazi cha sasa na kijacho, marekebisho ya Sheria yanayoweka masharti ya usimamizi wa Biashara ya Kaboni ni jambo Muhimu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inamshukuru mtoa hoja ambaye alizingatia maoni hayo na kuongeza kwenye jedwali la marekebisho mapendekezo yanayogusa usimamizi wa biashara hiyo. Hata hivyo, katika Ibara ya 29 D (1) ya jedwali ilipendekeza kuwepo kwa Mkurugenzi na Bodi ya Wakurugenzi wa Kituo cha Uratibu wa Biashara ya Kaboni. Aidha, muda wa ukomo kwa Wajumbe wa Bodi haukutajwa katika marekebisho hayo. Kwa muktadha huo, Kamati ilishauri kurekebishwa kwa Ibara hiyo ili kuonesha namna ambavyo Mkurugenzi wa Kituo hicho

atapatikana pamoja na ukomo wa Wajumbe wa Bodi. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na kuuzingatia kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia uchambuzi wa Kamati, madhumuni na sababu za kutungwa kwa Sheria hii, Kamati imeridhishwa na marekebisho madogo yaliyofanywa katika Muswada huu. Hata hivyo, ili kukidhi matarajio ya Bunge, Wananchi na maudhui ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021, Kamati inaona kuwa ipo haja kwa Serikali kuleta Miswada ya Sheria mipya itakayowezesha kutungwa kwa Sheria ya kulifanya Baraza la Taifa la Mazingira kuwa Mamlaka pamoja na Sheria ya masuala ya Uchumi wa buluu. Ni Matarajio ya Kamati kwamba Serikali italeta Miswada hiyo mapema wakati wa Mkutano wa 19 wa Bunge kama ilivyoahidi.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nikushukuru sana wewe kwa kutoa kibali ili Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira iweze kuufanyia kazi Muswada huu na kuipa fursa ya kuwasilisha maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumpongeza Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yusuf Masauni (Mb)Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Naibu Waziri Mhe. Khamis Hamza Khamis (Mb), Mhe. Hamza Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wataalamu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano wao wakati wa kuwasilisha maelezo ya Muswada huu na kutolea ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru kwa dhati Wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao ya kitaalamu katika Muswada huu ambayo kwa kiasi kikubwa yamezingatiwa na Kamati. Naomba kutambua mchango wa Wadau wafuatao: -

- Chama cha Washauri Elekezi wa Mazingira Tanzania (TEEA);

- Akili Platform Tanzania;
- Livingway (URT) Limited DSM;
- Tanzania Traditional Energy and Development Organization (TATEDO);
- Tanzania Recyclers Association (TARA);
- Mazingira ni Uhai;
- Mufindi Environmental Trust (MUET);
- Human Dignity and Environmental Care Foundation (HUDEFO);
- Balozi wa Mazingira;
- Chuo cha Mwalimu Nyerere; na
- Chuo Kikuu cha Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kwa weledi na umahiri wao waliouonesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa maoni, ushauri na mapendekezo ya kuuboresha Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa heshima na taadhima, **naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD).**

1. Mhe. Jackson G. Kiswaga, Mb. **Mwenyekiti**
2. Mhe. Anna R. Lupembe, Mb. **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Balozi Dkt. Bashiru A. Kakurwa Mb. Mjumbe
4. Mhe. Prof. Shukrani E. Manya, Mb. Mjumbe
5. Mhe. Asya Sharif Omar, Mb. Mjumbe
6. Mhe. Mhandisi Stella M. Manyanya, Mb. Mjumbe
7. Mhe. Charles John Mwijage, Mb. Mjumbe
8. Mhe. Soud Mohammed Jumah, Mb. Mjumbe
9. Mhe. Juma Usonge Hamad, Mb. Mjumbe
10. Mhe. Ritta Kabati Enespher, Mb. Mjumbe
11. Mhe. Haji Makame Mlenge, Mb. Mjumbe
12. Mhe. Kavejuru Eliadory Felix, Mb. Mjumbe
13. Mhe. Asya Mwadini Mohammed, Mb. Mjumbe
14. Mhe. Regina Ndege Qwaray, Mb. Mjumbe
15. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb. Mjumbe
16. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb. Mjumbe
17. Mhe. Deo Kasenyanda Sanga, Mb. Mjumbe

| | | |
|---|---|---|
| 18. Mhe. | Keneth Nollo Mb. | Mjumbe |
| 19. Mhe. | Kasalali E. Mageni Mb. | Mjumbe |
| 20. Mhe. | Suleiman Omar Mohamed, Mb. | Mjumbe |
| 21. Mhe. | Robert C. Maboto, Mb. | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, Kamati inamshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukuu yake ipasavyo.

**Mheshimwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jackson G. Kiswaga (Mb),
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda kwenye uchangiaji, nina majina hapa. Nimwite sasa Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga atakuwa mchangiaji wetu wa kwanza, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, ajiandae.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi leo kuwa mchangiaji wa kwanza. Pia, niishukuru sana Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa kuona umuhimu wa kuleta marekebisho haya ya sheria ili kuweza kuipatia nguvu sheria ya kusimamia masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee sana nimshukuru Mheshimiwa Rais ambaye ndiye mwanamazingira namba moja

wa Taifa hili, ni mapenzi yake mema kuona kwamba tunaendelea kufanya maboresho ya sheria mbalimbali ili ziweze kutusaidia kusimamia mazingira ambayo yanaendelea kuharibika sana na madhara yake yamekuwa ni dhahiri mno kwa Taifa letu pia kwa dunia kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea marekebisho ya Muswada kwa kadri Mheshimiwa Spika alivyoelekeza kutokana na kile Kifungu cha Kanuni za Bunge, Kanuni ya 97 ambayo inamataka Spika baada ya kupata Muswada aielekeze Kamati husika iweze kuupokea na kuujadili mapema kwa kadri iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilifanya hivyo, imekuwa na muda mzuri wa kujadili Muswada huo ambao ulikuwa na Ibara 28 na kuona kweli ipo tija ya kufanya mabadiliko kadhaa ambayo yameonekana kwenye Miswada hiyo ili masuala yanayohusu mabadiliko ya tabianchi na mazingira kwa ujumla yaweze kusimamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, niseme kwamba ninaunga mkono hoja. Nianze kwa kuunga mkono hoja na ningeweza kusema niishie hapa baada ya kuuunga mkono hoja, maana taarifa ya Kamati imejieleza vizuri sana maeneo ambayo ushauri Kamati imeelekeza. Hata hivyo, kwa msisisto ninaweza kugusia maeneo machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ambalo ninapenda kuligusia ni lile ambalo linamwongezea Waziri wa Mazingira nguvu ya kuweza kusimamia masuala yanayohusu mazingira hasa kwa kujadiliana na Waziri wa Fedha kuona ni maeneo gani au ni vyanzo gani tunaweza tukatafuta vya fedha ambavyo vitasaidia kusimamia masuala yanayohusiana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kwa Waziri wetu kuwa na hayo mamlaka na nguvu, pia kuwa na fedha ambayo inatengwa mahsusi kwa ajili ya masuala yanayohusu mabadiliko ya tabianchi. Ukiangalia kwenye masuala ambayo yanayohusu

mabadiliko ya tabianchi yamekuwa yakitengewa fedha kidogo sana. Sasa, kama tukiweka nguvu kwenye sheria maana yake itamtaka Waziri wa Fedha kutekeleza takwa hilo ambalo linakuwa ni la kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, uanzishaji wa Kamati ya Kitaifa inayohusu mabadiliko ya tabianchi ambayo itaongozwa na Katibu anayehusiana na masuala ya mazingira ni jambo muhimu. Kamati hii ambayo itahusisha wadau ambao wana unasaba na masuala yanayohusu mazingira itaweza kuwa na nguvu ya kuandaa mikakati na usimamizi wa mipango inayohusiana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Kamati ya Kitaifa itakuwa na uwezo wa kufuatilia kuona ni wapi tumefikia katika kutekeleza ile mikakati na mipango inayohusu mabadiliko ya tabianchi. Kwa hiyo, ni jambo muhimu ambalo sisi tumeona kwa kweli linatakiwa lipite ili masuala ya mabadiliko ya tabianchi yaweze kusimamiwa kwa mapana yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Kamati tumelielezea kwa mapana na tumeliunga mkono kama taarifa ya Kamati ilivyoonesha ni suala la kuzipa mamlaka, hizi Serikali za Mitaa kuandaa mpango kazi unaohusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Mpango kazi huo ambao utakuwa unaandaliwa kila baada ya miaka mitano pia utaonesha ni maeneo yapi ambayo mpango huo unaweza kupatiwa fedha uwekewe bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya kufanya hivyo itasaidia pia hawa wanaosimamia masuala ya mazingira kwenye Serikali za mitaa. Pia, kwenye sekta nyingine ambazo kama tulivyoeleza kwenye taarifa kwamba, sekta nyingine pia lazima ziwe na kitengo ambacho kinahusika na masuala ya mabadiliko ya tabianchi na kiwekewe fedha. Kikishawekewa fedha itakuwa ni rahisi kuweza kutekekeleza kwa ukamilifu masuala ya mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine Kamati imeipongeza Serikali, ni suala la kukitambua Kituo cha Usimamizi wa Masuala ya

Kaboni kisheria. Kwanza, tuipongeze Serikali ilianzisha kituo hiki mwaka 2015 na imekuwa ni nchi ya kwanza kutengeneza kanuni zinazosimamia masuala ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa tunavyofanya kazi na vyombo vingine vya kimataifa, kwa kuwa kituo hiki kilikuwa hakitambuliki kisheria unakuta kwamba nchi imekuwa ikikosa fursa za kuweza kunufaika na biashara zinazohusiana na masuala ya kaboni. Pia, kuweza kutoa taarifa zinazohusiana na masuala ya gesijoto duniani na usimamizi wake. Kwa hiyo, hilo pia tunaipongeza Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ushirikishwaji wa sekta binafsi…

*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzai)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ninaomba uhitimishe hoja yako.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mwisho ninavyoenda kuhitimisha hoja ni lile ambalo Kamati imesisitiza kwamba ni matamanio ya Kamati kuona kwamba tunampatia Mheshimiwa Rais chombo chenye nguvu na mamlaka ya kusimamia masuala ya mabadiliko ya tabianchi na hii ni *NEMC* kuifanya iwe mamlaka. Suala la *blue economy* kuwa mamlaka itasaidia nchi kuweza kusimamia masuala ya mazingira kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jackson Kiswaga. Nimwite sasa Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, halafu Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah atafuatiwa na Mheshimiwa Kavejuru Felix ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia hii nafasi. Nami niungane na Wajumbe wa Kamati yangu kumpongeza sana Mheshimiwa

Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano pamoja na Naibu wake, hali kadhalika Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na watenda kazi wote kwa ujumla wake, kwa jitihada kubwa ambayo wameifanya kuhakikisha kwamba Muswada huu unaboreshwa na kuwezesha kutimiza malengo yanayokusudiwa katika kusimamia vizuri suala la mazingira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefurahishwa pia na hali ya usikivu wao kwa yale tuliyowashauri na hasa sasa katika kuhusisha masuala mengine yanayohusiana na hewa ukaa pamoja na uchumi wa buluu. Pia, kama walivyosema wenzangu masuala ya kuhitaji kuwa na chombo madhubuti cha kusimamia masuala ya mazingira *(NEMC)* wakati huo labda pengine itakuwa *NEMA* au vyovyote itakavyoitwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu leo hasa ni katika kufafanua baadhi ya maeneo. Kwa mfano, eneo ninalotaka kulizungumzia ni suala la umuhimu wa kuwa na watu wabobezi wanaotambulika kwa ajili ya usimamizi wa mazingira. Kwa sasa, hatuna *professional board* ambayo inasimamia eneo hili. Vilevile, tunataka kuondoa changamoto zisizo za lazima. Kwa mfano, kuna baadhi ya wataalam ambao wapo katika ajira hawaruhusiwi kushiriki katika utafiti wanapokuwa katika tafiti zinazoendelea na zinazotolewa kuleta maendeleo au kazi mbalimbali katika nchi. Kwa hiyo, kuna maeneo ambayo bado tunahitaji yafanyiwe kazi japo hayapo katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu suala la kuwa na Maofisa Mazingira Maalum kwenye ofisi zetu za TAMISEMI. Hilo ni suala muhimu sana, kwa sababu utekelezaji mkuu wa uendelezaji wa mazingira yetu au kufanya mazingira yawe hilimivu na endelevu, kunafanyika kupitia halmashauri zetu. Sasa tunapokuwa hatuna wataalam mahsusi katika maeneo hayo changamoto inaendelea kuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta kwamba inakuwa labda pengine kuna watu wanachukuliwa, kwamba anasimamia mambo ya maliasili wakati huo huo huyo huyo ndiye wa mazingira. Kwa hiyo, tunatamani kuona kabisa kwamba kitengo

hicho kinaimarishwa na kinakuwa imara, kwa sababu suala la mazingira ni tishio kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema pia kwamba wawezeshwe, wapate fedha za kutosha ili waweze kusimamia ipasavyo. Fedha hizo haziwezi kutegemea kwa mjomba tu, ni lazima sisi wenyewe tuziweke kwenye bajeti zetu ili kuona kwamba kweli jambo hili tunalipa uzito wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo ilizungumzwa kwamba maafisa hao wawe na cheti cha *degree* na kuendelea. Sisi Kamati tumeona kwamba si lazima kuweka cheti katika sheria, kwa sababu tuna muundo wa kiutumishi ambao upo, unaoweza kueleza kwamba kwa nafasi hii mtu awe na sifa zipi. Kwa hiyo, tuliwashauri wasiweke hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, si tu suala la kuwa na cheti; kwa sababu tumeshashuhudia sasa hivi watu wanamaliza vyuo, wana vyeti wanazunguka navyo, lakini wanashindwa hata kujaribu kufanya jambo linalohusiana na hilo suala alilosomea. Tunasema iwe ni mtu mwenye cheti kikubwa kinachotambulika, kama ni cheti cha kiutaalam katika masuala ya mazingira, lakini pia awe amebobea, ana uzoefu wa kutosha; huyo ndiye tunayemhitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo tulisema kwamba hakuna haja ya kuweka kwenye sheria, kwa sababu utaweka sheria kwa ajili ya huyo afisa mazingira, vipi kuhusu Mkurugenzi? Vipi kuhusu mwingine anayesaidia? Kwa hiyo, hivyo vibaki kwenye muundo wa kiutumishi, lakini inapokuja katika suala la sheria itamke tu kwamba tunahitaji mtu mwenye sifa za kutosha, mwenye ubobevu na uwezo mkubwa katika kushughulikia masuala hayo. Tunashukuru sana kwamba Wizara ilituelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hili suala la biashara ya hewa ukaa. Ukiangalia nchi yetu, pamoja na jitihada tunazozungumza juu ya uharibifu wa mazingira, lakini kwa kweli Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo kwa kiwango kikubwa

tumehifadhi mazingira yetu vizuri. Isipokuwa tu kwenye mipangilio ya kutenga maeneo, kwamba sasa eneo hili tunalihifadhi kwa ajili gani, eneo hili la fukwe ni kwa ajili gani na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la biashara ya hewa ukaa limekuwa ni suala geni kidogo kwetu. Wengine wanalijua na wengine hawalijui. Ukiambiwa leo akina nani wanahusika na hewa ya ukaa utakuta tu wafanyabiashara wanasema mimi ninahusika. Inafanyikafanyika vipi, haijulikani sawasawa. Kwa hiyo, hali hiyo inafanya wengine wanufaike na wengine wasinufaike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Kamati yetu imesisitiza kuweka chombo maalum chenye mamlaka na chenye nguvu kisheria, kama kile kituo cha biashara ya hewa ukaa pale Morogoro. Chombo hicho kipate meno ya kutosha na kiweke mwongozo ulio wazi kabisa ili mtu yeyote au kikundi chochote cha watu watakaoamua kujihusisha na biashara hii waweze kufuata zile taratibu kwa wazi na hivyo nchi kuweza kunufaika kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, baada ya mchango huu ninalishukuru Bunge hili kwa sababu limekuwa likituunga mkono Kamati yetu. Pia ninazidi kukushukuru wewe mwenyewe Mheshimiwa Mwenyekiti na uongozi wa Mheshimiwa Spika, pamoja na timu yake yote kwa ujumla, kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakiisaidia Kamati yetu ili kuleta matokeo makubwa zaidi kwa ajili ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana Mheshimiwa Rais wetu na Makamu wa Rais, ambaye suala hili liko katika ofisi yake. Ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Eng*. Stella Manyanya. Sasa nimwite Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, atafuatia Mheshimiwa Kavejuru Felix na Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ninachukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mheshimiwa Waziri na timu yake. Wamefanya kazi nzuri ya kutuletea huu Muswada na uwasilishaji wake *Masha Allah* ulikuwa mzuri. Halikadhalika, Katibu Mkuu na wasaidizi wake wamefanya kazi nzuri kuweza kuutengeneza Muswada huu; kuurekebisha na kukaa na Kamati, kwenda na kurudi na hatimaye wamekuja na Muswada ambao sasa hivi umekidhi matakwa ya Kamati na matakwa ya Serikali kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Rais Mama Samia, ambaye ni mhifadhi na mwanamazingira namba moja. Tumeona jitihada zake; amehudhuria, ninafikiri hii *cop* ya mara hii iliyofanyika imekuwa ni *cop* yake ya tano kuhudhuria mwenyewe *in person*. Ninafikiri hatujawahi kuona huko nyuma kiongozi wa nchi kuhudhuria mwenyewe mikutano kama hii. Tija yake tunaiona kwa sababu fedha nyingi zimeweza kutiririka, hasa katika masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Ninafikiria na hata haya mabadiliko ambayo tunayafanya yanaelekea huko huko kwenda kuongeza wigo wa kuweza kupata fedha zaidi za kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Muswada huu uliposomwa kwa mara ya kwanza hapa Bungeni sisi Kamati ya Maji na Mazingira na Bunge lako kwa ujumla liliingia hamasa kubwa sana, na nikajua sasa hivi ule msamiati ambao kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo tumekuwa tukiazimia kwamba tuone mabadiliko makubwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira yanafanyika, ili twende tukatatue changamoto za kimazingira ambazo zinaongezeka siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tumekwenda kwenye Kamati kule na tukasomewa ule Muswada ulivyo kiasi fulani

tulinyong'onyea. Tulinyong'onyea kwa sababu tuliona yale mambo mengi makubwa ambayo tulikuwa tunayahitaji kuyaona na tumeazimia hapa Bungeni yalikuwa yanakosekana, ikiwemo suala la hiki kituo cha hewa ukaa; halikuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ule wigo wa mabadiliko ya tabianchi; tulikuwa tunataka sheria ambayo itasheheni maeneo na usimamizi wa wadau, halikadhalika na ushiriki wa watu wengi zaidi katika usimamizi wa mabadiliko ya tabianchi. Pia, ilikuwa ni ibara mbili tu; Ibara ya 12 na Ibara ya 13, Vifungu 75, 75A, ndivyo vilivyokuwa vinaonyesha utaratibu wa mabadiliko ya tabianchi. Maeneo yaliyobakia yote ilikuwa ni mazingira, mazingira, mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, tunashukuru kwamba baada ya kukaa na wenzetu wa Serikali wakatuelewa, kwa kuwaambia kwamba mambo tuliyoyaazimia kuhusiana na Muswada huu mengi hayamo walikwenda wakabadilisha. Hapa ninamshukuru kwa makusudi Mheshimiwa Masauni. Mheshimiwa Masauni ameonesha ukomavu, ameonesha *maturity* ya hali ya juu, kwa sababu baada ya kukubaliana na Kamati alikwenda akaunda timu yake ikaenda ikajifungia Morogoro na ikaja na mabadiliko mazuri, ikiwemo kuingiza huu utaratibu wa kituo cha hewa ukaa. Hongera sana kwa Mheshimiwa Masauni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika suala la *scope* ya mabadiliko ya tabianchi; sasa hivi tukiangalia Muswada wetu umesheheni mambo mengi ya mabadiliko ya tabianchi, ikiwa ni pamoja na Kamati ile ya Ushauri na Usimamizi, mambo ya hewa joto, ya usimamizi wa gesi joto, halikadhalika na *scope* ya wadau nayo imeongezeka vilevile. Kwa hiyo, hongereni sana Serikali. Kwa kweli mmeheshimiwa mabadiliko ya tabianchi, kwa sababu sasa hivi maeneo mengi yameweza kukidhi haja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni suala la Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ninaomba uhitimishe mchangiaji.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi limeguswa humu kidogo, lakini bado halijawa *qualified* kuingiza mabadiliko ya tabianchi bila ya Mfuko huu. Kwa hiyo ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, wakati atakapotayarisha kanuni akatayarishe kanuni ambayo itasaidia huu Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi ili nao uwe sehemu ya Mfuko wa Mazingira ambao sasa hivi umo kwenye sheria yetu hii. Kwa sababu wenzetu Umoja wa Mataifa ukiangalia kuna *GEF (Global Environmental Facility),* yaani Mifuko ya Mazingira, lakini bado wamekuja na Mifuko ya Mazingira kama vile *Green Climate Fund, Adaptation Fund* na *Lease Development Fund*. Yote hii ni Mifuko ya Mabadiliko ya Tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa tu kwamba Mfuko wetu huu wa Mazingira twende tukaufanyie utaratibu mzuri ili uweze kuingiza pia masuala yanayohusu mabadailiko ya tabianchi, kama ambavyo sheria imezungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimwite sasa Mheshimiwa Kavejuru Felix, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya na Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi ajiandae na wachangiaji mtachangia kwa dakika tano.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia hoja hii ya Muswada unaopendekeza marekebisho madogo kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191. Ninaomba nitoe pongezi kwa Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na watumishi wote kwa kazi kubwa na njema ambayo wameifanya. Wamefanya marekebisho ambayo ni ya msingi ambayo yatawezesha kutatua changamoto mbalimbali ambazo zilikuwa zinajitokeza katika

utekelezaji wa Sheria hii ya Mazingira. Hongera sana kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa dakika tano ni muda mfupi, kwanza ninapongeza kwa uanzishwaji wa kituo cha kuratibu biashara ya kaboni. Biashara hii imekuwa ikiendeshwa ikiwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, lakini ilikuwa haitambuliwi na sheria. Kwa sababu ilikuwa haitambuliwi na sheria, kituo hiki kilishindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Si majukumu yake tu bali pia kilikosa sifa za kuingia mikataba ya kitaifa na kimataifa. Matokeo yake kikakosa fedha ambazo zinatolewa na taasisi za kimataifa, hususan kwenye mabadiliko ya tabianchi. Hongereni sana kwa kuanzisha kituo hiki, ambacho kitatumika kwa ajili ya kuratibu shughuli za biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tutafaidika, halmashauri ambazo zina hifadhi ya misitu zitafaidika na Serikali itafaidika. Kwa kuwa tumejaaliwa na maliasili ya misitu, tutaongeza pato, tena tukiwa na kituo ambacho kinatambulika kisheria. Hongera sana kwa Waziri Mheshimiwa Masauni, hongera kwa Naibu na hongera kwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hii kazi kubwa ambayo imefanywa, ninaunga mkono hoja kwa ibara zote na vifungu vyote ambavyo vimefanyiwa marekebisho. Hata hivyo, ili kukidhi matarajio ya wananchi kwa lengo la kutatua changamoto za mazingira zilizopo kitaifa na kimataifa, ni wakati sasa ambapo ipo haja kwa Serikali kuleta Muswada wa sheria mpya zitakazosimamia masuala ya uchumi wa *blue* na kulifanya Baraza la Mazingira kuwa mamlaka kamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo Baraza hili la Mazingira likibadilishwa na kuwa mamlaka kamili, basi mamlaka hii itakuwa ni *regulator* wa taasisi zote ambazo zinajihusisha na shughuli za kimazingira. Kwa sababu Mungu ametuzawadia sisi maliasili nyingi, tutakapokuwa na chombo hiki ambacho kitakuwa madhubuti, basi kitaweza kutatua changamoto zote zinazohusiana na mazingira kitaifa na kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ninampongeza Mheshimiwa Rais, ambaye ni mhifadhi namba moja wa mazingira, na ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Philop Isdor Mpango, Makamu wa Rais, kwa kusimamia Wizara hii ya Mazingira kwa mafanikio makubwa sana na kampeni nyingi ambazo amezianzisha ambazo zinasoma na mti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Wanakamati wenzangu kwa kazi kubwa ambayo tumeifanya na sasa leo tumefikia hatua hii...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Felix. Nimwite sasa Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya. *(Makofi)*

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2024. Ninatangulia kusema kwamba ninaunga mkono hoja zote za Kamati yetu ya Maji na Mazingira, kama zilivyowasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaomba nilipongeze Bunge lako; kwa kutambua umuhimu wa mazingira kwamba ni suala mtambuka lilikubali kuiweka Kamati ya Maji na Mazingira mahsusi kwa ajili ya kulishughulikia suala hili kama Kamati ya Kudumu ya Bunge. Ni kutokana na kuwepo kwa Kamati hii mambo haya makubwa yanayosimamia mazingira, na matarajio makubwa ambayo kimsingi Kamati imekubaliana na Wizara kwamba yatafanyika; tunaamini kwamba Wizara kutokea hapa, baada ya kuleta mabadiliko madogo, sasa wataleta yale makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwamba atalipa msukumo jambo hilo na matarajio ya Kamati ni kwamba, kabla Bunge la Kumi na Mbili halijafikia ukomo, yale mabadiliko makubwa yataweza kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Kamati siku zote imekuwa ni kuona kwamba tutakapokuwa na mamlaka madhubuti, mamlaka imara inayosimamia mazingira, basi itakuwa ni kulibadilisha Baraza kuwa mamlaka kamili. Ni kwa sababu gani tunafikiria hivyo? Bado kuna mambo ambayo yanalegalega, ambayo tunaamini kwamba iwapo Baraza litakuwa mamlaka yanaweza kusimamiwa vizuri. Kwa ajili ya muda, ninaomba niyaorodheshe kwa ufupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna katazo la mifuko ya plastiki, lakini plastiki bado zinaendelea kuonekana. Nenda sokoni utapewa plastiki kama kifungashio. Bado kuna utupaji taka na chupa katika fukwe zetu ambazo haziwezi kurejelezwa. Bado tuna uchimbaji wa madini unaoacha mashimo na ku-*expose* miamba ya sumu na bado kuna matumizi ya zebaki katika uchimbaji madini. Pia bado kuna kelele nyingi sana wakati wa usiku Watanzania wanapokuwa wanahitaji kulala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna ujenzi katika vilima na ujenzi katika vyanzo vya maji unaoendelea hapa nchini. Bado kuna makazi mengi, sasa hivi tunashuhudia Tanzania ikiwa na miji midogo midogo inayokua, lakini pasipo kutengewa maeneo ya dampo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, bado Watanzania kama jamii tunaendelea kuchanganya taka zetu katika miji yetu na hata tunapopeleka dampo ni taka ambazo haziwezi kutenganishwa. Mambo hayo ni mengi, ningeweza kuwa na orodha ndefu, lakini muda ni mfupi. Mambo kama haya na mengine kadha wa kadha ndiyo yanayoipelekea Kamati yetu ya Maji na Mazingira kutamani Baraza liweze kuwa Mamlaka Madhubuti ya Kusimamia Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada uliowekwa mezani Serikali imezitaka Wizara za kisekta kuwa na kitengo au sehemu inayohusika na usimamizi wa mazingira kila mahali. Jambo hili ni la msingi. Tunatambua kwamba wizara zimefanya hivyo, lakini zile zingine ambazo hazijawa na sehemu au kitengo mahsusi cha kusimamia mazingira ni wakati muafaka sheria inapopita wizara zikafanye hivyo, kwa sababu mazingira ni suala mtambuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada uliowekwa mezani, Waziri anayeshughulikia mazingira atakuwa na jopo linalohusika na Mawaziri wa Kisekta. Kabla ya kutangazwa kwamba eneo fulani ni eneo lindwa basi wanakaa pamoja ili waweze kujadili na hivyo tutagundua kwamba jambo hili litaepusha migogoro mingi ambayo wakati mwingine Waziri alikuwa akifanya kazi peke yake na kwa jinsi hiyo pia linaleta utengamano katika utendaji kazi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Hitimisha.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay*, kwa ajili ya muda sasa, tunaipongeza Wizara pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, kwa kutambua na hatimaye kuweka kipengele cha mabadiliko ya tabianchi kama jambo ambalo ni la msingi la kusimamiwa katika nchi yetu. Hii ni kwa sababu ni jambo ambalo liko wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafuriko ambayo hayatarajiwi, ukame unaochukua muda mrefu, maporomoko ya ardhi pamoja na kuendelea kufutika kwa theluji yetu katika Mlima Kilimanjaro ni vielelezo dhahiri vya mabadiliko ya tabianchi na hivyo kuliweka katika Muswada ni jambo ambalo tunaipongeza sana Wizara. Kwa kusema hivyo, naunga mkono hoja na ahsante kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Elisha Manya. Namwita sasa Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi. *(Makofi)*

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi nichangie katika mada hii nikiwa kama mdau wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kwa kuipongeza Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri wetu, na Kamati yetu kwa uchambuzi mzuri na maoni ambayo wameyatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii imekuja miaka 20 ikirekebisha ile ambayo ilikuwepo, kwa hiyo, ni miaka 20 imepita. Niseme ukweli, ni kama imechelewa vile na imekuja wakati muafaka ambao sisi kama Taifa na kwenye dunia hii tuna changamoto nyingi sana za kimazingira. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kuleta marekebisho ya sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda, niseme ukweli kutoka rohoni mwangu kama mdau, kwamba, sheria hii kwa maoni yangu haijajitosheleza kabisa kama walivyosema Kamati. Wamefanya marekebisho madogo. Mwanzo ndio mwendo, kidogo kidogo tutafika, lakini nilitegemea sheria hii ingekuja kwa lengo kubwa la kuhakikisha kwamba tunalinda rasilimali za asili za nchi yetu. Tutengeneze mazingira mazuri ya kuzilinda hizi rasilimali za nchi yetu, kwa mfano, ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi tunajua ni kitu muhimu sana. Ndipo tunapolima, tunapojenga, tunapofugia mifugo yetu na kadhalika. Hata uchimbaji wa madini unafanyika kutoka katika ardhi yetu, lakini sheria hii marekebisho yamelenga udongo. kifungu namba 80 nafikiri kimeongelea udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa upana wake napendekeza tuangalie suala la ardhi na tutoe vifungu vikali vya kisheria vya kuilinda ardhi yetu ili iwe salama isije ikaharibiwa

haribiwa kwa sababu, bila ardhi kama Taifa tutakuwa tumekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni maji na vyanzo vyake. Sawa, tumeigusa kidogo kidogo kwenye Kifungu Na. 57 lakini maji ni uhai. Tunajua vyanzo vya maji, na bila maji hakuna maisha, na hata sisi hapa hatutakuwa na maisha kabisa. Kwa hiyo, naomba tuje na vifungu vikali vya kisheria vya kuhakikisha kwamba maji kama maji tunayalinda ili yawepo na yatatusaidia kwenye kuboresha maisha yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchafuzi wa hali ya hewa, nalo hili ni jambo muhimu sana. Tunajua kuna uchafuzi mkubwa sana wa hali ya hewa ambao unaendelea duniani na hapa tunaona kuna Kamati imeongelea kitu cha *carbon trade*. Ni ukweli kuna uchafuzi ambao wanafanya wenzetu huko. Sasa tuje na sheria kali ambayo itakuwa inatusaidia kuhakikisha kwamba hewa yetu ipo salama tuweze kupumua kwenye hewa ambayo hatutaumia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhifadhi wa bioanuwai, kuna rasilimali zetu za Taifa ambazo zipo, kwa mfano, mimea, miti, wadudu na kadhalika ambavyo vingine vinapatikana tu hapa Tanzania. Sasa naomba sheria hii kwa mtoa hoja waende waje na kifungu kabambe ambacho kitakuwa kinalinda rasilimali zetu hizi za bioanuwai ili ziweze kuwepo leo na kwa ajili ya vizazi vijavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchafuzi wa mazingira nao ni jambo muhimu sana, naomba tuje na vifungu ambavyo vina-*address issue* ya uchafuzi wa mazingira vizuri ili mazingira yetu yawe salama kwa ajili ya maisha ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda, namwomba mtoa hoja akakae na wataalamu wake, wasomi tunao wengi sana katika nchi hii, wa-*address* vile vitu vyote ambavyo Kamati imezungumzia. Kwa mfano, mambo ya uchumi wa buluu, tunajua *potential* ya bahari, maziwa na mito yetu kwenye kuboresha uchumi wa nchi yetu, tuje na vifungu kabambe vya kuhakikisha

kwamba uchumi wa buluu unakuwa *addressed* katika Sheria yetu ya Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NEMC* kuwa mamlaka, nalo ni jambo muhimu na la heri. Suala la *carbon trade,* liwekwe wazi, wale watu wanaokuja kufanya biashara ya *carbon trade* hapa, wana masharti ambayo siyo rafiki kwa watu wetu. Kwa mfano, mkulima mwenye miti yake pale, kama haipo kwenye eneo la hifadhi ambayo haisumbuliwi, hatapata fursa ya kufanya hii biashara. Kwa hiyo, tuwe na vifungu vyetu kama nchi vitakavyosaidia wakulima wetu na wananchi wetu kwa ujumla waweze kunufaika na hii biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabianchi nalo ni jambo ambalo naomba liwekewe mkazo. Kuna ukame ambao hautarajiwi. Mwezangu hapa Mheshimiwa Prof. Manya amezungumzia suala la mabadiliko ya tabianchi yanavyoharibu barabara na kilimo kinavyoathiriwa na ukame. Basi tuje na sheria ambazo zitatusaidia ku-*address* hivi vitu na mabadiliko haya ni mabadiliko ya kusema yaendane na Dira yetu ya Maendeleo ya 2050 ili kama Taifa tujue kwamba tunakwenda mahali salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huo, mengine nimeshaandika kwa maandiko, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi. Nimwite sasa mtoa hoja aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ya kufanya majumuisho ya mjadala kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2024. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia Muswada huu kwa kuzungumza, naomba niwatambue kwa majina, ni Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Kiswaga, Mheshimiwa *Engineer* Manyanya, Mheshimiwa Soud, Mheshimiwa

Kavejuru, Mheshimiwa Profesa Manya na Mheshimiwa Prof. Ndakidemi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa wote ambao wamepata fursa ya kuweza kuchangia kwa mawazo yao mazuri sana ambayo wameyatoa. Pia wote wale ambao hawajapata nafasi ya kuchangia, ninaamini wamewakilishwa vyema na wale ambao wamechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezizungumza kiujumla tumefarijika sana kama Serikali, kwamba tunadhani hatukwenda tofauti na Kamati yetu ya Bunge. Waheshimiwa Wabunge kama ambavyo wamethibitishia Bunge hili Tukufu kwamba yale yote ambayo walitushauri kwenye Kamati tumeyazingatia, na ndiyo maana hapa ukiangalia michango yao yote hakuna jambo kubwa zaidi ya kutupongeza kwa kuweza kuwasikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaahidi kwamba tutaendelea kuisikiliza Kamati yetu na kushirikiana nayo kwa karibu kwa maslahi mapana ya nchi yetu. Yale ambayo wamezungumza kwamba hatujayazingatia, kama ambavyo nilieleza juzi wakati wa taarifa ya Kamati na kama ambavyo Kamati kwenye ripoti yake imeeleza, na Waheshimiwa Wajumbe wamezungumza juu ya ahadi yetu kama Serikali ya kufanyia kazi kwa nguvu sana mapendekezo yao ya marekebisho makubwa ya Sheria ya Mazingira, baadaye mapema ikiwezekana mambo yote yakienda sawa, tukifanikisha kila kitu, tutajitahidi sana ili Bunge lijalo tuweze kuleta kwa ajili ya mabadiliko haya kupitishwa na Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie kama nilivyosema juzi kuwa mpaka sasa tunakwenda vizuri. Ni imani yangu kwamba tutakapokuwa tumeweza kufanya marekebisho hayo makubwa ambayo yatahusisha pamoja na mambo mengine kuangalia upya muundo wa Baraza letu la Mazingira, tutawasilisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, hata suala la uchumi wa buluu na lenyewe ni katika hoja ambayo takribani Wabunge wote waliosimama hapa walizungumza, na lenyewe tunaamini kabisa jambo hili ni muhimu sana na litakuwa ni sehemu ya sheria ambazo tunafanya kila linalowezekana ili tuweze kuziharakisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni mengine ambayo yamezungumzwa, yote yale ambayo hayajakuwemo katika mabadiliko madogo haya ambayo tunakwenda nayo, basi pale ambapo tunaleta mabadiliko makubwa tutayahusisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kimsingi nadhani hakuna la ziada lingine la kulisema. Natambua Mheshimiwa Prof. Manya alizungumzia changamoto mbalimbali kwenye Sekta ya Mazingira, na imani yake ni kwamba mabadiliko haya ya Baraza la *NEMC* yanaweza yakasaidia kupambana na changamoto hizi. Nimhakikishie kwamba, hata sisi tuna imani hiyo, lakini hata kipindi hiki ambacho bado tupo katika hatua za mchakato ambayo ipo *NEMC* tunafanya kila linalowezekana ili changamoto hizi tuweze kukabiliana nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiujumla nimalizie kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri na kwa maono yao ambayo yanalenga katika kusaidia Wizara yetu na Serikali kwa ujumla kutimiza wajibu wake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imekubaliwa. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yussuf Masauni, ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Kamati ya Bunge Zima.

*(Hapa Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2024 *(The Environmental Management (Amendments) Bill, 2024)***

Kifungu cha 1

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 3
Kifungu cha 4

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu Kipya cha 5
Kifungu Kipya cha 6
Kifungu Kipya cha 7

Kifungu Kipya cha 8
Kifungu Kipya cha 9

*(Vifungu vipya vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Kifungu cha 5
Kifungu cha 6

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 7

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 8

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu Kipya cha 12

*(Kifungu Kipya kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Kifungu cha 12

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 13
Kifungu cha 14

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu Kipya cha 15
Kifungu Kipya cha 16

*(Vifungu Vipya vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Kifungu cha 15
Kifungu cha 16

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 17

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu Kipya cha 21
Kifungu Kipya cha 22

*(Vifungu Vipya vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23

Kifungu cha 24
Kifungu cha 25

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Kifungu cha 26

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 27
Kifungu cha 28

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mabadiliko ya mpangilio wa namba kuanzia kifungu cha 5 mpaka 28 kuwa vifungu vya 10 mpaka 33.

*(Mpangilio wa namba za vifungu vilivyotajwa hapo juu ulipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2023,

ninapenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2024 *(The Environmental Management (Amendments) Bill, 2024)* ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2024 *(The Environmental Management (Amendments) Bill, 2024)* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na sasa nitawahoji kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2024 *(The Environmental Management (Amendments) Bill, 2024)* ambao umeshawasilishwa Bungeni.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2024 (The Environmental Management (Amendments) Bill, 2024 Ulipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2024 [*The Environmental Management (Amendments) Bill, 2024*]**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua ya Bunge, kazi yetu imeishia hapa. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Kamati, Mwenyekiti na timu yako kwa kazi kubwa mliyoifanya kuhakikisha Muswada huu mnaelewana na Serikali na hatimaye sasa unapelekwa kwenye mikono ya mamlaka ya juu ya Ofisi ya Rais, kuidhinishwa na kuwa Sheria. Akishasaini sasa inakuwa sheria rasmi.

Nampongeza tena Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri mliyoifanya wewe na timu yako. Pia, nawapongeza Katibu Mkuu, *NEMC* na Wizara ya Mazingira na *Chief Executive* wa *NEMC* Dkt. Sware kwa kazi nzuri ambazo mnafanya. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge. *(Makofi)*

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya shughuli za Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC)* kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kumshukuru Mwenyezi Mung, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia zawadi ya uhai, na hivyo kuwa na fursa ya kukutana hapa siku ya leo. Kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* zilizotekelezwa katika kipindi cha Januari, 2024 hadi Januari, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutimiza madhumuni hayo, Taarifa hii inagusa uchambuzi wa Taarifa za Kaguzi za Kiufundi *(Technical Audits)* na Kaguzi za Ufanisi *(Performance Audits)* kama zilivyokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023. Vilevile Taarifa hii inahusu ziara za ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali na kukaguliwa na Kamati mwezi Machi, 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli nyingine iliyotekelezwa na Kamati ya *PAC* na kutolewa Taarifa inahusu, uchambuzi wa Taarifa ya *CAG* kwa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli hiyo ilifanyika na Taarifa yake iliwasilishwa na kujadiliwa hapa Bungeni kuanzia tarehe 29 hadi 31 Oktoba, 2024. Hivyo, Taarifa hii imefanya rejea ya shughuli hiyo na idadi ya Maazimio ya Bunge yaliyojadiliwa na kuazimiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina na ufafanuzi kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi chote hicho yamefafanuliwa katika sehemu ya pili ya Taarifa hii.

Mheshimwa Naibu Spika, sehemu ya pili ni kuhusu Majukumu ya Kamati. Maudhui ya Taarifa hii yanahusu matumizi ya fedha za umma kwenye Serikali Kuu na Mashirika ya Umma nchini. Mambo hayo yanasimamiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 13 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kwa mujibu wa Kifungu hicho Kamati ina majukumu yafuatayo: -

(a) Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali na Mashirika ya Umma yaliyoainishwa katika Taarifa za *CAG*,

(b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo yaliyobainika kwa mujibu wa kanuni hii, na

(c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Wizara za Serikali na Mashirika ya Umma kuhusu matumizi mazuri ya fedha za umma ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na *CAG* kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 15 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia zilizotumika katika utekelezaji wa kazi za Kamati. Kanuni za Bunge Toleo la Februari, 2023 zimeweka masharti kwamba taarifa yoyote ya Kamati inayoingia Bungeni, inatakiwa kubainisha njia zilizotumiwa na Kamati kufanya kazi inayotolewa taarifa. Njia hizo ni kama zinavyoonyeshwa katika aya ya kwanza na ya tatu ya taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa yangu yote iingie katika Hansard. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, njia na mbinu hizo ziliiwezesha Kamati kufanya uchambuzi wa kina kwa nia ya kulishauri Bunge kuhusu hatua za kuchukua. Mbinu hizo ziliendana na matumizi na marejeo ya miongozo ambayo nayo imeainishwa katika aya ya moja na tatu ya taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ni matokeo ya uchambuzi. Kufuatia vigezo na mambo ya msingi niliyoyataja hapo awali, naomba sasa kutoa maelezo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2024 hadi Februari, 2025 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi na Kaguzi za Kiufundi, kwa kipindi cha shughuli za Kamati cha kuanzia tarehe 15 Januari, 2025 hadi tarehe 25 Januari, 2025, Kamati ilijielekeza katika kupitia na kujadili Taarifa za Kaguzi za Kiufundi *(Technical Audits)* na Kaguzi za Ufanisi *(Performance Audits)*. Taarifa hizi zilitokana na kaguzi zilizokuwa zimefanywa na *CAG* kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefanikiwa kupitia na kujadili jumla ya Taarifa tisa za ukaguzi wa ufanisi na wa kiufundi. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kufanya mahojiano na Maafisa Masuuli wanaosimamia mafungu husika yaliyoguswa na taarifa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya ukaguzi huu wa taarifa hizo tisa kama ifuatavyo: Kwanza, Taarifa ya Ukaguzi ya Kiufundi kuhusu Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato ni sehemu ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Tanzania, sambamba na Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unahusisha ujenzi wa uwanja mpya wa ndege wa Kimataifa wenye kituo cha abiria, barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara mbili za maungio, visaidizi vya usafiri wa anga na huduma zinazohusiana na uendeshaji hasa mtandao wa usambazaji wa mafuta, mifumo ya usambazaji wa maji, vituo vya usambazaji umeme na vifaa vya kuzima moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za ujenzi wa mradi huu ilikadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 329.47. Aidha, Makubaliano ya muundo wa ufadhili wa mradi huo yalifanyika tarehe 13 Machi, 2020 ambapo Benki ya Maendeleo ya Afrika ilikubali kutoa mkopo kwa Serikali ya Tanzania wa kiasi cha Dola za Marekani milioni 271.63 na Serikali ya Tanzania ilitarajiwa kuchangia kiasi cha Dola za Marekani milioni 57.84.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ukaguzi huu wa kiufundi katika Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato ni kama ifuatavyo: -

(a) Ukaguzi ulibaini mradi kuanza kutekelezwa na baadhi ya kwa wahandisi ambao hapo awali hawakuwa wamesajiliwa na Mamalaka husika za Kitaalamu kama vile *ERB* na *CRBO*,

(b) Ukaguzi ulibaini kuanza ujenzi wa majengo bila ya kuwa na hatimiliki na vibali vya ujenzi. Jambo hili lilikuwa kinyume na matakwa ya Kanuni Na. 4(1) ya Kanuni za Ujenzi wa Mipango Miji ya Mwaka 2018 ambayo inahitaji ujenzi wowote kupata kibali cha ujenzi kinachotolewa na mamlaka ya upangaji kulingana na michoro ya ujenzi iliyoidhinishwa na mamlaka ya mji husika;

(c) Ukaguzi ulibaini changamoto katika upembuzi yakinifu wa kina hali iliyosababisha ongezeko la gharama kiasi cha shilingi bilioni 3.04;

(d) Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa ongezeko la malipo kiasi cha shilingi bilioni 5.729 kwa mkandarasi kwa kazi ambazo hazikuidhinishwa na Bodi ya Zabuni. Shilingi bilioni 5.729 hazikuidhinishwa na Bodi ya Zabuni, lakini zimetumika;

(e) Ukaguzi ulibaini kucheleweshwa kwa malipo ya mkandarasi wa kazi za ujenzi wa miundombinu na kusababisha malipo ya riba ya shilingi milioni 303.814; na

(f) Ukaguzi ulibaini kwamba, katika mchakato wa ununuzi Wakala wa Barabara Tanzania iliidhinisha ombi la mapendekezo ya mradi *(RFPs)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Katika Udhibiti wa Usambazaji wa Mbolea kwa Wakulima. Kwa kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 2022/2023, *TFRA* ilitumia kiasi cha shilingi bilioni 392 kwa ajili ya kudhibiti na kuhakikisha uwepo na upatikanaji wa mbolea na virutubisho vya mbolea hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ukaguzi huu wa ufanisi katika udhibiti wa usambazaji wa mbolea ni kama ifuatavyo: -

(a) Ukaguzi ulibaini uwepo wa baadhi ya mbolea na virutubisho vyenye changamoto ya ubora sokoni,

(b) Ukaguzi ulibaini kuwa *TFRA* haikuwa na utaratibu na mfumo madhubuti wa kukadiria mahitaji halisi na ya kutosheleza ya mbolea pamoja na kutumia bilioni zote hizo,

(c) Ukaguzi ulibaini changamoto ya upatikanaji wa mbolea kwa baadhi ya wakulima, mathalani hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 jumla ya idadi ya wakulima waliosajiliwa ilikuwa milioni 3.3. Hata hivyo ni wakulima 838,712 (sawa na 25% ya wakulima waliosajiliwa) ndio waliweza kununua mbolea kupitia mfumo huo. Kwa hiyo, katika milioni tatu, hata milioni moja ya wakulima hawakuweza kutumia mfumo huo kununua mbolea; na

(d) Ukaguzi ulibaini changamoto kadhaa katika matumizi ya Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa pamoja. Mathalani, ukaguzi ulibaini changamoto katika matumizi ya mfumo, na hivyo kutokukidhi mahitaji kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2020/2021 hadi mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kuhusu Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Katika Ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi na Huduma vya Mikoa. Kamati inatambua, inathamini na kupongeza jitihada kubwa na za dhati za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kukubali kutoa fedha jumla ya shilingi bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa vyuo hivyo katika wilaya ambazo zilikuwa hazina vyuo vya ufundi stadi pamoja na Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya ukaguzi huo wa kiufundi kama ifuatavyo: -

(a) Wizara iliandaa makadirio ya gharama za vifaa vya ujenzi na ufundi yanayolingana kwa vyuo vyote 63 vya ufundi stadi vya wilaya. Hivyo, makadirio ya mwanzo hayakuwa yamezingatia uwepo wa utofauti wa umbali na jiografia za maeneo husika;

(b) Uchambuzi wa Kamati katika ukaguzi huu, ulibaini kuwa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Njombe ulianza bila ya kuwa na hatimiliki ya kiwanja na kibali cha ujenzi jambo

ambalo linaweza kusababisha migogoro kati ya Serikali na wamiliki wa awali wa eneo husika;

(c) Ukaguzi ulibaini kuwa, nukuu ya bei kutoka kwa mmojawapo wa Mzabuni kwa ajili ya nondo haikuhusisha gharama za usafirishaji. Hali hii ilisababisha mzabuni kuwasilisha bei ya ziada ya usafirishaji ambayo ilikuwa shilingi milioni 323.7 kwa vyuo 63 vya ufundi stadi vya wilaya na shilingi milioni 15.7 kusafirisha nondo kwa chuo cha ufundi stadi na huduma cha Mkoa wa Songwe;

(d) Ukaguzi ulibaini kuwa, miundombinu ya usalama dhidi ya moto iliyokuwa imeanishwa katika michoro ya usanifu wa ujenzi iliondolewa kwenye makadirio ya gharama za ujenzi hivyo kusababisha kutokujengwa kwa miundombinu hiyo katika vyuo vyote 25 vya ufundi stadi vilivyojegwa,

(e) Ukaguzi ulibaini kuchelewa kukamilika kwa Vyuo sita vya Ufundi Stadi vya Wilaya ya Chemba, Bahi, Igunga, Korogwe na Lushoto kwa miezi 32. Hali hii ilisababisha gharama za madirisha kuongezeka kwa kiasi cha shilingi milioni 175.64. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Katika Udhibiti wa Vifaatiba Katika Vituo vya Umma vya Kutolea Huduma za Afya. Kwa mwaka 2020, Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya ilitumia kiasi cha shilingi bilioni 68.7 kununua vifaatiba kwa vituo vya afya vilivyoko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 22 kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu masuala yaliyobainika katika ukaguzi huo kama ifuatavyo:-

(a) Ukaguzi ulibaini uwepo wa baadhi ya vifaatiba visivyofanya kazi kwa ukamilifu kinyume na malengo yaliyoainishwa kwenye Mpango - Mkakati wa Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania wa Mwaka 2016/2017 - 2020/2021;

(b) Ukaguzi ulibaini changamoto katika taratibu za usajili wa vifaatiba. *TMDA* ilipewa jukumu la kusajili vifaatiba

vinavyotengenezwa ndani na nje ya nchi kabla ya kutumika. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 2022/2023 kulikuwa na vifaatiba 150 kati ya 209 vilivyosajiliwa sawa na 72%, lakini havikurekodiwa na *TMDA,* kwa hiyo, vinaweza kupotea tu;

(c) Ukaguzi ulibaini kuwa kati ya mwaka 2019/2020 hadi 2022/2023, ripoti za ukaguzi na vyeti vya uingizaji wa vifaatiba, hazikuwa na maelezo ya kina kuhusu ukaguzi uliofanyika kwenye vifaatiba katika bandari ya kuingilia. Hii ni kinyume na matakwa ya Kanuni ya 56(1) ya Kanuni ya Chakula, Dawa na Vipodozi Tanzania ya udhibiti wa Vifaatiba ya Mwaka 2015;

(d) Kutokuwepo taratibu sanifu za uendeshaji *(SoP)* kwa vifaatiba katika vituo vya kutolea huduma za afya;

(e) Ukaguzi ulibaini kutokuwepo mfumo thabiti unaofanya kazi ya ufuatiliaji wa utunzaji na matengenezo kinga katika vituo vya kutolea huduma za afya 13 kati ya 17 sawa na 76% ya vituo vilivyotembelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Usimamizi na Ufuatiliaji wa Watoa Huduma za Bima *(TIRA)*. Uchambuzi wa Kamati katika ukaguzi huu umebainisha hoja kadhaa ambazo zinatakiwa kufanyiwa kazi na Serikali ili kuhakikisha thamani halisi ya fedha za umma na maslahi ya wananchi inapatikana katika Sekta ya Bima. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo: -

(a) Ongezeko la 11% la ucheleweshaji wa malipo ya bima yanayodaiwa kwa kampuni za bima. Taarifa ya ukaguzi imebainisha kuwepo kwa ukiukwaji wa Sheria ya Bima ya Mwaka 2009 Sura Na. 394 katika Kifungu cha 131(1) kinachohitaji kila kampuni ya bima kulipa madai ndani ya siku arobaini tu toka tarehe ya kusainiwa hati ya malipo;

(b) Changamoto za kimawasiliano kati ya *TIRA*, watoa huduma za bima na wateja wa bima zipo;

(c) Dosari katika kusimamia ushughulikiaji wa malalamiko yanayotokana na madai ya bima yasiyolipwa;

(d) Ukaguzi pia ulibaini kuwa *TIRA* ilikuwa ikijihusisha na shughuli za kushughulikia malalamiko nje ya mamlaka yake; na

(e) Ukaguzi ulibaini Kampuni za Bima hazikuwa zinaweka ipasavyo dhamana inayotakiwa kisheria katika Benki Kuu ya Tanzania, hivyo ni hatari kwa waliokata bima kuweza kulipwa fedha zao kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Katika Ujenzi wa Kivuko Kipya cha Nyamisati, MV. Kilindoni na Ukarabati wa MV. Kazi na MV. Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania *(TEMESA)* ilifadhili ujenzi wa vivuko mbalimbali kikiwemo kivuko cha MV. Ukara II - Hapa Kazi Tu kilichogharimu shilingi bilioni 4.2, kinachofanya kazi kati ya Bugolora na Visiwa vya Ukara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kivuko cha Chato kilichogharimu shilingi bilioni 3.12, kinachohudumia Nkome hadi Mharamba na visiwa vya karibu vya Senga, Bukondo, na Izumacheli) na kiasi cha shilingi bilioni 5.3 zilitolewa kwa ajili ya kujenga kivuko cha Kilindoni Hapa Kazi Tu kwa ajili ya kuhudumia Kisiwa cha Mafia na Kijiji cha Nyamisati mkoani Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala muhimu yaliyobainika katika ukaguzi wa vivuko tajwa hapo juu kwa muhtasari ni kama ifuatavyo: -

(a) *TEMESA* ilianza ujenzi wa kivuko kipya cha Nyamisati bila kuwa na Taarifa ya Dhana ya Mradi *(Concept note)* haikuwepo*;*

(b) Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa miradi hii yote haukufanyika ipasavyo kwa kukosekana kwa wataalamu wa

kutosha wa ndani wenye uzoefu wa kujenga vivuko vipya kama vile Wahandisi na Wasanifu wa Vivuko;

(c) Miradi hii ilianza kutekelezwa bila kuwa na makadirio ya gharama za uhandisi. Inawezekana hiyo kweli? Yaani hapakuwa na *engineering estimate*. Dosari hii ilisababisha ongezeko la gharama za mradi kwa Kivuko cha Nyamisati kwa kiasi cha shilingi bilioni 3.2; *(Makofi)*

(d) *TEMESA* haikufanya uhakiki wa kina *(Due-diligence)* kabla ya kusaini mkataba wa ujenzi wa kivuko kipya cha Nyamisati. Dosari za usimamizi zilisababisha kiasi cha shilingi milioni 28.5 kujumuishwa katika malipo ya ufundi kwenye kivuko cha *MV. Nyerere* kimakosa, zimetoka hizo shilingi milioni 28 kimakosa; *(Makofi)*

(e) Kuvuja kwa mafuta kwenye injini mpya zilizofungwa kwenye kivuko cha *MV* Kazi; na

(f) *TEMESA* ilitekeleza shughuli za ujenzi na ukarabati wa vivuko bila kuishirikisha *TASAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu huu unaweza kuchangia kutokupatikana thamani ya fedha inayotumika kwenye miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, taarifa ya ukaguzi wa ufanisi kuhusu uwezeshaji wa wachimbaji wadogo wa madini; kwa ujumla hali ya ukusanyaji wa maduhuli katika sekta ya uchimbaji mdogo wa madini imekuwa ikiongezeka kutoka shilingi bilioni 62 mwaka 2018/2019 hadi shilingi bilioni 220 mwaka 2022/2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala muhimu yaliyobainika katika ukaguzi huu yanahusu moja kwa moja mapato ya Serikali kama inavyofuata hapa chini: -

(a) Ukaguzi ulibaini kwamba wachimbaji wadogo hawakupata taarifa za kutosha za kijiolojia na uwepo wa madini

(mashapo). Wachimbaji wadogo 48 tu sawa na asilimia moja ya leseni zote zilizotolewa mwaka 2021/2022, ndio walipata huduma za uchenjuaji;

(b) Ukaguzi ulibaini kupitia ripoti ya utendaji wa kila mwaka kutoka Wizara ya madini kuwa, kulikuwa na changamoto ya upatikanaji wa mikopo na ruzuku kwa wachimbaji wadogo wa madini;

(c) Ukaguzi ulibaini kuwa mahitaji na vipaumbele vya wachimbaji wadogo hayakuhusishwa kikamilifu wakati wa maandalizi ya mipango ya mwaka ya Wizara na Bajeti zake;

(d) Ukaguzi ulibaini utengaji wa rasilimali usiotosheleza kwa wachimbaji wadogo; na

(e) Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na changamoto ya tathmini ya uwezeshaji wa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba nane ni taarifa ya ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Uchambuzi wa taarifa ya ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi ilibaini masuala kadhaa ambayo yanahusiana na fedha za umma kama ifuatavyo: -

(a) Changamoto katika usimamizi wa shughuli za uvuvi kama vile utoaji wa leseni bila vibali vya aina na kiasi cha samaki wa kuvuliwa, kwa hiyo, kuvua kulikuwa holela tu;

(b) Ziwa Tanganyika lilikuwa na 45% mialo isiyo na vitengo vya usimamizi wa fukwe, bahari ya Hindi ikiwa na 36%, wakati Ziwa Victoria lilikuwa na idadi ndogo tu ya asilimia moja ya miale isiyokuwa na usimamizi wa fukwe;

(c) Vyombo vingi vya uvuvi havijasajiliwa au havina leseni, hali inayochangia uvuvi haramu na kutokuwepo kwa takwimu sahihi za uvuvi. Hii imesababisha hasara inayokadiriwa kuwa shilingi bilioni 15.16;

(d) Ukaguzi ulibaini uwepo wa samaki wadogo sana sokoni kinyume na kanuni za uvuvi;

(e) Ukaguzi ulibaini changamoto katika ukusanyaji na usimamizi wa takwimu za uvuvi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili, ni taarifa za ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Taarifa ya kina ya miradi hiyo inaonekana katika aya 2.2 ya taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Taarifa ya Mthibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa ukaguzi wa hesabu za Serikali Kuu na mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 29 Oktoba, 2024 Kamati ya *PAC* iliwasilisha taarifa zake Bungeni kuhusu uchambuzi wa Taarifa za *CAG* kwa Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2023…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungmzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mwenyekiti twende kwenye maoni na mapendekezo.

**MHE. NAGENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya, ahsante. Maoni na mapendekezo; Mapendekezo yafuatayo yametokana na hayo yote niliyoongea hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukaguzi wa kiufundi, ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Msalato, Bunge linaazima kwamba:-

(a) Serikali ifanye mapitio ya vipaumbele vya mikataba ya makubaliano ya ufadhili *(financing agreement)* ili kuweka usawa wa malipo ya gharama zinazoongezeka kwa kuhakikisha kuwa upande uliosababisha ongezeko hilo unawajibika;

(b) Serikali ihakikishe Wizara ya Ujenzi na *TANROADS* wanasimamia kikamilifu mradi na kufanya tathmini ya kina kuhusu hasara zilizotokana na dosari za awali za usanifu, ikiwa ni pamoja na kuweka uwajibikaji wa gharama zilizozalishwa kwa pande zinazohusiana na mkataba; na

(c) *TANROADS* ihakikishe kuwa kazi zilizoongezeka na zitakazoendelea kuongezeka zinaidhinishwa na Bodi ya zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusu ukaguzi wa kuhusu ukaguzi wa kiufundi katika Ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi na Huduma vya Mikoa, Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Wizara ya Fedha itoe kipaumbele cha kutoa fedha za kukamilisha miradi ya ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi ili vikamilike na kuanza kutoa ujuzi kwa Vijana wa Kitanzania kama ilivyokusudiwa;

(b) Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)* zihakikishe kunakuwepo usimamizi thabiti wa miradi ya ujenzi wa vyuo vya ufundi ili kufikia viwango vya ubora vya ujenzi vinavyokubalika; na

(c) Serikali ihakikishe kuwa mahitaji yote muhimu ikiwemo mifumo ya kupambana na majanga ya moto inajumuishwa katika ujenzi unaoendelea wa vyuo vya ufundi stadi na huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuhusu ukaguzi wa ufanisi katika udhibiti wa usambazaji wa mbolea kwa wakulima, Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Mamlaka ya Udhibiti Mbolea Tanzania ziimarishe mifumo ya usambazaji wa mbolea kwa kuzingatia ubora, bei elekezi…

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mwenyekiti, kengele ya pili hiyo. Toa kauli kuwa zote ziingie kwenye *Hansard*.

**MHE. NAGENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa yangu yote iingie katika *Hansard*, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mwenyekiti hujatoa hoja. Maana mimi nilitaka ukakae niahirishe Bunge sasa hivi, maana ulikuwa huna hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. NAGENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani sana. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC)
## TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI KWA MWAKA 2024
## SEHEMU YA KWANZA

### MAELEZO YA JUMLA
Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia zawadi ya uhai na hivyo kuwa na fursa ya kukutana hapa siku ya leo. Kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) zilizotekelezwa katika kipindi cha Januari 2024 hadi Januari 2025.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutimiza madhumuni hayo, Taarifa hii inagusa uchambuzi wa Taarifa za Kaguzi za Kiufundi *(Technical Audits)* na Kaguzi za Ufanisi *(Perfomance Audits)* kama zilivyokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023. Vilevile Taarifa hii inahusu ziara za ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali na kukaguliwa na Kamati Mwezi Machi, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** shughuli nyingine iliyotekelezwa na Kamati na kutolewa Taarifa inahusu, uchambuzi wa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023. Shughuli hiyo ilifanyika na Taarifa yake iliwasilishwa na kujadiliwa hapa Bungeni kuanzia tarehe 29 hadi 31 Oktoba, 2024.Hivyo, Taarifa hii imefanya rejea ya shughuli hiyo na idadi ya Maazimio ya Bunge yaliyojadiliwa na kuazimiwa.

**Mheshimiwa Spika,** maelezo ya kina na ufafanuzi kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi chote hicho yamefafanuliwa katika sehemu ya pili ya Taarifa hii.

**Muundo wa Taarifa**

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya kurahisisha ufuatiliaji wa Taarifa hii, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla ikiwemo muundo wa Taarifa, majukumu ya Kamati, msingi wa kazi za Kamati na muhtasari wa matokeo ya uchambuzi. Lengo la sehemu hii ni kubainisha muktadha wa Taarifa ili kuwezesha ufuatiliaji utakaosaidia kufanya uamuzi.

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa shughuli zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi cha Mwezi Januari, 2024 hadi Februari, 2025.Katika sehemu hii, Taarifa inafafanua mambo ya msingi kuhusu uchambuzi na kubainisha matokeo ya uchambuzi huo. Lengo la sehemu hii ni kuonesha hoja zilizobainika katika matumizi ya fedha za umma na kuweka msingi wa mtazamo wa Kamati kuhusu matumizi ya fedha za umma kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024. Sehemu hii inajenga msingi wa sehemu ya tatu ya taarifa inayohusu Maoni na Mapendekezo.

**Majukumu ya Kamati**

**Mheshimwa Spika**, maudhui ya Taarifa hii yanahusu matumizi ya fedha za umma kwenye Serikali Kuu na Mashirika ya Umma Nchini. Mambo hayo yanasimamiwa na Kamati ya Kudumu ya

Bunge ya Hesabu za Serikali kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 13 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kwa mujibu wa Kifungu hicho Kamati ina majukumu yafuatayo: -

a) Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali na Mashirika ya Umma yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG);

b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo yaliyobainika kwa mujibu wa kanuni hii; na

c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Wizara za Serikali na Mashirika ya Umma kuhusu matumizi mazuri ya fedha za umma ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 15 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

**Njia zilizotumika Katika Utekelezaji wa Kazi za Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni za Bunge Toleo la Februari, 2023 zimeweka masharti kwamba Taarifa yoyote ya Kamati inayoingia Bungeni, inatakiwa kubainisha njia zilizotumiwa na Kamati kufanya kazi inayotolewa Taarifa. Kwa msingi huo naomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika na kuwezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba kuzitaja njia hizo kama ifuatavyo: -

a) Mapitio ya jumla ya Ripoti za CAG ili kubaini maeneo ya kuwekea mkazo na kukidhi masharti ya Ripoti hiyo ulikuwa msingi wa kazi za Kamati zilizopangwa kwenye Ratiba;

b) Kupokea vidokezo (*"briefs")* vya Ripoti za CAG kwa hoja za ukaguzi za mafungu yaliyopangwa kujadiliwa na Kamati kabla ya Kukutana na Afisa Masuuli anayehusika. Mbinu hii iliiwezesha Kamati kuzielewa hoja na wigo wa mahojiano na Afisa Masuuli kwa lengo la kupata undani wa tatizo la matumizi mabaya ya fedha za umma;

c) Mahojiano na maafisa masuuli kuhusu hoja za ukaguzi ili kupata undani wa matatizo ya matumizi ya fedha za umma na kubaini chimbuko la tatizo, wigo wa dosari na uwezekano wa kuepuka matumizi mabaya ya fedha za umma kwa siku zijazo;

d) Uchambuzi wa kina wa Taarifa za Wakaguzi wa hesabu za Fungu linalohusika kwa pamoja na majibu ya Menejimenti za Taasisi, wizara au Shirika lililokaguliwa. Lengo ni kuelewa kwa kina muktadha wa hoja na matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za Umma; na

e) Tafiti mbalimbali kuhusu masuala ya usimamizi wa fedha za umma. Lengo la njia hii ni kuona na kuutumia uzoefu wa jumla unaopatikana kwa tafiti hizo ili kutathmini maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma kama yalivyoainishwa na CAG.

**Mheshimiwa Spika,** njia na mbinu hizo ziliiwezesha Kamati kufanya uchambuzi wa kina kwa nia ya kulishauri Bunge kuhusu hatua za kuchukua. Mbinu hizo ziliendana na matumizi na marejeo ya miongozo ifuatayo: -

a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inayoonesha dhamana ambayo Serikali imepewa na wajibu wa Bunge kuisimamia na kuishauri Serikali ikiwemo eneo la matumizi ya fedha za umma;

b) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008 inayofafanua masharti muhimu kwa ajili ya kuwezesha ukaguzi,

uandaaji wa Ripoti za CAG, uwasilishaji wake na hatimaye kujadiliwa na Kamati na Bunge;

c) Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348 inayoweka miongozo ya matumizi ya fedha za umma na kusaidia kuamua iwapo kuna matumizi mabaya ya fedha za umma;

d) Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, inayohusika na usimamizi wa matumizi ya Fedha za Umma kwa kuweka taratibu za utekelezaji wa bajeti na usimamizi wake;

e) Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370 inayogusa usimamizi wa matumizi ya Fedha za Umma katika mashirika ya umma;

f) Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410, inayoweka taratibu za kufuatwa wakati wa ununuzi wa bidhaa, huduma na kuingia mikataba kwa gharama ambazo zinahusisha matumizi ya fedha za umma;

g) Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, Sura 286, inayosimamia weledi wa wahasibu na wakaguzi ili kuwezesha kumbukumbu za kutumainiwa za fedha na usimamizi bora wa matumizi ya Fedha za Umma;

h) Sheria ya Kinga Madaraka na Haki za Bunge, Sura 296 inayoliwezesha Bunge, Wabunge na Kamati za Bunge kupata stahili kutokana na madaraka yake na kupata ushahidi bila kukwama wakati wa kufuatilia matumizi ya fedha za umma; na

i) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 zinazobainisha utaratibu wa Ripoti za CAG kuhusu matumizi ya fedha za umma kuwasilishwa Bungeni, kushughulikiwa na Kamati na hatimaye Kamati kutoa Taarifa hii Bungeni.

**Vigezo vya Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, uaandaji wa vigezo vya kuzingatiwa ni jambo muhimu katika uhakiki na tathmini yoyote ile. Suala la matumizi mabaya ya fedha za umma linaweza kubainika kutokana na vigezo vya matumizi ya fedha za umma. Aidha, uamuzi wa kuwahoji Maafisa Masuuli kutokana na Taarifa za CAG ni jambo lililohitaji kuwekewa vigezo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa sababu hiyo, baada ya kupokea Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati ilitengeneza vigezo muhimu vya kuzingatia katika kutimiza majukumu yake ya Kikanuni.

Vigezo hivyo vilitoa mwongozo wa uchaguzi wa mafungu ambayo yalipewa kipaumbele katika uchambuzi na mahojiano na Maafisa Masuuli.Aidha, vigezo hivyo vilisaidia katika kuchagua miradi ambayo ilitembelewa katika ziara za ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika**, vigezo vilivyozingatiwa wakati wa kuchagua vipaumbele katika utekelezaji wa shughuli za Kamati vilikuwa kama ifuatavyo: -

a) Uzito wa hoja ya ukaguzi kama ilivyoibuliwa na CAG;

b) Maslahi ya umma kuhusu hoja za fungu linalohusika;

c) Hali ya hati ya ukaguzi iliyotolewa kwa fungu linalohusika;

d) Kujirudia mara kwa mara kwa hoja husika katika Wizara, Idara, Wakala, Balozi au Mradi wa Maendeleo uliokaguliwa;

e) Kiwango cha fedha kinachohusika katika hoja za ukaguzi wa fungu linalohusika;

f) Kuleta uendelevu wa ufuatiliaji wa ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati kwa fungu husika kwa siku za nyuma;

g) Kutoa kipaumbele kwa sekta na taasisi za kimkakati *(Strategic Sectors and Parastatals)* kwa kuzingatia utekelezaji wa malengo ya sasa ya Serikali;

h) Kutoa kipaumbele kwa kaguzi maalum *(Special Audits)* zilizofanyika hivi karibuni; na

i) Uzingatiaji wa kaguzi za ufanisi na kaguzi za kiufundi kwa mwaka husika.

**Mheshimiwa Spika,** vigezo hivyo viliisaidia Kamati kuendelea na mchakato wa kufuatilia matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Ripoti za CAG. Nikiri kuwa vigezo hivyo vimeisadia Kamati kufikia lengo la kupitia na kuchambua taarifa nyingi na kubainisha maeneo yenye mapungufu katika matumizi ya fedha za umma.

## SEHEMU YA PILI

## MATOKEO YA UCHAMBUZI

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia vigezo na mambo ya msingi niliyoyataja hapo awali, naomba sasa kutoa maelezo ya kina kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2024 hadi Januari, 2025 kama ifuatavyo: -

### Uchambuzi wa Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi na Kaguzi za Kiufundi

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha shughuli za Kamati cha kuanzia tarehe 15 Januari, 2024 hadi tarehe 25 Januari, 2024, Kamati ilijielekeza katika kupitia na kujadili Taarifa za Kaguzi za Kiufundi *(Technical Audits)* na Kaguzi za Ufanisi *(Perfomance Audits)*. Taarifa hizi zilitokana na kaguzi zilizokuwa zimefanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanikiwa kupitia na kujadili jumla ya Taarifa tisa (09) za ukaguzi wa ufanisi na wa kiufundi. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kufanya mahojiano na Maafisa Masuuli wanaosimamia mafungu husika yaliyoguswa na taarifa hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa nipende kukushukuru tena kwa kuipa fursa Kamati hii kupitia na kuchambua Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi wa Kiufundi. Hatua hii ni ya kipekee na ya mfano kwa Bunge letu ukilinganisha na Mabunge mengine katika Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara. Kaguzi hizi zina mawanda mapana kwa kutoangalia masuala ya fedha peke yake bali kwa kuangalia ufanisi, tija na uwekevu mtawalia (efficiency, economy & effectiveness respectively).

**Mheshimiwa Spika,** hatua hii ya uwajibikaji iliyofikiwa katika Bunge letu inathibitishwa kwa kurejea tena maelezo ya Ndugu George C. Haule ambaye ni Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) anayesimamia Kaguzi za Ufanisi na Kiufundi aliyoyatoa mbele ya Kamati kuhusu umuhimu wa Taarifa hizi. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo[1] yake kama ifuatavyo: -

**Nukuu:**

> ***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, tunapenda kutoa shukurani zetu za dhati kabisa kupata fursa hii, kwa kweli kwenye preamble ulitoa ulizungumzia dhamira ya Bunge letu kupitia Kamati yetu hii ya kuhakikisha kwamba taarifa za ukaguzi wa ufanisi na zile za kiufundi zinafanyiwa kazi. Hili tunaliona Kamati yako inalifanyia kazi na kila mwaka kwa kweli taarifa za ukaguzi wa ufanisi zinafanyiwa kazi vizuri na mmekuwa very effective na tunaona matunda yake sisi ambao tupo field…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

[1] Rejea Uk. 2 wa Majadiliano Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge Kikao cha Pili, Tarehe 14 Januari, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya uchambuzi wa Taarifa hizo tisa (09) kama ifuatavyo: -

***Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Kuhusu Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato***

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato ni sehemu ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Tanzania, sambamba na Dira ya Maendeleo ya Tanzania (TDV)[2] 2025. Mradi huu unahusisha ujenzi wa uwanja mpya wa ndege wa kimataifa wenye kituo cha abiria, barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara mbili za maungio, visaidizi vya usafiri wa anga na huduma zinazohusiana na uendeshaji hasa mtandao wa usambazaji wa mafuta, mifumo ya usambazaji wa maji, vituo vya usambazaji umeme na vifaa vya kuzima moto.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa kwa awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza inahusisha loti ya kwanza pekee na ndiyo inayoendelea sasa katika vifurushi viwili. Kifurushi cha kwanza kinahusiana na ujenzi wa miundombinu ya barabara na kifurushi cha pili kinahusiana na ujenzi wa majengo.

**Mheshimiwa Spika,** gharama za ujenzi wa mradi huu ilikadiriwa kuwa **Dola za Marekani Milioni 329.47**. Aidha Makubaliano ya muundo wa ufadhili wa mradi huo yalifanyika tarehe 13 Machi, 2020 ambapo Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB)[3] ilikubali kutoa mkopo kwa Serikali ya Tanzania wa kiasi cha **Dola za Marekani Milioni 271.63** na Serikali ya Tanzania ilitarajiwa kuchangia kiasi cha **Dola za Marekani Milioni 57.84**.

**Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini kama Wakala wa Barabara Tanzania anasimamia ujenzi wa kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Msalato kwa ufanisi, amefanya ununuzi kwa njia sahihi ili kuhakikisha thamani ya fedha inakuwepo. Aidha, ukaguzi ulilenga kubainisha iwapo TANROADS

[2] Tanzania Development Vision, 2025 (TDV).

[3] African Development Bank (AFDB).

ilifanya usanifu wa mradi kwa mujibu wa viwango na amehakikisha kuwa hakuna ongezeko la gharama zisizotarajiwa wakati utekelezaji wa mradi ukiwa unaendelea ili kufikia ubora unaotakiwa kulingana na viwango vilivyowekwa. Aidha ukaguzi ulitathmini hatua za uanzishaji, upangaji na utekelezaji wa mradi huo isipokuwa kwa hatua ya kufunga mradi kwani mradi ulikuwa bado upo kwenye hatua za utelezaji.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya ukaguzi huu wa Kiufundi katika Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato ni kama ifuatavyo: -

a) Ukaguzi ulibaini kutumika kwa wahandisi ambao hapo awali hawakuwa wamesajiliwa na Mamalaka husika za Kitaalam katika utekelezaji wa mradi. Kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Usajili wa Wahandisi ya mwaka 2007 kinahitaji wahandisi waliosajiliwa tu kufanya kazi za uhandisi za kitaalamu na kwamba wafanyakazi wote wanaofanya kazi kama wahandisi wataalamu wasajiliwe kwenye Bodi ya Usajili wa Wahandisi;

b) Ukaguzi ulibaini kuanza ujenzi wa majengo bila ya kuwa na hatimiliki na vibali vya ujenzi. Jambo hili lilikuwa kinyume na matakwa ya Kanuni Na.4(1) ya Kanuni za Ujenzi wa Mipango Miji ya mwaka 2018 ambayo inahitaji ujenzi wowote kupata kibali cha ujenzi kinachotolewa na mamlaka ya upangaji kulingana na michoro ya ujenzi iliyoidhinishwa na mamlaka ya mji husika;

c) Ukaguzi ulibaini changamoto katika upembuzi yakinifu wa kina hali iliyosababisha ongezeko la gharama kiasi cha **Shilingi Bilioni 3.04.** Kwa mujibu wa sehemu ya 3.3 ya mwongozo wa usanifu wa Kijiometri wa Barabara wa wizara ya Ujenzi wa mwaka 2011 unaelekeza upembuzi yakinifu kufanyika kwenye masuala ya hali ya udongo, kiwango cha mteremko kwenye eneo la mradi, gharama za ujenzi na uchaguzi wa njia ya kupitisha barabara. Aidha tofauti katika vipimo hivi ilitokana na mbinu iliyotumika wakati wa upembuzi yakinifu ambapo ndege nyuki *(drones)* zilitumika kupima mwinuko wa

usawa wa ardhi bila kusafisha eneo la mradi, hivyo kutotafsiri kwa usahihi kuwa usawa wa vichaka kama ndiyo usawa wa ardhi. Hali hii ilipelekea kuathiriwa kwa utekelezaji wa mradi kutokana na tofauti kati ya viwango halisi vya mwinuko na viwango vya michoro;

d) Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa ongezeko la malipo kiasi cha **Shilingi Bilioni 5.729** kwa mkandarasi kwa kazi ambazo hazikuidhinishwa na Bodi ya Zabuni. Mapitio ya hati ya malipo ya kazi za ujenzi namba tisa kwa mkataba wa kwanza kwa ajili ya kazi za miundombinu ambayo ilihusisha malipo ya hati zilizopita (hati namba moja hadi hati namba nne), yalionesha malipo ya **Shilingi Bilioni 5.729** kutokana na mabadiliko ya kazi katika vipengele vya makadirio ya gharama za ujenzi wa mradi bila kupata idhini ya Bodi ya Zabuni. Mabadiliko haya yalitokana na changamoto katika usanifu na dosari ya vipimo vya usawa wa ardhi wakati wa upembuzi yakinifu wa tipografia;

e) Ukaguzi ulibaini kucheleweshwa kwa malipo ya mkandarasi wa kazi za ujenzi wa miundombinu na kusababisha malipo ya riba ya **Shilingi Milioni 303.814**, hadi kufikia hati Na. 9 ya mkandarasi wa kifurushi cha kwanza. Malipo ya mradi yalicheleweshwa kwa muda wa kati ya siku nane (8) hadi siku sabini (70), hali hii ilipelekea gharama zilizotokana na riba kuongezeka. Aidha Serikali ya Tanzania ilitakiwa kulipa riba hizi kulingana na makubaliano yake na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB); na

f) Ukaguzi ulibaini kwamba, katika mchakato wa ununuzi Wakala wa Barabara Tanzania iliidhinisha ombi la mapendekezo ya mradi (RFPs)[4] ambayo hayakukamilika. Maombi hayo yalikosa maelezo muhimu kama vile mawanda ya kazi, michoro ya mradi na vipengele vya ongezeko la thamani na viwango vya ubora wa mradi. Hali hii ilisababisha zaidi ya maombi 50

[4] RFP (request For Proposal).

ya ufafanuzi kutoka kwa wazabuni ambapo nusu yake hayakujibiwa.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hoja zilizobainishwa hapo juu CAG alitoa mapendekezo 15 ambayo yalitakiwa kufanyiwa kazi ili kuboresha mradi husika. Ufuatiliaji wa mapendekezo hayo ulibaini kuwa mapendekezo 2 kati ya 15 yalikuwa yametekelezwa kikamilifu, mapendekezo 8 kati ya 15 yalikuwa yapo katika hatua za utekelezaji unaoridhisha. Aidha mapendekezo 4 kati ya 15 yalikuwa yapo katika hatua za awali za utekelezaji na pendekezo 1 kati ya 15 lilikuwa bado halijatekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 16 Januari, 2025 Kamati ilikutana na Afisa Masuuli Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Afisa Masuuli Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) ili kujadili kwa kina hoja za ukaguzi wa kiufundi ambazo hazijatekelezwa kwa ukamilifu. Kuhusu hoja ya kutumia wahandisi wasiosajiliwa na Bodi ya Wahandisi Afisa Masuuli TANROADS alikiri kuwa wakati mradi unaanza baadhi ya wahandisi walikuwa hawajasajiliwa kwasababu walikuwa bado wanasubiria vibali kutoka Mamlaka nyingine lakini kwa sasa wote wamesajiliwa na Bodi ya Wahandisi kwa mujibu wa matakwa ya Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, kwa hoja inayohusu ujenzi kukidhi viwango tarajiwa, Afisa Masuuli TANROADS aliifahamisha kamati kuwa ujenzi huo umezingatia viwango vya kimataifa katika ujenzi wake. Aidha, Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kuwa, mapendekezo ya CAG yanayohusu ubora wa kazi yataendelea kufanyiwa kazi kwa weledi kadri mradi unavyoendelea kutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa hoja ya malipo ya ziada ambayo hayakuidhinishwa na Bodi ya Zabuni kutokana na kuongezeka kwa kazi, Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kuwa ongezeko la kazi hizo lilitokana na dosari zilizojitokeza wakati wa kufanya upembuzi yakinifu wa mradi. Aidha, kuhusu malipo kwa mshauri elekezi kuwa makubwa ukilinganisha na kiwango cha kazi kilichofanyika, Afisa Masuuli alikiri kuwa kuchelewa kuanza kwa

utekelezaji wa mradi katika kifurushi cha pili ndio kulisababisha ongezeko hilo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maelezo ya kina ya Afisa Masuuli Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Afisa Masuuli Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), Kamati imetoa mapendekezo mahsusi kwaajili ya maboresho katika sehemu ya tatu (3) ya taarifa hii ambayo yanalenga kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati, kwa ubora uliokusudiwa na bila ongezeko zaidi la gharama za mradi.

***Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Katika Udhibiti wa Usambazaji wa Mbolea kwa Wakulima***

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano kuanzia Mwaka 2021/22 hadi 2025/26 unabainisha kuwa Sekta ya Kilimo Nchini Tanzania inachangia takribani asilimia 27 ya Pato la Taifa, pia inatoa ajira kwa asilimia 65 ya wananchi na huchangia asilimia 24 ya mapato yanayotokana na uuzaji wa bidhaa nje ya nchi. Aidha, kilimo ni chanzo kikuu cha chakula kwa wananchi na chanzo kikubwa cha malighafi za viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa sehemu ya 4(1) ya Sheria ya Mbolea ya Mwaka 2009, usambazaji wa mbolea na virutubisho vya mbolea unajumuisha shughuli mbalimbali kama vile usajili, utoaji wa leseni za mbolea kwa wafanyabiashara, utoaji wa vibali vya uagizaji na usafirishaji, ukaguzi wa mbolea na wafanyabiashara wa mbolea na udhibiti wa bei ya mbolea na virutubisho vya mbolea.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2022/23, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) ilitumia kiasi cha **Shilingi Bilioni 392** kwa ajili ya udhibiti na kuhakikisha uwepo na upatikanaji wa mbolea na virutubisho vya mbolea hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la ukaguzi huu lilikuwa ni kutathmini iwapo Wizara ya Kilimo kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) inasimamia kwa ufanisi usambazaji wa mbolea ili

kuhakikisha mbolea bora na virutubisho vya mbolea vyenye ubora vinapatikana kwa wakati kwa wakulima. Aidha ukaguzi ulihusisha kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2020/21 hadi 2022/23. Kipindi hiki kilichaguliwa kwasababu ni wakati ambao Serikali ilifanya juhudi kubwa ya kuanzisha mipango mbalimbali ili kuhakikisha uwepo na upatikanaji wa mbolea kwa wakulima nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Ukaguzi huu ulitathmini mambo kadhaa ambayo ni kama ifuatavyo: -

a) Ufanisi wa mfumo wa makadirio ya mahitaji, utoshelevu wa uratibu na ushirikishwaji wa wadau wote muhimu wanaohusika katika kukadiria mahitaji ya mbolea;

b) Ufanisi wa Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja (BPS) katika kuwezesha kuagiza mbolea kwa wakati na kwa utoshelevu;

c) Ufanisi wa huduma za udhibiti zinazotolewa na TFRA katika udhibiti wa bei ya mbolea;

d) Utoshelevu wa mipango na taratibu za ukaguzi wa mbolea na wauzaji wa mbolea; na

e) Ufanisi wa viashiria vya kupima utendaji vilivyowekwa, upatikanaji wa takwimu kamili na zenye uhakika ili kuwezesha ufuatiliaji wa utoshelevu wa mchakato wa usambazaji na utoshelevu katika kufanya tathmini ya utendaji wa TFRA.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya ukaguzi huu wa ufanisi katika udhibiti wa usambazaji wa mbolea ni kama ifuatavyo: -

(a) Ukaguzi ulibaini uwepo wa baadhi ya mbolea na virutubisho vyenye changamoto ya ubora sokoni (Maduka yanayouza mbolea). Ripoti ya ukaguzi ilibaini ongezeko la mbolea zisizosajiliwa sokoni kutoka aina saba (7) mwaka 2020/21 hadi kumi na mbili (12) mwaka

2022/23. Aidha, kulikuwa na matukio ya wauzaji wa mbolea kuuza mbolea ambazo zilikuwa zimegandamana, zilizokwisha muda wake wa matumizi na ambazo hazikufungwa vizuri au kuwekwa kwenye mifuko iliyo funguliwa jambo ambalo linaathiri ubora wa mbolea hizo;

(b) Ukaguzi ulibaini Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania haikuwa na utaratibu na mfumo madhubuti wa kukadiria mahitaji halisi na ya kutosheleza ya mbolea. Ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ilikusanya takwimu na taarifa za mahitaji kutoka Halmashauri na kuzitumia kukadiria mahitaji ambayo hayakuweza kutoa taarifa sahihi ya mbolea inayohitajika. Dosari katika ukadiriaji wa mahitaji ulisababishwa na uhaba wa Maafisa Kilimo katika ngazi ya kijiji ambao walihitajika kuainisha na kukadiria aina ya mbolea inayohitajika kulingana na udongo katika vijiji vyao;

(c) Ukaguzi ulibaini changamoto ya upatikanaji wa mbolea kwa baadhi ya wakulima, mathalani hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 jumla ya idadi ya wakulima waliosajiliwa ilikuwa 3,389,951, hata hivyo ni wakulima 838,712 (sawa na asilimia 25 ya wakulima waliosajiliwa) ndio waliweza kununua mbolea kupitia mfumo. Hii inamaanisha kwamba wakulima 2,551,239 sawa na asilimia 75 hawakuweza kupata mbolea ya ruzuku. Ukaguzi ulibaini pia upatikanaji mdogo wa mbolea ya ruzuku na kukosekana kwa wasambazaji katika baadhi ya Halmashauri ni miongoni mwa sababu zilizo changia matumizi madogo ya mbolea na kutokufikiwa kwa wakulima walio wengi na mbolea ya ruzuku; na

(d) Ukaguzi ulibaini changamoto kadhaa katika matumizi ya Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja. Lengo la kuanzishwa kwa mfumo wa ununzi wa pamoja lilikuwa ni kuhakikisha upatikanaji wa mbolea na kusaidia kupunguza bei kutokana na kuagizwa kwa mbolea nyingi kwa mara moja. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini

changamoto katika matumizi ya mfumo na hivyo kutokukidhi mahitaji, kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2020/21 hadi mwaka 2022/23 Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja (BPS) haukutumika kuagiza kutoka nje kwa msimu wa kilimo wa 2020/21.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana hoja za ukaguzi zilizobainika Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alitoa jumla ya mapendekezo 9 ambapo mapendekezo 3 yalielekezwa Wizara ya Kilimo na mapendekezo 6 yalielekezwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ulibaini kuwa mapendekezo 2 kati ya 9 yametekelezwa kikamilifu na mapendekezo 7 kati ya 9 yapo katika hatua za utekelezaji unaoridhisha na hakuna pendekezo ambalo halijatekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 15 Januari, 2025, Kamati ilikutana na Afisa Masuuli Wizara ya Kilimo pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania ili kujadili hoja za ukaguzi wa ufanisi ambazo bado hazijajibiwa kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu mbolea ya ruzuku Afisa Masuuli aliifahamisha kamati kuwa kwa sasa Serikali haitoi mbolea ya ruzuku bali imeweka fedha kwa kila mfuko wa mbolea kwa wauzaji waliosajiliwa kuuza mbolea ya ruzuku kwa nchi nzima. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Ndugu Gerald G. Mweli, Katibu Mkuu, Wizara ya Kilimo aliyotoa mbele ya Kamati akifafanua kuhusu hoja hii kama ifuatavyo[5]:-

**Nukuu: -**

***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza, Tanzania, Serikali hainunui mbolea kwa ajili ya kugawa ruzuku, bali inaweka fedha kwa ajili ya kugharamia ruzuku. Tunagharamiaje sasa? Tumeruhusu kila mtu mwenye mbolea aisajili na mbolea yake, baada ya***

[5] Rejea Ukurasa wa 20 wa Taarifa Rasmi za Bunge, Kikao cha Pili, Tarehe 15 Januari, 2025.

***kuisajili inapewa QR Code very special number za QR Code. Wakati tunaanza ruzuku, mfuko mmoja wa DAP ulikuwa 120,000 mpaka 130,000. Serikali ikasema mkulima atanunua kwa shilingi 70,000. Mheshimiwa Mwenyekiti kwa hiyo kwa kila bag ambayo mkulima anauziwa 70,000, Serikali inalipa shilingi 50,000. Kwa hiyo, muuzaji na muingizaji wa mbolea kwa sasa siyo Serikali ni watu binafsi ili kuondoa upotevu na changamoto zilizokuwepo kwenye mifumo mingi …"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu udhibiti wa ubora wa mbolea zinazo zalishwa nchini na zinazo agizwa nje ya nchi Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kuwa anaye sajiliwa kuingiza mbolea nchini ni yule aliyetambuliwa kuwa ataingiza mbolea hivyo ni kazi ya TFRA kupima ubora wa mbolea hizo na kutoa idhini ya kutumika na wakulima au kuzuia kuingizwa sokoni.

**Mheshimiwa Spika,** Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kuwa kuna mbolea nyingine zinatengenezwa na viwanda bubu ndani ya nchi ambazo nyingi wamekuwa wakizikamata na kupima ubora wake ili kubainisha iwapo zinafaa kwa matumizi ya wakulima wetu. Aliendelea kuifahamisha Kamati kuwa suala hili linashughulikiwa kwa jitihada kubwa ili kuhakikisha wakulimwa wanatumia mbolea na virutubisho vilivyokidhi viwango vya ubora. Naomba kununukuu sehemu ya maelezo ya Ndugu Joel Laurent, Mkurugenzi Mkuu wa TFRA kuhusu idadi na kiwango cha matumizi ya mbolea aliyotoa kwa Kamati kama ifuatavyo[6]:-

**Nukuu:**

***"…Mheshimiwa Mwenyekiti na Wajumbe, naomba nimshukuru sana Katibu Mkuu kwa kutoa ufafanuzi. Labda ni jambo dogo tu la kuongezea ni***

[6] Rejea Ukurasa wa 27 wa Taarifa Rasmi za Bunge, Kikao cha Kamati Tarehe 15 Januari, 2025.

***kwamba, kwa mikakati ilikuwa inafanyika ni kwamba matumizi ya mbolea yameongezeka kutoka tani 3,223 kwa mwaka 2022/2023 mpaka kufikia tani 8,040 kwa mwaka 2023/2024…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na maelezo ya Afisa Masuuli Kilimo kuhusu hoja za ukaguzi huu wa ufanisi Kamati imeendelea kusisitiza kuhusu kuhakikisha kutokuwepo kwa mbolea zisizokidhi viwango ili kuepusha hasara kwa wakulima na upotevu wa mapato ya Serikali. Kwa msingi huu Kamati imetoa pendekezo mahsusi la kuondoa changamoto hizo katika sehemu ya tatu ya taarifa hii.

***Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Katika Ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi na Huduma vya Mikoa***

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini (VETA), imepewa jukumu la kukuza, kuratibu, kutoa, kudhibiti na kugharamia Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi pamoja na kusimamia mfumo mzima wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali ilitenga **Shilingi Bilioni 40** kwa ajili ya ujenzi wa vyuo 25 vya ufundi stadi vya wilaya.

**Mheshimiwa Spika,** katika hatua za utekelezaji, Serikali ilitenga **Shilingi Bilioni 28.7** kutoka kwenye fungu la Mpango wa kukabiliana na athari za UVIKO Tanzania (TCRP). Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni 20** zilitengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi (ununuzi wa vifaa vya ujenzi na gharama za ufundi), na kiasi cha **Shilingi Bilioni 8.7** zilitengwa kwa ajili ya usambazaji wa samani katika vyuo vilivyojengwa.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali ilitenga **Shilingi Bilioni 100** kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kutekeleza ujenzi wa vyuo vingine 63 vya ufundi vya wilaya na chuo kimoja cha ufundi stadi na huduma cha Mkoa wa Songwe.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua, inathamini na kupongeza jitihada kubwa na za dhati za **Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan** kwa kukubali kutoa fedha jumla ya **Shilingi Bilioni 100** kwa ajili ya ujenzi wa vyuo hivyo katika wilaya ambazo zilikuwa hazina vyuo vya ufundi stadi pamoja na Mkoa wa Songwe.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa ujenzi huu, Wizara iliamua kutumia utaratibu wa **" Force Account"** ambapo inatumia Taasisi zilizo chini yake kama Washauri Elekezi ambao ni Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia (MUST), Chuo cha Ufundi Arusha (ATC), Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU), na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).Aidha, utekelezaji wa mradi huu umekuwa ukifanyika kwa kutumia Taasisi zilizo chini ya Wizara hii zilizopo katika Wilaya na Mkoa husika ambazo ni Vyuo vya Ualimu 5, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 23 na Ofisi za Udhibiti wa Ubora wa Shule 36.

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi huu wa Kiufundi ulifanyika ili kutathmini thamani ya fedha kwenye ujenzi wa vyuo hivyo na kutoa mapendekezo kwa Serikali ili kufikia lengo la kuwekeza katika vyuo vya ufundi stadi ili kuwapa vijana ujuzi na kufikia mahitaji ya soko la ajira nchini.


**Mheshimiwa Spika,** naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya ukaguzi huo wa kiufundi kama ifuatavyo: -

**Uandaaji wa Makadirio ya Ujenzi Yanayolingana kwa Vyuo Vyote 63 Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi ulibaini kuwa pamoja na ukweli kwamba gharama ya kupata vifaa vya ujenzi kama vile mchanga, mawe na kokoto hutofautiana kutoka eneo moja la ujenzi hadi eneo lingine, Wizara iliandaa makadirio ya gharama za vifaa vya ujenzi na ufundi yanayolingana kwa vyuo vyote 63 vya ufundi stadi vya wilaya. Hivyo makadirio ya mwanzo hayakuwa yamezingatia uwepo wa utofauti wa umbali na jiografia za maeneo husika. Chati Na. 1.1 hapa chini inabainisha utofauti wa gharama za

ununuzi wa vifaa vya ujenzi *(material)* katika vyuo vitatu vilivyotembelewa wakati wa ukaguzi.

**Chati Na. 2.1 : Gharama ya Mchanga, Kokoto na Mawe katika maeneo matatu ya ujenzi yaliyotembelewa**




**Chanzo:** ***Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Kuhusu Ujenzi wa Vyuo vya Ufundi, Januari, 2025.***

**Mheshimiwa Spika,** kama inavyobainishwa kwenye Chati Na.1.1 hapo juu, gharama ya kupata mita ya ujazo ya mawe kwa ajili ya ujenzi kwa chuo cha mafunzo ya ufundi stadi cha wilaya ya Njombe ilikuwa mara mbili zaidi kuliko gharama ya mawe kwenye ujenzi wa chuo cha ufundi stadi cha wilaya ya Bukombe. Aidha, gharama ya mita za ujazo za mchanga kwa chuo cha ufundi stadi cha wilaya ya Njombe ilikuwa mara nne zaidi ya gharama ya kununua mita moja ya ujazo wa mchanga kwa chuo cha ufundi stadi cha wilaya ya Bukombe.

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi ulibaini kuwa utofauti huu haukuakisiwa katika uandaaji wa mahitaji ya ujenzi kabla ya kuanza ujenzi ili kuweza kupata usahihi wa gharama halisi za kila chuo cha ufundi stadi. Taarifa ya ukaguzi ilibainisha kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitoa kiasi sawa cha fedha cha **Shilingi 228,942,380** kwa kila chuo, kwa ajili ya ujenzi wa awamu ya kwanza kwa vyuo vyote 63 vya ufundi stadi vya wilaya.

**Kukosekana kwa Hati za Viwanja kwa Baadhi ya Maeneo ya Vyuo**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika ukaguzi huu ulibaini kuwa ujenzi wa chuo cha ufundi stadi cha wilaya ya Njombe ulianza bila ya kuwa na hati miliki ya kiwanja na kibali cha ujenzi jambo ambalo linaweza kupelekea migogoro kati ya Serikali na wamiliki wa awali wa eneo husika.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia mahojiano na msimamizi wa mradi, ilibainika kuwa, wakati wa utekelezaji wa mradi huo, kulitokea mgogoro wa ardhi kati ya mmiliki wa ardhi na wizara kwa sababu alikuwa hajalipwa fidia. Hata hivyo, baada ya kushauriana na Mkuu wa Wilaya husika, mmiliki alikubali kuruhusu kazi za ujenzi kuendelea.

**Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, ukaguzi ulibaini kuwa ukubwa wa eneo la ujenzi haukuwa umebainishwa ili kuweza kujua kama miundombinu yote iliyokuwa imependekezwa kwa vyuo vya wilaya ingetosheleza katika eneo husika.

**Kutojumuishwa kwa Gharama za Usafirishaji wa Nondo Katika Nyaraka za Zabuni za Wasambazaji na Kusababisha Ongezeko la Gharama ya Shilingi 339,564,800**

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi ulibaini kuwa, nukuu ya bei kutoka kwa mmojawapo wa Mzabuni kwa ajili ya nondo haikuhusisha gharama za usafirishaji. Kutoainishwa kwa gharama za usafirishaji wa nondo, kulipelekea kumtaka muuzaji wakati wa mazungumzo, kuwasilisha bei ya ziada ya usafirishaji, ambayo ilikuwa **Shilingi 323,796,800** kwa vyuo 63 vya ufundi stadi vya wilaya na **Shilingi 15,768,000** kwa chuo cha ufundi stadi na huduma cha Mkoa wa Songwe.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kutojumuishwa kwa gharama za usafiri kwenye zabuni zilizowasilishwa hapo awali, kulisababisha gharama ya ziada ya usafirishaji yenye thamani ya **Shilingi 339,564,800** ambayo haikuwa imebainishwa wakati wa tathmini ya zabuni.

**Kuchelewa Kuwasilishwa Kwa Vifaa vya Ujenzi Kutoka kwa Wazabuni**

**Mheshimiwa Spika,** mapitio ya mkataba wa msambazaji wa vifaa vya ujenzi kwa chuo cha mafunzo ya ufundi stadi cha Mkoa wa Songwe yalibaini kuwa kandarasi ya usambazaji wa saruji, nondo na wavu wa jamvi (BRC) zilitolewa kwa Mbeya Cement LTD na Kamaka LTD. Mkataba huo ulihusisha usambazaji wa mifuko 10,080 ya saruji na vipande 160 vya wavu kwa ajili ya jamvi. Ukaguzi ulibaini kuwa wasambazaji waliopewa zabuni husika hawakuwasilisha saruji na wavu kwa ajili ya jamvi kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** kwa nondo 250 zilizokuwa zikihitajika kwa awamu ya kwanza, mzabuni aliwasilisha nondo 90 tu mnamo tarehe 11 Julai 2023, wakati nondo 160 zilizobaki ziliwasilishwa miezi mitatu baadaye (6 Oktoba 2023). Kutokana na kuchelewa kwa nondo hizo 160 kwa siku 87, maendeleo ya kazi yaliathiriwa kwa sababu mafundi hawakuweza kuendelea na kazi za ujenzi wa majengo ambayo yalihitaji nondo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, mifuko 18,000 ya saruji iliyonunuliwa kutoka kwa kiwanda cha saruji cha Mbeya, ni mifuko 7,800 tu iliyokuwa imefikishwa kwenye maeneo ya ujenzi hadi tarehe 9 Septemba 2023. Hadi kufika tarehe 2 Novemba 2023 kazi za ujenzi zenye kuhitaji saruji zilikuwa zimesimama kwa zaidi ya siku 54 kwenye ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Songwe, kutokana na ukosefu wa saruji.

**Kutokuwepo kwa Vifaa vya Kupambana na Moto Katika Orodha ya Vifaa vya Ujenzi kwa Baadhi ya Vyuo vya Ufundi Stadi**

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi ulibaini kuwa, miundombinu ya usalama dhidi ya moto iliyokuwa imeanishwa katika michoro ya usanifu wa ujenzi iliondolewa kwenye makadirio ya gharama za ujenzi hivyo kupelekea kutokujengwa kwa miundombinu hiyo katika vyuo vyote 25 vya ufundi stadi vilivyojegwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Sababu za kuondolewa kwa miundombinu ya usalama dhidi ya majanga ya moto ilikuwa ni

kupunguza gharama za ujenzi ili kuendana na kiasi cha fedha kilichoonekana kutokidhi gharama za ujenzi kama wangejumuisha ujenzi wa miundombinu hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** kutokuwekwa kwa vifaa vya usalama dhidi ya majanga ya moto kunahatarisha hali ya udhibiti wa majanga ya moto yanayoweza kutokea kwenye vyuo hivyo vya ufundi stadi.

**Ongezeko la Gharama la Shilingi 175,615,952.15 kwa Vyuo 6 vya Ufundi Stadi vya Wilaya Vilivyotembelewa**

**Mheshimiwa Spika,** sehemu ya 2.0 ya andiko la mradi wa ujenzi wa vyuo 25 vya ufundi stadi vya wilaya katika wilaya 25 la Mwaka 2019 ilitaka ujenzi wa vyuo 25 vya ufundi stadi vya wilaya kukamilika mnamo tarehe 30 Juni 2023 kwa kutumia utaratibu wa matumizi ya rasilimali za ndani (Force Account).

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi ulibaini kuchelewa kukamilika kwa vyuo 6 vya ufundi stadi vya wilaya kwa miezi 32. Hadi wakati ukaguzi huu unafanyika, chuo cha ufundi stadi cha wilaya ya Igunga pekee ndicho kilikuwa kimekamilika. Kuchelewa kukamilika kwa vyuo hivi kulitokana na kuchelewa kwa utoaji wa fedha toka Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ambapo fedha hizo zilikuwa zikitolewa kwa awamu.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa vyuo hivyo kulikuwa na ongezeko la gharama kwa vifaa kama vile madirisha ya "*aluminium*" iliyosababishwa na kupanda kwa gharama za vifaa hivyo katika soko. Ilibainika kuwa gharama za madirisha ya aluminium katika majengo ya vyuo vya ufundi stadi vya Wilaya ya Chemba, Bahi, Igunga, Korogwe na Lushoto ziliongezeka kwa **Shilingi 175,615,952.15** kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 2.1.**

**Jedwali Na. 2.1 : Mchanganuo wa Ongezeko la bei za Madirisha.**

| Jina la Mradi | Ukubwa wa Vioo vya Madirisha ($M^2$) | Ongezeko la Gharama /$M^2$ | Ongezeko la Gharama (TZS) |
|---|---|---|---|
| Chuo cha ufundi stadi cha Wilaya ya Bahi | 155 | 115,009.90 | 17,826,534.50 |
| | 129.4 | 108,022.80 | 13,978,150.32 |
| Chuo cha ufundi stadi cha Wilaya ya Chemba | 26.4 | 113,022.80 | 2,983,801.92 |
| | 243 | 108,022.80 | 26,249,540.40 |
| Chuo cha ufundi stadi cha Wilaya ya Korogwe | 737.32 | 62,827.6 1 | 46,324,053.41 |
| Chuo cha ufundi stadi cha Wilaya ya Lushoto | 79.34 | 93,022.80 | 7,380,428.95 |
| Chuo cha ufundi stadi cha Wilaya ya Igunga | 795.75 | 76,498.20 | 60,873,442.65 |
| **Jumla** | | | **175,615,952.15** |

**Chanzo:** ***Uchambuzi wa Kamati kwenye Taarifa za Ukaguzi za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Januari, 2025.***

**Mheshimiwa Spika,** Jedwali Na. 2.1 linaonesha kuwa gharama za aluminium ziliongezeka kwa kiasi cha **Shilingi 175,615,952.15**. Kiasi hiki kingeweza kuokolewa endapo fedha za ujenzi zungetolewa kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 21 Januari, 2025, Kamati ilipata fursa ya kukutana na uongozi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili kujadiliana kwa kina kuhusu hoja za ukaguzi na utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hoja inayohusu ujenzi katika maeneo ambayo hayana hati miliki, Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kwamba, hadi kufikia tarehe 03 Januari, 2025 Wilaya 16 zilikuwa zimeshapata hati miliki ya maeneo yao. Wilaya hizo ni Gairo,

Biharamulo, Mbinga, Iramba, Mwanga, Songwe RVTSC, Sengerema, Chamwino, Liwale na Kisarawe. Wilaya nyingine ni Kakonko, Tanganyika, Kigamboni, Kiteto, Songwe na Kilolo.

**Mheshimiwa Spika,** Afisa Masuuli alifafanua zaidi kuwa, Wilaya 49 bado hazijawasilisha hati miliki hivyo ufuatiliaji unaendelea. Vile vile kwa suala la upatikanaji wa huduma za umeme, maji na barabara, jukumu hilo limekuwa likifanyiwa kazi na halmashauri husika.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu kuchelewa kukamilika kwa mradi kutokana na changamoto ya mtiririko wa fedha, hoja hii pia ilitolewa maelezo na Afisa Masuuli mbele ya Kamati.

Kamati ilifahamishwa kuwa kwa mwaka 2023/2024 Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitenga kiasi cha **Shilingi 95,788,410,341.60** kwaajili ya ujenzi wa vyuo 64 vya wilaya na kimoja cha mkoa wa Songwe. Hata hivyo hadi kufikia tarehe 03 Januari,2025 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 52,015,278,439**.

**Mheshimiwa Spika,** mtiririko wa fedha katika miradi husika, ulikuwa katika awamu tatu ambapo katika awamu ya kwanza ya tarehe 08 Mei, 2023 Wizara ilipokea *exchequer* ya **Shilingi 24,811,243,544.66** ambapo fedha halisi iliyotolewa ilikuwa kiasi cha **Shilingi 24,793,650,687.00** na kiasi cha **Shilingi 17,592,857.66** hakikutolewa. Katika awamu ya pili ya tarehe 06 Oktoba,2023 Wizara ilipokea *exchequer* ya **Shilingi 20,000,000,000.00** ambapo fedha halisi iliyopokelewa ni kiasi cha **Shilingi 17,221,627,752.65** na kiasi cha **Shilingi 2,778,372,247.35** hakikutolewa.

**Mheshimiwa Spika,** awamu ya tatu ya mapokezi ya fedha ilikuwa tarehe 27 Septemba, 2024 ambapo Wizara ilipokea *exchequer* ya **Shilingi 10,000,000,000.00**, ambapo fedha halisi iliyopokelewa ni kiasi **cha Shilingi 6,770,332,818.05** na kiasi cha **Shilingi 3,229,667,181.00** hakijatolewa.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebainisha masuala kadhaa katika mtiririko wa fedha za ujenzi wa vyuo vya VETA kama ifuatavyo:-

a) Katika awamu ya kwanza, utoaji wa fedha ulikuwa karibu na kiwango kilichoidhinishwa (**99.93%**), ikimaanisha kuwa kulikuwa na utolewaji fedha wa kuridhisha;

b) Awamu ya pili Wizara ilipokea (**86.11%)** ya fedha iliyoidhinishwa, ikionyesha pungufu ya kiasi cha fedha kilichotolewa (**Shilingi Bilioni 2.78**); na

c) Awamu ya tatu ilipata kiwango cha chini zaidi cha utoaji wa fedha (**67.70%**), ambapo zaidi ya **Shilingi Bilioni 3.2** hazikutolewa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia mtitiriko na mchanganuo wa utoaji wa fedha kwa mradi wa ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi vya Wilaya na Mkoa, ni dhahiri fedha zimechelewa kutoka kwa wakati. Hali hii imechangia kutokamilika kwa wakati kwa ujenzi na hivyo manufaa ya mradi kutofikiwa kwa wakati kama ilivyokuwa imepangwa. Kamati imetoa mapendekezo ya namna ya kutatua changamoto hii katika sehemu ya tatu ya taarifa hii.

***Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Katika Udhibiti wa Vifaa Tiba Katika Vituo vya Umma vya Kutolea Huduma za Afya***

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO) wa Mwaka 2016 unaohusu Udhibiti wa Vifaa Tiba hatua kwa hatua, Udhibiti wa vifaa Tiba unahusisha shughuli zinazohakikisha kuwa vifaa hivyo ni bora, salama, na vinafanya kazi kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** mchakato huu unajumuisha hatua za uzalishaji, ununuzi, usimikaji, uendeshaji, matengenezo, urekebishaji na utupaji wa vifaa vilivyoisha muda wa matumizi. Aidha udhibiti unaofaa wa vifaa tiba husaidia usimamizi wa vituo

vya kutolea huduma za afya kutunza na kufuatilia vifaa hivyo na kuhakikisha ufanisi na usalama wake unazingatiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Sera ya Afya ya Mwaka 2017 ilisisitiza matumizi ya vifaa vinavyotumia teknolojia ya kisasa katika huduma za uchunguzi. Vifaa hivi ni kama X-ray za kidijitali, Mashine za Uchunguzi wa Mawimbi ya Sauti ya Mwili (MRI) na Vipimo vya Kompyuta (CT scan). Vifaa vinavyotumia teknolojia ya kisasa vinahusishwa na changamoto kama gharama kubwa za ununuzi na uendeshaji, matumizi duni ya vifaa husika na uhaba wa wataalam wenye ujuzi wa kuhudumia vifaa hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mantiki hii mwaka 2020, Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya ilitumia kiasi cha **Shilingi Bilioni 68.7** kununua vifaa tiba kwa vituo vya afya vilivyoko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ishirini na mbili (22) kote nchini kwa ajili ya kutekeleza Sera ya Taifa ya Afya ya Mwaka 2017. Kwa msingi huu ni muhimu kudhibiti ipasavyo vifaa tiba ili kufanikisha matumizi bora ya rasilimali na huhakikisha utoaji wa huduma za afya kwa ubora unaokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la ukaguzi huu lilikuwa ni kutathmini ufanisi wa Wizara ya Afya pamoja na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA) katika kudhibiti vifaa tiba ili kuhakikisha usalama na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya umma vya kutolea huduma za afya nchini. Ukaguzi huu ulijumuisha kipindi cha miaka minne ya fedha yaani kuanzia Mwaka 2019/20 hadi Mwaka 2022/23.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu masuala yaliyobainika katika ukaguzi huo kama ifuatavyo: -

a) Ukaguzi ulibaini uwepo wa baadhi ya vifaa tiba visivyofanya kazi kwa ukamilifu kinyume na malengo yaliyoainishwa kwenye Mpango-Mkakati wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania wa Mwaka 2016/17-2020/21.Mpango huu uliiagiza Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania kuimarisha usimamizi na kuhakikisha ubora, usalama, na ufanisi wa vifaa tiba visivyotumika.

Aidha katika vutuo 18 vya umma vya kutolea huduma za afya vilivyotembelewa, ukaguzi ulibaini kuwa vifaa tiba 135 kati ya 492 sawa na asilimia 27 havikuwa vinafanya kazi kwa ukamilifu. Asilimia kubwa ya vifaa tiba visivyofanya kazi vilibainika katika Kanda ya Kati iliyokuwa na vifaa tiba 37 visivyofanya kazi kati ya 115 sawa na asilimia 32. Aidha uchunguzi ulionesha kuwa vifaa tiba visivyofanya kazi vilitokana na ukosefu wa matengenezo-kinga *(preventive maintanance)* ya vifaa tiba;

b) Ukaguzi ulibaini changamoto katika taratibu za usajili wa vifaa tiba. Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba ilipewa jukumu la kusajili vifaa tiba vinavyotengenezwa ndani na nje ya nchi kabla ya kutumika. Kwa mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2022/23 kulikuwa na vifaa tiba 150 kati ya 209 vilivyosajiliwa sawa na asilimia 72 lakini havikurekodiwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba Tanzania. Aidha ukaguzi ulibaini kuwa kati ya mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2022/23 kulikuwa na ucheleweshaji mkubwa wa usajili wa vifaa tiba. Katika kipindi hicho ni vifaa tiba 5 pekee kati ya 59 vilisajiliwa kwa kufuata muda uliowekwa wa siku 45 hadi 90 za kazi;

c) Ukaguzi ulibaini kuwa kati ya mwaka 2019/20 hadi 2022/23, ripoti za ukaguzi na vyeti vya uingizaji wa vifaa tiba hazikuwa na maelezo ya kina kuhusu ukaguzi uliofanyika kwenye vifaa tiba katika bandari ya kuingilia. Hii ni kinyume na matakwa ya Kanuni ya 56(1) ya Kanuni ya Chakula, Dawa na Vipodozi Tanzania ya udhibiti wa Vifaa tiba ya Mwaka 2015. Aidha vifaa tiba katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya viliingizwa nchini na kufungwa bila ya kufanyiwa uhakiki wa awali juu ya usalama, ubora na ufanisi wake. Sababu kubwa iliyochangia ilikuwa ni ukosefu wa rasilimali watu *(Biomedical Engineers)* wenye ujuzi unaohitajika ili kuhakiki ubora wa vifaa tiba vilivyoagizwa kutoka nje ya nchi;

d) Kutokuwepo taratibu sanifu za uendeshaji (SoP) kwa vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za Afya.Ukaguzi ulibaini kutotumika kwa taratibu sanifu za uendeshaji wa vifaa tiba katika baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya. Hii ilibainika katika vituo vya kutolea huduma za afya vilivyotembelewa ambapo vifaa tiba 263 kati ya 426 viliendeshwa bila uwepo wa taratibu sanifu za uendeshaji wa vifaa tiba;

e) Ukaguzi ulibaini changamoto katika utunzaji wa vifaa tiba katika baadhi ya vituo vya umma. Hali hii ilichangiwa na kutokuwepo mfumo thabiti unaofanya kazi ya ufuatiliaji wa utunzaji na matengenezo kinga katika vituo vya kutolea huduma za afya 13 kati ya 17 sawa na asilimia 76 ya vituo vya kutolea huduma za afya vilivyotembelewa. Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa utekelezaji wa usawazishaji upya (*Calibration and re-calibration*) wa vifaa tiba ulifanyika kwa mashine za 'centrifuge' pekee, vifaa vingine havikufanyiwa urekebishaji; na

f) Ukaguzi ulibaini uondoshaji usiojitosheleza wa vifaa tiba visivyofanya kazi. Kati ya mwaka wa fedha 2019/20 na 2022/23 Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania haikuanzisha wala kupokea maombi ya kuidhinisha uondoshaji wa vifaa tiba badala yake ilipokea ripoti za uondoshaji wa bidhaa nyingine zilizodhibitiwa kama sindano na glavu. Hali hii ilitokana na ukosefu wa miongozo ya uondoshaji wa vifaa tiba ambayo ingesaidia kuanzisha na kusimamia uondoshaji sahihi wa vifaa tiba.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto alizobainisha CAG kwenye taarifa ya ukaguzi huu, CAG alitoa jumla ya mapendekezo 7. Matokeo ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa umebainisha kuwa mapendekezo 3 kati ya 7 yalikuwa katika hatua za utekelezaji unaoridhisha, mapendekezo 3 kati ya 7 yalikuwa katika hatua za awali za utekelezaji na pendekezo 1 halikutekelezwa kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 14 Januari, 2025 Kamati ilikutana na Afisa Masuuli Wizara ya Afya na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA) ili kujadili hoja za ukaguzi huu wa ufanisi ambazo hazijajibiwa kikamilifu na hususan zile ambazo hazijafungwa. Kuhusu uondoshaji wa vifaa tiba Afisa Masuuli TMDA aliifahamisha Kamati kuwa vifaa vikubwa huwa haviteketezwi bali vinabadilishwa baadhi ya vifaa kutokana na mabadiliko ya teknolojia. Naomba kununukuu sehemu ya maelezo ya Ndugu Dkt Adam M. Fimbo, Mkurugenzi Mkuu – TMDA kuhusu hoja hii kama ifuatavyo[7]:-

**Nukuu:**

***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ambayo kidogo imekaa kitaalam sana juu ya vifaa tiba vikubwa kuteketezwa na tumekuwa na mjadala na wenzetu wa CAG kuhusiana na utekeketezaji wa vifaa tiba vikubwa, X rays'machines, citi scans, MRI's ambazo zimefungwa kwenye hospitali kubwa na maalum hapa nchini. Hilo ndio eneo ambalo bado halijatekelezwa kikamilifu kutokana na nature yake tu vifaa hivyo. Kwa hiyo kazi kubwa imefanyika kinachofuata ilikuwa kusimamia matengenezo ya vifaa hivyo na vile ambavyo havifanyi kazi au vimepitwa na wakati au teknolojia yake ni ya zamani basi viweze kuwa disposed au kuondolewa kwenye vituo hivyo…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa hoja ya changamoto ya uondoshaji wa vifaa tiba vikubwa, Afisa Masuuli TMDA aliifahamisha Kamati kuwa utekelezaji wa zoezi la kuondoa vifaa hivyo unachukua muda kwa kuwa unahusisha taasisi mbalimbali za kiserikali. Mathalani, vifaa

[7] Rejea Taarifa Rasmi za Bunge (Majadiliano ya Kamati), Ukurasa wa 22, Kikao cha Pili, Tarehe 14 Januari, 2025.

tiba hivi kama *x rays* machines na *MRI's* vina mionzi hivyo kunahitajika vibali kutoka kwa mamlaka nyingine ili kuviondoa.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu changamoto ya udhibiti wa dawa na vifaa tiba, Afisa masuuli TMDA aliifahamisha Kamati kuwa kwa sasa Mamlaka ina maabara kubwa za kupima ubora wa dawa zinazotumika nchini. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Ndugu Dkt Adam M. Fimbo, Mkurugenzi Mkuu, TMDA akitoa ufafanuzi wa hoja hii kama ifuatavyo[8]:-

**Nukuu:**

***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi inafanyika na mifumo imewekwa. Lakini kazi kubwa inafanyika tuna maabara kubwa ambazo zimepitishwa na WHO zipo pre qualify na ISO Satisfied kwa maana ya upimaji wa dawa. Mheshimiwa Mwenyekiti kwa maana ya mifumo ya udhibiti, ipo inafanya kazi, watumishi tunao inawezekana hawatoshi ni kweli, lakini wapo…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu mfumo wa usajili wa dawa na vifaa tiba, Afisa Masuuli aliifahamisha kamati kuwa kwa sasa wameboresha mfumo wa usajili wa dawa na vifaa tiba ili kuongeza udhibiti wa dawa na vifaa tiba. Wataalam wa TMDA wamekuwa wakifanya tathmini ya maombi ya usajili wa vifaa tiba kutoka wa watengenezaji. Aidha uhakiki hufanyika kwa kuzingatia taarifa za kisayansi kabla ya usajili. Hadi sasa vifaa tiba 2,060 vimesajiliwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hoja iliyohusu kutokukusanya ada kwa huduma zinazotolewa na TMDA, Afisa Masuuli alitoa ufafanuzi kwamba, kwa sasa TMDA haipokei ombi ambalo halijalipiwa ada, hivyo Wakala hauwezi kutoa mtathimini kufanya tathmini ya ombi

---

[8] Rejea Taarifa Rasmi za Bunge (Majadiliano ya Kamati), Ukurasa wa 31. Kikao cha Pili, Tarehe 14 Januari, 2025.

la usajili bila ada kulipwa na ada zote zinalipwa kupitia mfumo wa malipo ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu hoja ya usawazishaji upya *(calibration and re-calibration),* Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kuwa kwa sasa wanajenga kituo katika Hospitali ya Afya ya Akili Mirembe jijini Dodoma kwa ajili ya kufanya usawazishaji upya wa vifaa tiba na kitakuwa pia ni kituo cha mafunzo kwa wataalamu wetu.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupokea maelezo ya kina ya Afisa Masuuli TMDA, Kamati imetoa mapendekezo mahsusi katika sehemu ya tatu ya taarifa hii. Mapendekezo hayo yamezingatia gharama kubwa ambazo Serikali imewekeza katika ununuzi wa vifaa tiba kwa vituo vya afya vya umma. Ni kwa msingi huo, ni muhimu thamani ya fedha za umma ikaonekana katika kuhifadhi, kutumia na kuondosha vifaa hivyo pindi inapotakiwa kufanyika hivyo kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo.

***Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Usimamizi na Ufuatiliaji wa Watoa Huduma za Bima (TIRA)***

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Bima Tanzania imekuwa kwa kiwango kikubwa tangu kuanzishwa kwa soko huria mwaka 1996, ambapo kumekuwa na ongezeko kubwa la watoa huduma za bima hapa nchini. Sekta ya bima inapozidi kukua ni muhimu kuwa na udhibiti na usimamizi toshelevu ili kuweza kudumisha sekta hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Bima Tanzania inasimamiwa na Sheria ya Bima Sura Na. 394, ambayo ilianzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) yenye jukumu la kusimamia sekta ya bima. Lengo la ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi na ufuatiliaji wa watoa huduma za bima ulijikita zaidi katika kutathmini endapo Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania inasimamia na kufuatilia kampuni za bima ipasavyo ili kuhakikisha kuwa Kampuni za Bima zinakidhi matakwa ya kisheria, kiufundi na kifedha.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika ukaguzi huu umebainisha hoja kadhaa ambazo zinatakiwa kufanyiwa kazi na

Serikali ili kuhakikisha thamani halisi ya fedha za umma na maslahi ya wananchi inapatikana katika Sekta ya Bima. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo: -

(a) Ongezeko la asilimia 11 la madai ya bima yanayodaiwa kwa kampuni za bima.Taarifa ya ukaguzi imebainisha kuwepo kwa ukiukwaji wa Sheria ya Bima ya Mwaka 2009 Sura Na.394 katika Kifungu cha 131(1) kinachohitaji kila kampuni ya bima kulipa madai ndani ya siku arobaini toka tarehe ya kusainiwa hati ya malipo (discharge voucher),endapo kampuni itashindwa kulipa madai ndani ya muda huo, inaweza kuomba kwa Kamishna wa Bima kuongezewa muda, na Kamishna anaweza kutoa muda wa ziada usiozidi siku arobaini na tano (45) mpaka madai hayo kukamilika;

(b) Changamoto za kimawasiliano kati ya TIRA, watoa huduma za bima na wateja wa bima. Taarifa ya ukaguzi imebainisha kuwa TIRA haikuweza kuandaa na kutekeleza mpango wa uhamasishaji kuhusu masuala ya bima kupitia mitandao ya kijamii kati ya mwaka wa fedha 2019/20 na 2022/23. Hali hii ilipunguza uelewa wa umma, ushirikishwaji wa wadau, na utoaji wa taarifa za usimamizi wa huduma za bima nchini. Ingawa mpango huo uliidhinishwa Disemba 2023, utekelezaji wake bado ulikuwa katika hatua za awali katika kipindi cha Mwezi Disemba Mwaka 2024;

(c) Dosari katika kusimamia ushughulikiaji wa malalamiko yanayotokana na madai ya bima yasiyolipwa. Taarifa ya ukaguzi imebainisha mapungufu katika usimamizi wa malalamiko yanayotokana na madai yasiyolipwa ya bima. Moja ya changamoto iliyojitokeza ni muingiliano wa majukumu kati ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima na Msuluhishi wa Migogoro ya Bima (TIO);

(d) Ukaguzi pia ulibaini kuwa TIRA ilikuwa ikijihusisha na shughuli za kushughulikia malalamiko nje ya mamlaka yake. Ripoti ya utekelezaji ya TIRA ya mwaka wa fedha

2020/21 ilibainisha kuwa mamlaka hiyo ilipokea na kutatua malalamiko moja kwa moja kutoka kwa wateja wa bima, kinyume na masharti ya vifungu vya 122 na 123 vya Sheria ya Bima na Kanuni ya (6) ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima. Hatua hii imesababisha ucheleweshaji katika kulipa wateja wa bima kwa haki na kwa wakati, na pia kukwamisha uelewa wao wa ofisi inayostahili kushughulikia malalamiko yao; na

(e) Ukaguzi ulibaini pia, Kampuni za Bima hazikuwa zinaweka ipasavyo dhamana inayotakiwa kisheria[9] katika Benki Kuu ya Tanzania.Kanuni hiyo inataka Kampuni za bima kuweka na kudumisha amana ya dhamana *(security deposit*) ya angalau asilimia 50 ya kiwango cha chini cha mtaji uliopo katika Benki Kuu ya Tanzania. Amana hiyo inapaswa kuwa sehemu ya mali kuhusiana na mtaji wa kampuni husika.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hoja zilizobainishwa hapo juu, CAG alitoa mapendekezo kadhaa ya utekelezaji kuhusu ufuatiliaji na usimamizi wa watoa huduma wa Bima. Jumla ya mapendekezo 10 yalitolewa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA). Hadi Kamati inakutana kupitia na kuchambua hoja za ukaguzi huu, mapendekezo ya ukaguzi yalikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 15 Januari,2025 kamati ilikutana na Afisa Masuuli TIRA kwa mahojiano na kupata ufafanuzi kuhusu hoja zilizojitokeza katika ukaguzi huu. Kwa hoja inayohusu ukaguzi wa Kampuni za Bima, Afisa Masuuli TIRA alifafanua kwamba, kampuni za bima zimekuwa zikikaguliwa kwa kutumia njia mbili. Njia kwa ya kwanza ukaguzi hufanyika kwa kupitia na kuchambua taarifa za utendaji "*of sight*". Katika njia hii, Kampuni za Bima huwasilisha ripoti za utendaji kila robo mwaka au wakati wowote wanapohitajika.

---

[9] Rejea Masharti ya Kanuni ya 20 (1) ya Kanuni za Bima za mwaka 2009, kama ilivyorekebishwa mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika,** njia ya pili ukaguzi ni ukaguzi wa kina*"insight"* wa Kampuni za Bima kwa kutumia sampuli *(Sampling)* . Ukaguzi huu ufanyika pale inapobainika uwepo wa viashiria vya Kampuni ya Bima kuwa na viatarishi vya ukwasi unaokubalika kisheria au taarifa za utendaji mbaya wa biashara kutoka kwa mawakala wa Bima.Kupitia kaguzi hizo, hatua stahiki uchukuliwa kwa kuzingatia matokeo ya ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, hoja inayohusu ukaguzi wa Kampuni za Bima iliendelea kutolewa ufafanuzi na Afisa Masuuli TIRA,Ndugu Dkt Baghayo A. Saqware, naomba kunukuu sehemu ya maelezo yake kwa Kamati kama ifuatavyo[10]:-

**Nukuu:**

***"…katika usimamizi wa sekta ya bima unaendelea vizuri na tunatumia vigezo vya standard ya kimataifa kupima ufanisi, wanaita insurance core – principles ambazo zinatengenezwa na taasisi za kimataifa na unapima kwa kuangalia utendaji kwa maana ya soko linaendeleaje? Ukuaji wa soko, ukuaji wa mitaji, ajira na ukwasi wa makampuni. Kwa takribani miaka 3 sasa soko letu kwa maana ya watoa huduma wamekuwa wakiongezeka kwa 34%, soko letu limekuwa likitoa ajira rasmi zaidi ya 5000 kwa mwaka 2023. Kwa upande wa ukwasi nao umeongezeka kwa makampuni yetu kwa maana ya asset kwa zaidi ya 11%…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimwa Spika,** katika kujibu hoja nyingine ya ukaguzi inayohusu ukwasi wa makampuni ya bima kuwa chini ya kiwango cha kisheria, Afisa Masuuli aliifahamisha kamati kuwa ni sahihi

[10] Rejea Taarifa Rasmi za Bunge (Majadiliano ya Kamati), Ukurasa wa 43, Kikao cha Tatu, Tarehe 15 januari, 2025.

kuna Kampuni za Bima 6 ambazo ukwasi wake ulikuwa chini ya kiwango kinachotakiwa kisheria kwa maana ya **Shilingi Bilioni 2.5** kwa Kampuni ya Bima ya kawaida na **Shilingi Bilioni 9**, kwa Kampuni ya Bima mtawanyo.

**Mheshimiwa Spika,** Afisa Masuuli TIRA alitoa maelezo kuwa, hatua zilizochukuliwa kwa watoa huduma hao kwa sasa ni pamoja na kufanya mawasiliano nao (*business engagement)* za kuwaeleza kuwa wana mapungufu na wamejipanga vipi kukidhi matakwa ya kisheria. Endapo hatua ya kwanza itakuwa haina mafanikio, hatua ya pili ambayo TIRA inaweza kuchukua ni kuyaweka makampuni husika chini ya usimamizi, ambapo TIRA inakuwa na uwezo wa kusimamia shughuli za kampuni husika moja kwa moja.

**Mheshimiwa Spika,** vilvile Afisa Masuuli TIRA, aliifahamisha Kamati kuwa, hatua ya mwisho kwa mujibu wa sheria ambayo TIRA inaweza kuchukua dhidi ya kampuni za bima zenye ukwasi mdogo na zilizokiuka taratibu ni kufunga kampuni endapo TIRA itajiridhisha kuwa makampuni hayo yana changamoto za ukwasi na za kiutendaji kwa mujibu wa sheria.

***Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Katika Ujenzi wa Kivuko Kipya cha Nyamisati , MV Kilindoni na Ukarabati wa MV Kazi na MV Nyerere***

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) ilifadhili ujenzi wa vivuko mbalimbali, kikiwemo kivuko cha MV Ukara II - Hapa Kazi Tu kilichogharimu **Shilingi Bilioni 4.2,** kinachofanya kazi kati ya Bugolora na visiwa vya Ukara.

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulihusisha pia kivuko cha Chato kilichogharimu **Shilingi Bilioni 3.12,** kinacho hudumia Nkome hadi Mharamba na visiwa vya karibu vya Senga, Bukondo, na Izumacheli). Taarifa ya ukaguzi imebainisha kuwa, kiasi cha **Shilingi Bilioni 5.3** zilitolewa kwa ajili ya kujenga kivuko cha Kilindoni Hapa Kazi Tu kwa ajili ya kuhudumia Kisiwa cha Mafia na kijiji cha Nyamisati mkoani Pwani, ambacho kingeanza kutumika mwezi Novemba 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango Mkakati wa TEMESA kwa mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2020/21 ulilenga kuimarisha huduma za kihandisi na miundombinu inayohusiana na vivuko ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa vivuko 8 vipya hadi kufikia Mwezi Juni 2021, ukarabati wa vivuko 12 na sehemu ya maegesho ya vivuko (ramps) 7 zilizokarabatiwa au kupanuliwa kufikia Mwezi Juni 2021. Aidha, lengo hili lilisisitiza umuhimu wa kushughulikia uboreshaji wa huduma za vivuko. Mradi huu ulizingatia hitaji la ukarabati mkubwa kwa baadhi ya vivuko vilivyopo na upatikanaji wa vivuko vipya.

**Mheshimwa Spika,** lengo la jumla la ukaguzi wa kiufundi lilikuwa kutathmini kama Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) inasimamia ipasavyo ujenzi na ukarabati wa vivuko nchini ili kuhakikisha uwepo wa thamani ya fedha. Malengo mahususi ya ukaguzi yalikuwa ni kutathmini iwapo: -

a) Uanzishaji na upangaji wa ujenzi na ukarabati wa vivuko ulifanyika ipasavyo ili kuwezesha kufikia malengo yaliyowekwa;

b) Usanifu wa vivuko ulifanyika kikamilifu ili kufikia malengo yaliyowekwa;

c) Ununuzi wa wakandarasi, washauri elekezi, bidhaa na huduma ulifanyika kwa mujibu wa sheria na kanuni za manunuzi husika;

d) Usimamizi wa mikataba (muda, gharama, ubora, mawanda, na maswala mengine ya kimkataba kama vile matumizi ya fedha za mradi, mazingira, usimamizi wa kijamii, usalama na afya, na suala la rasilimali watu) katika ujenzi na/au ukarabati wa vivuko ulifanywa kwa ufanisi kulingana na masharti na vigezo vya mikataba, sheria na kanuni za nchi; na

e) Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC) linaidhinisha vyema michoro iliyopendekezwa ya vivuko na kukagua ubora wa kazi iliyofanywa katika ujenzi na ukarabati wa kivuko.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kufafanua malengo mahsusi ya ukaguzi huu, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu masuala yaliyobainika katika ukaguzi huo kwa kuyagawanya katika sehemu kuu nne (4) kwa kuzingatia miradi iliyokaguliwa kama ifuatavyo:-

**Matokeo ya Ukaguzi wa Kivuko Kipya cha Nyamisati**

**Mheshimiwa Spika,** masuala muhimu yaliyobainika katika ukaguzi wa kivuko kipya cha Nyamisati ni kama ifuatavyo: -

(a) TEMESA ilianza ujenzi wa kivuko kipya bila kuwa na Taarifa ya Dhana ya Mradi *(Concept note)*. Taarifa ya ukaguzi imebainisha kwamba, TEMESA haikuandaa muhtasari wa kina wa dhana ya mradi kwa sababu ya ukosefu wa uzoefu wa umuhimu wa kuandaa na kuwasilisha dhana ya mradi. Kutokuwepo kwa dhana ya mradi kunaweza kuwa na athari kadhaa, kwa mfano, malengo ya mradi, upeo, na mantiki haziwezi kufafanuliwa kwa uwazi. Hii inaweza kusababisha mkanganyiko na kutoelewana miongoni mwa wadau kuhusu madhumuni ya mradi na matokeo yanayotarajiwa;

(b) Ukaguzi ulibaini kutofanyika kwa kina upembuzi yakinifu wa mradi. Hali hii kwa kiasi kikubwa ilisababishwa na kukosekana kwa wataalam wa kutosha wa ndani wenye uzoefu wa kujenga vivuko vipya kama vile Wahandisi na Wasanifu wa Vivuko;

(c) Mapitio ya Maelezo ya Kiufundi kwenye makadirio ya uhandisi yaliyowasilishwa na mkandarasi yalionesha nukuu ya manunuzi ya injini kuu mbili (2) zenye thamani ya **Dola za Marekani 180,000** zitakazonunuliwa kutoka Korea. Aidha, katika nyaraka hizohizo, uchambuzi ulibaini uwepo wa nukuu ya ununuzi wa injini nyingine mbili kama vipuri zenye thamani sawa kwa **Dola za Marekani 180,000,** Hali hii ilisababisha ongezeko la gharama ya **Dola za Marekani 180,000** kwenye mkataba

wa ununuzi wa kivuko kipya. Kiasi hicho cha fedha kingeweza kutumika kwa madhumuni mengine;

(d) Ukaguzi ulibaini kuwa Wakala wa Ufundi na Umeme alitangaza zabuni na kuagiza wazabuni kuwasilisha zabuni zao bila kuwa na makadirio ya kina ya mhandisi. Kukosekana kwa makadirio ya awali ya mhandisi wakati wa zabuni kulisababisha tofauti ya **Shilingi Bilioni 3.199**, sawa na asilimia 50.78 kutoka makadirio ya awali ya gharama ya bajeti ya **Shilingi Bilioni 6.3** iliyopendekezwa na Idara Tumizi (user department) dhidi ya zabuni iliyowasilishwa ya **Shilingi Bilioni 9.499**;

(e) TEMESA haikufanya uhakiki wa kina *(Due-diligence)* kabla ya kusaini mkataba wa ujenzi wa kivuko kipya. Barua kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya tarehe 9 Mei 2022 yenye kumbukumbu Na. CBD.14/385/18, kipengele Na. 18 ilielekeza kwamba TEMESA ilitakiwa kufanya uhakiki *(Due – diligence)* kabla ya kusaini mkataba. Hata hivyo, katika kupitia jalada la barua za utekelezaji wa mkataba wa kivuko kipya, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa Wakala wa Ufundi na Umeme hakufanya uhakiki kwa mujibu wa sheria na kanuni za manunuzi ya umma;

(f) Ukaguzi ulibaini dosari kwa mkandarasi kutokuwa na mitambo na vifaa vya kutosha kwenye eneo la ujenzi wa vivuko. Ukaguzi ulibaini kuwa mkandarasi alikuwa katika hatua ya awali ya maandalizi ya eneo la ujenzi wa kivuko na hakukuwa na ushahidi kwamba mkandarasi alitoa taarifa kwa Wakala wa Ufundi na Umeme kuhusu mabadiliko ya eneo la ujenzi; na

(g) TEMESA ilichelewa kuwasilisha kwa TASAC michoro na muundo wa vivuko kwa ajili ya idhini kwa zaidi ya siku 105.

**Matokeo ya Ukaguzi wa Kivuko cha MV Kilindoni**

**Mheshimiwa Spika**, masuala muhimu yaliyobainika katika ukaguzi wa kivuko cha MV Kilindoni ni kama ifuatavyo: -

a) Taarifa ya ukaguzi imebainisha kuwa Wakala wa Ufundi na Umeme hakufanya tathmini ya kutosha ya mahitaji ya huduma za kivuko kwenye njia iliyopendekezwa. Tathmini hiyo ilitakiwa ili kubainisha ipasavyo masuala ya kiufundi ya ujenzi wa kivuko, kama vile muundo, vifaa, na mbinu za ujenzi. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa hapakufanyika uchambuzi wa kifedha wa gharama za mradi, gharama za uendeshaji, makadirio ya mapato na vyanzo vya fedha;

b) Ukaguzi haukupata ushahidi wowote kuwa Wakala wa Ufundi na Umeme ulipitia usanifu wa awali wa mradi wa MV Kilindoni au kuuwasilisha kwa Shirika la Uwakala wa Meli ili kuidhinishwa kinyume na Kanuni ya 20 (2) ya Usafirishaji wa Majini (Usalama wa Meli Ndogo, Meli za Mizigo, kupitia na Ukaguzi wa Meli zinazojihusisha na Safari za Ndani na Pwani, Maji ya ndani), 2004 inayoelekeza Wakala wa Ufundi na Umeme kuwasilisha kwa mamlaka kwa ajili ya kuidhinishiwa michoro inayoonesha vifaa na muundo wa meli;

c) Ukaguzi ulibaini kuwa Wakala wa Ufundi na Umeme haikuhusisha huduma ya mshauri elekezi na wataalamu wengine katika kusimamia mradi wa MV Kilindoni;

d) Ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa Ufundi na Umeme ilishindwa kuandaa Makadirio ya Gharama ya Uhandisi *(Engineering estimates)* kabla ya kutangaza zabuni za mradi wa ujenzi wa kivuko cha MV Kilindoni. Hali hii inaweza kuathiri gharama za mradi wakati wa utekelezaji; na

e) Mradi huo ulikumbwa na ucheleweshaji kwa miezi tisa, na haukukamilika kama ilivyotarajiwa kufikia Mwezi

Machi 2020. Ucheleweshaji huo ulitokana na changamoto kama vile athari za janga la COVID-19, mvua zilizokuwa zinaendelea; na

f) Dosari za kiusimamizi katika kuhakikisha mkandarasi anamaliza kazi kwa muda uliopangwa kimkataba.

**Matokeo ya Ukaguzi Ukarabati wa Kivuko cha MV Nyerere**

**Mheshimiwa Spika,** masuala muhimu yaliyobainika katika ukaguzi wa kivuko cha MV Nyerere ni kama ifuatavyo: -

a) Ukaguzi ulibaini kuwa Wakala wa Ufundi na Umeme hakufanya tathmini ya hali ya kivuko, ambayo ni muhimu kwa upembuzi yakinifu kabla ya utekelezaji wa mradi. Kutokuwepo kwa tathmini ya hali ya kivuko kulisababisha maandalizi ya nukuu za makadirio ya ukubwa wa kazi na bei (BoQs) kuwa na maelezo yasiyo na kina na kuwa na kazi zilizojirudia;

b) Ukaguzi ulibaini kasoro katika usimamizi wa Wakala wa Ufundi na Umeme kuhusu mradi wa ukarabati wa MV Nyerere katika hatua ya usanifu. Mfano, Wakala wa Ufundi na Umeme hakupitia mabadiliko ya usanifu yaliyofanywa na mkandarasi, wala hakupeleka michoro iliyosanifiwa na mkandarasi kwa Shirika la Uwakala wa Meli kwa ajili ya kuidhinishwa;

c) Ukaguzi ulibaini baadhi ya vipengele kwenye Nukuu za Makadirio ya Ukubwa wa Kazi hazikuwa na maelekezo ya kina, vizio vya vipimo vyenye mapungufu na kuwekwa kwa bei ya jumla ya kazi (lumpsum) ambazo hazikuwa zimeainishwa kwa kina kama inavyooneshwa kwenye jedwali Na.1 kwa maelezo ya kina;

d) Ukaguzi ulibaini kuwa Wakala wa Ufundi na Umeme ulishindwa kuhakikisha dhamana mpya ya utendaji kazi (performance bond) kufuatia kuongezwa kwa tarehe ya kukamilika kwa mradi. Hii ni kunyume na Kifungu cha 9.1

cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC)[11] ambacho kilimtaka mkandarasi kutoa dhamana ya utendaji kazi sawa na asilimia 15 ya bei ya mkataba ndani ya siku 14 baada ya kupokea taarifa ya tuzo ya mkataba; na

e) **Shilingi 218,552,000** kama malipo ya ufundi iliwekwa kimakosa katika zabuni hii. Pamoja na dosari ya kuhusisha gharama hizo, ukaguzi ulibaini kwamba TEMESA ilishindwa kutoza kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa ada za malipo ya wafanyakazi kwa mkandarasi yenye gharama ya **Shilingi 218,552,000** na kusababisha kutokukusanywa mapato ya Serikali ya kiasi cha **Shilingi 39,339,360**.

**Matokeo ya Ukaguzi wa Ukarabati wa Kivuko cha MV Kazi**

**Mheshimiwa Spika**, masuala muhimu yaliyobainika katika ukaguzi wa kivuko cha MV Kazi ni kama ifuatavyo: -

a) Ukaguzi ulibaini kuwa mradi wa ukarabati wa MV Kazi ulifanyika bila uchunguzi wa hali ya kivuko ambapo uchunguzi huo ungejumuisha ukaguzi wa mwili wa chombo na majaribio ya vifaa. Ukaguzi huu ungeweza kusaidia kubaini kasoro ambazo ni muhimu katika kutathmini gharama za mradi kabla ya majadiliano. Kutokana na hali hiyo, hakukuwa na maandalizi ya kutosha ya nyaraka za zabuni, na kusababisha kuongezeka kwa kazi kama vile kuondoa bati la chini karibu na maeneo ya pump jet kwa takriban mita moja pande zote. Pia kulisababisha kuongezeka kwa gharama na muda wakati wa ukarabati wa kivuko;

b) Kwa kuzingatia tathmini iliyofanyika, ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo kuhusiana na usanifu wa maeneo ya kivuko;

   (i) Mfumo wa chumba cha nahodha ulikuwa unategemea hewa kupitia kufungua madirisha

[11] General Conditions of a Contract (GCC).

hivyo kusababisha mvua kuingia. Hata hivyo, katika ripoti za ukaguzi zilizofanyika tarehe 8 Novemba 2018, TEMESA ilitatua tatizo hili kwa kufunga mfumo wa viyoyozi;

(ii) Vifuta maji (Wipers) vilisafisha sehemu ndogo ya kioo kwa sababu hazikuwekwa katikati ya kioo;

(iii) Redio ya mawasiliano ya masafa ya juu sana (VHF) haikuwa inafanya kazi; na

(iv) Kiyoyozi kilikuwa kidogo hivyo hakikuhakikisha uingizaji hewa wa kutosha kwenye chumba cha nahodha.

c) Wakala wa Ufundi na Umeme haikujumuisha wahandisi wa vivuko katika timu ya majadiliano, jambo ambalo lingesaidia kusimamia masuala ya kiufundi ya baharini. Hali hii ilisababisha vikwazo vya gharama na ubora duni wa vifaa na vifaa vipya vilivyohitajika;

d) Kuvuja kwa mafuta ya injini mpya zilizobadilishwa. Ukaguzi ulibaini kuwa Wakala wa Ufundi na Umeme ulibadilisha injini hizi licha ya kuwa zilikuwa zimewekwa mwaka 2017, bila maelezo ya sababu za kubadilishwa kwake mapema. Injini za dizeli zinazotumika kwenye chombo cha baharini, ikiwa zitahudumiwa ipasavyo, hudumu hadi miaka 20. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa injini mpya za MV Kazi zilizofungwa zilikuwa zinavuja mafuta na changamoto nyingine za kiufundi, ikiwemo injini moja na gia boksi ya pampu jeti ya injini nyingine ambazo hazikuwa zinafanya kazi; na

e) Ukaguzi pia ulibaini kuwa waendeshaji walishindwa kufuata ratiba ya matengenezo na TEMESA haikuwa na miongozo ya uendeshaji ya injini. Hatua hii ilikuwa kinyume na masharti ya mkataba.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hoja za ukaguzi zilizobainishwa hapo juu, CAG alitoa mapendekezo kadhaa ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa vivuko vya MV kilindoni na kivuko kipya cha Nyamisati, na ukarabati wa vivuko vya MV Nyerere na MV Kazi. Jumla ya mapendekezo 11 yalitolewa ambapo mapendekezo 7 yalitolewa na kuelekezwa kwa Mamlaka ya ufundi na Umeme (TEMESA) na mapendekezo 4 yalielekezwa kwa Wizara ya Ujenzi.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 16 Januari,2025 kamati ilikutana na Afisa Masuuli, Wizara ya Uchukuzi ambapo alitoa ufafanuzi kuhusu hoja za ukaguzi. Afisa Masuuli alikiri kupokea hoja za ukaguzi na kuanza kuzifanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuandaa miongozo muhimu inayohusu ujenzi na ukarabati wa vivuko. Mathalani, TASAC imepitia na kuboresha Utaratibu Na. F-MSE-RSI-004-ASD wa kutoa idhini ya michoro ya Meli katika hatua ya ujenzi na ukarabati ili mchakato wa kupitia michoro na kutoa idhini ukamilike ndani ya siku 30. Vilevile TASAC imeendelea na awamu ya pili ya uundaji wa Mfumo wa Menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti Majini (Maritime Administration Management System, MAMS) ambao unajumuisha udhibiti wa ujenzi na ukarabati wa meli.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa TEMESA kuhusu hoja ya kuanza miradi bila ya ya kuwa na Dhana ya Mradi, Kamati ilifahamishwa kwamba, ili kuwa na Dhana ya Miradi *(Project Concept)* inayokidhi mahitaji, pendekezo hili lipo katika hatua ya awali ya utekelezaji. Kwa sasa TEMESA inamtumia mtaalam elekezi, Taasisi ya Bahari Dar es salaam (Dar es salaam Maritime Institute- DMI) kwa kushirikiana na wataalam wa ndani kufanya kazi hizi za dhana ya mradi" na utafiti wa kina wa uwezekano wa mradi kufanyika "Feasibility study". Kwa mujibu wa Afisa Masuuli TEMESA, utekelezaji wa dhana za miradi utaanza kwa miradi mipya kwani tangu ukaguzi ufanyike hadi sasa hakuna mradi mpya wa ujenzi wa vivuko vipya uliotekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kuchelewa kukamilika kwa miradi, mkataba pekee ambao utekelezaji wake ulileta changamoto ni wa Kivuko kipya cha Mafia - Nyamisati, ambapo mmoja wa Mbia K.L Heavy Industries ya KOREA aliyeingia ubia na

Dar es Salaam Mechant Group (DMG) ambaye ni Mtanzania kutofautiana na hivyo kusababisha mradi kutokutekelezwa kama ilivyopangwa kwenye hatua za awali. Hata hivyo Wakala alibaini changamoto hiyo na kuingilia kati kwa kumuelekeza mkandarasi mzawa M/s DMG kutimiza matakwa ya kimkataba vinginevyo mkataba uvunjwe. Mkandarasi M/s DMG alitimiza masharti na hivi sasa mradi unaendelea na mkandarasi ameshawasilisha hati ya malipo Na. 1 (IPC No. 1).

**Mheshimiwa Spika**, kwa hoja iliyohusu michoro kutokupitiwa kwa wakati, Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kuwa ni kweli michoro ilipitishwa kwa muda zaidi ya ule uliowekwa na sababu kubwa ilikuwa ni upungufu wa wataalamu, kulikuwa na mtaalamu mmoja (01) tu. Aidha kuhusu changamoto ya usanifu wa mradi Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kuwa wakati wanapewa kazi ya kusimamia ujenzi wa vivuko baadhi ya vivuko kama MV Kilindoni ulikuwa umeanza.


***Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Uwezeshaji wa Wachimbaji Wadogo wa Madini***

**Mheshimiwa Spika,** shughuli za uchimbaji mdogo wa madini nchini zinachangia ubora wa maisha na ni chanzo muhimu cha mapato katika jamii ya kitanzania. Zaidi ya watu milioni 1.2 wameajiriwa moja kwa moja katika sekta ya uchimbaji mdogo wa madini, ambao ni zaidi ya asilimia 90 ya ajira zote katika sekta ya madini, na hivyo kusaidia watu takribani milioni 7.2 kuendesha maisha yao ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa za ukusanyaji wa mapato kutoka Tume ya Madini, katika mwaka wa fedha 2022/23, sekta ya uchimbaji mdogo wa madini ilichangia takriban asilimia 40 ya mapato kutoka sekta ya madini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla hali ya ukusanyaji wa maduhuli katika sekta ya uchimbaji mdogo wa madini imekuwa ikiongezeka kutoka **Shilingi Bilioni 62** mwaka 2018/19 hadi **Shilingi Bilioni 220** mwaka 2022/23, kama inavyooneshwa katika **Chati Na. 2.2** hapa chini.

**Chati Na. 2.2 : Hali ya Makusanyo ya Maduhuli Katika Sekta ya Uchimbaji Mdogo wa Madini**




***Chanzo: Uchambuzi wa Taaarifa za Makusanyo ya Maduhuli kutoka Tume ya Madini.***

**Mheshimiwa Spika**, ongezeko la mapato katika sekta ndogo ya madini linaloonekana katika Chati Na. 2.2 hapo juu lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na uimarishwaji na uanzishwaji wa masoko ya madini na vituo vidogo vya kufanyia biashara ya madini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa za Tume ya Madini, uzalishaji wa madini kwa ujumla ulionekana kuongeza, isipokuwa madini ya Almasi kama inaovyooneshwa katika Chati Na. 2.3 hapa chini.

**Chati Na. 2.3 : Uzalishaji wa Madini Mbalimbali Katika sekta Ndogo ya Uchimbaji wa Madini**




***Chanzo: Uchambuzi wa Taaarifa za Makusanyo ya Maduhuli kutoka Tume ya Madini.***

**Mheshimiwa Spika,** kama inavyoonekana katika Chati Na. 2.3 hapo juu, hali ya uchimbaji mdogo wa madini imekuwa ikiimarika kwa madini yote kama makaa ya mawe, chumvi na madini ya ujenzi. Hata hivyo hali ya uzalishaji wa madini ya almasi ulishuka kiasi kutokana na kuanguka kwa bei ya madini hayo katika soko la dunia.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kulifahamisha Bunge lako Tukufu takwimu hizo muhimu kuhusu sekta ya uchimbaji mdogo wa madini, naomba kubainisha kuwa, lengo kuu la ukaguzi huu wa ufanisi lilikuwa ni kutathmini iwapo Wizara ya Madini kupitia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) pamoja na Tume ya Madini imewawezesha ipasavyo wachimbaji wadogo wa madini ili kuwezesha ukuaji wa sekta ya uchimbaji mdogo wa madini nchini na kuchangia mapato ya Serikali ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** malengo mahsusi ya ukaguzi huu yalikuwa ni kutathmini ikiwa Wizara ya Madini kupitia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Tume ya Madini wametekeleza masuala yafuatayo:-

a) Wachimbaji wadogo wa madini wamewezeshwa ipasavyo kutekeleza shughuli zao;

b) Iwapo Serikali imekuwa ikitenga na kuwezesha matumizi bora ya rasilimali ili kusaidia wachimbaji wadogo wa madini;

c) Iwapo kuna uratibu mzuri katika kuwawezesha wachimbaji wadogo wa madini; na

d) Iwapo Serikali imekuwa ikifanya ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara ya utendaji wa wachimbaji wadogo wa madini.

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi uliangazia shughuli za uchimbaji wa madini ya aina tofauti kama; dhahabu, vito vya thamani (almasi), makaa ya mawe, madini ya viwandani (chumvi) pamoja na madini ya ujenzi.

**Mheshimiwa Spika,**katika ukusanyaji wa taarifa, ukaguzi ulitembelea Mikoa ya Geita kwaajili ya madini ya dhahabu, Shinyanga kwaajili ya madini ya almasi, Ruvuma kwaajili ya madini ya makaa ya mawe na Lindi kwaajili ya madini ya chumvi. Vile vile, ukaguzi ulihusisha taarifa za miaka mitano ya fedha, kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** masuala muhimu yaliyobainika katika ukaguzi huo yanayohusu moja kwa moja mapato ya Serikali ni kama ifuatavyo:-

a) Mapitio ya Taarifa za leseni za uchimbaji mdogo, Mipango Mkakati ya Shirika la Madini la Taifa,na ripoti za utendaji wa mwaka, kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2022/23 zilibaini kuwa wachimbaji wadogo hawakupata taarifa za kutosha za kijiolojia na uwepo wa madini (mashapo). Hii ilithibitishwa na uwepo wa idadi ndogo ya wachimbaji wadogo waliopewa taarifa hizi kupitia Shirika la Madini la Taifa pamoja na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania;

b) Mapitio ya ripoti ya utendaji wa vituo vya mfano vya wachimbaji wadogo kuanzia Julai 2021 hadi Juni 2022 yalibaini kuwa asilimia 5 tu ya wachimbaji wadogo wa madini waliwezeshwa kupitia vituo hivyo. Mathalani, uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya ukaguzi ulibaini kuwa, wachimbaji wadogo 48 tu, sawa na asilimia moja (1) ya leseni zote zilizotolewa mwaka 2021/22, walipata huduma za uchenjuaji. Sanjari na hilo, ni wachimbaji 233 tu, sawa na asilimia nne (4) ya leseni zote zilizotolewa mwaka wa fedha 2021/22, walipata huduma ya uchimbaji wa madini kupitia vituo hivyo;

c) Ukaguzi ulibaini kupitia ripoti za utendaji za kila mwaka kutoka Wizara ya Madini kuwa kulikuwa na changamoto ya upatikanaji wa mikopo na ruzuku kwa wachimbaji wadogo wa madini kutoka taasisi za fedha kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2022/23.Hali hii ilichangiwa na

masuala kadhaa, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa vigezo vya kukopesheka na wachimbaji wadogo kutopata elimu ya masuala ya kifedha;

d) Ukaguzi ulibaini kuwa mahitaji na vipaumbele vya wachimbaji wadogo hayakuhusishwa kikamilifu wakati wa maandalizi ya mipango ya mwaka ya Wizara na bajeti zake. Ilibainika kuwa Mpango Mkakati wa Wizara ya Madini ulipendekeza kutoa zana za uchimbaji zenye gharama nafuu kwa wachimbaji wadogo. Hata hivyo, mpango huu haukuonekana katika Mipango ya Wizara ya Utekelezaji ya Mwaka, na hakukuwa na fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji;

e) Ukaguzi ulibaini utengaji wa rasilimali usiojitosheleza. Hali hii ilithibitishwa na ukosefu wa uwezeshaji wa kifedha pamoja na ukosefu wa wataalam wa kutosha kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji wadogo. Athari kubwa ya suala hili ni mapungufu katika kutimiza wajibu wa kuwawezesha wachimbaji wadogo wa madini. Vilevile, suala hili lilichangia ukosefu wa mtaji wa kununua vifaa bora vya uchimbaji hivyo kupunguza kasi ya maendeleo ya sekta ndogo ya madini nchini; na

f) Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na changamoto ya tathmini na ya uwezeshaji wa wachimbaji wadogo, kama ilivyothibitishwa na ukosefu wa mfumo wa utoaji wa taarifa za usimamizi wa wachimbaji wadogo. Mapungufu hayo yalitokana na kutokuwepo kwa mfumo madhubuti wa ufuatiliaji na tathmini katika Wizara ya Madini, Shirika la Madini la Taifa na Tume ya Madini.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kuchambua kwa kina matokeo ya ukaguzi huo, Kamati ilijielekeza kuangalia hali halisi ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi. Matokeo ya uhakiki wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa yalibainisha kuwa, kati ya mapendekezo tisa (9), pendekezo moja (1) lilitekelezwa kikamilifu, mapendekezo saba (7) yalikuwa katika hatua nzuri za

utekelezaji na pendekezo moja (1) lilikuwa halijaanza kutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Afisa Masuuli Wizara ya Madini ili kupata maelezo ya Serikali kuhusu utekelezaji wa hoja za ukaguzi huu wa ufanisi. Kwa hoja inayohusu wachimbaji wadogo kutokuwa na taarifa za kijiolojia kuhusu mashapo ya madini, Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kuwa, katika kuhakikisha pungufu hili linafanyiwa kazi, Wizara ya Madini kupitia Shirika la Madini la Taifa, imeweza kununua mitambo 15 ya uchunguzi wa kijiolojia kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

**Mheshimiwa Spika,** Afisa Masuuli aliendelea kufafanua kuwa, hadi sasa mitambo mitano (5) inafanya kazi. Aidha, kati ya kipindi cha tarehe 4 Disemba 2023 hadi kufikia Novemba 2024 mitambo hiyo imewafikia wachimbaji wadogo 23 na kuchoronga mita 6,929.33 katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, mitambo mingine kumi (10) tayari ipo bandarini na inatarajia kusambazwa kwenye maeneo mbalimbali ya wachimbaji wadogo hivi karibuni.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu upungufu wa vifaa vya uchimbaji na uchenjuaji wa madini, Kamati ilifahamishwa kuwa, kwa mwaka wa fedha 2023/24 Shirika la Madini la Taifa limekamilisha upanuzi wa kituo cha mfano cha Lwamgasa kutoka kuchenjua madini (mbale) tani 9 kwa siku hadi tani 30 kwa siku. Maboresho haya yamehusisha pia ujenzi wa mitambo ya uchenjuaji (*Carbon in Pulp, CIP)* na *(Elution Plant)* pamoja na ukarabati wa upondaji na usagaji wa mawe. Aidha, Shirika limeendelea na usimamizi wa vituo vya mfano vya Itumbi na Katente.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hoja inayohusu wachimbaji wadogo kuwezeshwa kupata mikopo, maelezo yaliyotolewa yanabainisha kuwa hoja hii bado haijafanyiwa kazi ipasavyo. Kwa upande wa ufuatiliaji na tathmini, Serikali kupitia Wizara ya Madini imeanzisha kitengo rasmi cha Ufuatiliaji na Tathmini na hivyo sasa kimeanza mchakato wa kushirikisha Taasisi zilizopo chini ya Wizara kwa kuwapatia majukumu maafisa wa Taasisi ambao watakuwa wanaratibu shughuli za Tathmini na Ufuatiliaji na kuripoti Wizarani.

**Mheshimiwa Spika,** baaada ya majadiliano ya kina ya Kamati na Wizara ya Madini na Taasisi zake, na kwa kuzingatia matokeo ya ukaguzi huu wa ufanisi, Kamati imeandaa mapendekezo mahsusi katika sehemu ya tatu ya taarifa hii ambayo kimsingi yatasaidia kuboresha shughuli za uchimbaji mdogo ili ziwe na tija zaidi na ufanisi kwa mapato ya Serikali na jamii kwa ujumla.

***Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Katika Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi***

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoongoza duniani katika uzalishaji wa samaki, ikiwa na uzalishaji wa wastani wa tani 395,006 kwa mwaka. Sekta ya uvuvi imekuwa ikikua kwa asilimia 1.5 kwa mwaka na inachangia kwa kiasi kikubwa usalama wa chakula na ustawi wa kijamii na kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Mpango Mkuu wa Sekta ya Uvuvi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2021/22-2036/37) Sekta ya Uvuvi inachangia asilimia 1.7 ya Pato la Taifa (GDP) na kutoa ajira za moja kwa moja kwa wavuvi 195,435 na wafugaji wa samaki 30,064. Aidha, watanzania takriban milioni 4.5 wanapata ajira zisizo rasmi kupitia shughuli za uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa rasimali za uvuvi ulijikita zaidi katika kutathmini endapo Wizara ya Mifugo na Uvuvi (MLF) na TAMISEMI, kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs), zimefanikiwa kutekeleza hatua za udhibiti wa uvuvi ili kuimarisha uvuvi endelevu nchini. Wizara zilizokaguliwa ni Wizara ya Mifugo na Uvuvi (MLF) na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupitia Halmashauri za Serikali za Mitaa (LGAs). Wizara ya Mifugo na Uvuvi ina jukumu la kusimamia rasilimali za uvuvi kwa ujumla, wakati TAMISEMI, kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs), inahusika na usimamizi wa rasilimali hizo katika ngazi za msingi.

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi ulilenga hasa kutathmini maendeleo na utekelezaji wa usajili wa vyombo vya uvuvi na wavuvi, uratibu na ufuatiliaji wa shughuli za uvuvi, ukaguzi na utoaji wa adhabu kwa wavuvi haramu, pamoja na ukusanyaji na utunzaji wa taarifa

sahihi za shughuli za uvuvi. Masuala yote haya yana uhusiano wa moja kwa moja na mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi ulijumuisha kipindi cha miaka mitano cha kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2022/23, ili kufuatilia utendaji na mwelekeo katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Ukaguzi huu ulifanyika kuanzia mwezi Septemba, 2023 na kukamilika mnamo mwezi Machi, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa taarifa ya ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi ulibaini masuala kadhaa ambayo yanahusiana na fedha za umma kama ifuatavyo: -

a) Changamoto katika usimamizi wa shughuli za uvuvi kama vile utoaji wa leseni bila vibali vya aina na kiasi cha samaki wa kuvuliwa.Taarifa ya ukaguzi imebainisha uwepo wa vyombo vya uvuvi visivyosajiliwa kwa ziwa Tanganyika, ziwa Victoria, na bahari ya Hindi. Ziwa Tanganyika lina asilimia 61, bahari ya hindi ina asilimia 42 huku ziwa Victoria likiongoza kwa asilimia 67 ya vyombo visivyokuwa na usajili. Changamoto kuu ilikuwa ukosefu wa usimamizi wa vitengo vya usimamizi wa fukwe (BMU) katika baadhi ya maeneo hali inayopelekea upotevu wa mapato ya Serikali;

b) Ukaguzi ulibaini kuwa ziwa Tanganyika lilikuwa na asilimia 45 ya mialo isiyo na vitengo vya usimamizi wa fukwe, bahari ya hiindi ikiwa na asilimia 36, wakati ziwa Victoria likiwa na asilimia ndogo (1%) ya mialo isiyokua na usimamizi wa fukwe. Uwepo wa mialo isiyo na usimamizi umechangia ongezeko la vyombo vya uvuvi visivyosajiliwa, hali inayohamasisha uvuvi haramu na kuikosesha Serikali mapato stahiki;

c) Ukaguzi ulibaini kuwa vyombo vingi vya uvuvi havijasajiliwa au havina leseni, hali inayochangia uvuvi haramu na kutokuwepo kwa takwimu sahihi za uvuvi. Hii imesababisha hasara inayokadiriwa kuwa **Shilingi Bilioni 15.16**, ikijumuisha mapato ya leseni, ada kutoka Shirika la

Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Mikoa yenye miundombinu bora kama Dar es Salaam na Lindi inakadiriwa kupata hasara ya wastani wa **Shilingi Milioni 500**, huku mikoa kama Mwanza na Kigoma, yenye changamoto za miundombinu na jiografia, ikipata hasara inayokadiriwa kuwa zaidi ya **Shilingi Milioni 500** kutokana na uwepo wa vyombo visivyosajiliwa;

d) Ukaguzi ulibaini uwepo wa samaki wadogo sokoni, kinyume na Kanuni za Uvuvi. Uvuvi wa samaki wasiofikia ukubwa umepungua katika maziwa lakini umeongezeka katika maeneo ya bahari. Hii inahatarisha uendelevu wa uvuvi na usalama wa chakula, ikichochea upungufu wa samaki;

e) Ukaguzi ulibaini changamoto katika ukusanyaji na usimamizi wa takwimu za uvuvi nchini. Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilikusanya taarifa za kila siku za uvuvi chini ya asilimia 10 ya mialo ya ziwa Victoria, na tafiti za tathmini ya upatikanaji wa samaki zilikosa ufadhili wa kutosha. Ukosefu wa fedha ulisababisha tafiti za kina kutofanyika, huku taarifa nyingi zikiwa na makadirio tu, hivyo kuathiri mipango na maamuzi; na

f) Ukaguzi ulibaini ukosefu wa uratibu wa kutosha katika kushirikiana taarifa za usimamizi wa uvuvi kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na TAFIRI;

**Mheshimiwa Spika,**ukaguzi ulifanya uhakiki wa majibu yaliyowasilishwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) hadi kufikia Disemba 2024.Kwa ujumla,katika mapendekezo yaliyotolewa, mapendekezo manne (4) utekelezaji wake ulikuwa haujaanza na mapendekezo (9) yapo katika hatua za utekelezaji, ambapo mapendekezo saba (7) yapo katika hatua zinazoridhisha na mawili (2) yapo katika hatua zaawali.Mapendekezo matatu (3)

yalikuwa yametekelezwa kikamilifu miongoni mwa mapendekezo yote yaliyotolewa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kufanya mahojiano na Afisa Masuuli, Wizara ya Uvuvi ili kupata maelezo ya ziada kuhusu hoja za ukaguzi ambazo zilikuwa hazijapata majibu ya kutosha. Kuhusu utoaji wa leseni za uvuvi, Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kuwa Ofisi ya Rais-TAMISEMI wao wanatoa leseni kwa Boti za ukubwa usiozidi mita 11 ambayo ni sawa na asilimia 70 na Wizara ya Uvuvi inatoa leseni kwa boti zinazozidi mita 11 sawa na asilimia 30.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu namna wanavyosimamia makusanyo ya fedha, Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kuwa makusanyo yanategemea ukubwa wa boti hivyo kwa zile boti ambazo zinazidi mita 11 fedha ya tozo inakusanywa kwa Wizara ya Uvuvi na kwa boti zenye ukubwa usiozidi mita 11 tozo zinalipwa Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Aidha aliifahamisha Kamati kuwa wameongeza Moduli katika Mfumo wa TAUSI ili kuweza kuongeza ufanisi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kusimamia rasilimali za uvuvi nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kuhusu uvuvi haramu, Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kuwa Serikali inajitahidi kudhibiti kwa nguvu zote uvuvi haramu ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa vifaa vya uvuvi na kufanya doria, lakini kazi ya kupambana na uvuvi haramu bado ipo mfano nyavu zinazonunuliwa na wavuvi zinakuwa zimekidhi vigezo lakini zinachezewa matokeo yake wanavyokuwa wanazitumia wanavua na samaki wadogo.Baada ya maelezo haya, Kamati imetoa mapendekezo ya namna ya kuboresha sekta hii ili kuhakikisha fedha za umma zinapatikana inavyostahili.

**Taarifa za Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** mapema Mwezi Machi, 2024, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ili kujiridhisha na thamani halisi ya fedha iliyotumika katika utekelezaji wa miradi hiyo. Ziara zilifanyika katika Mikoa ya Dodoma, Tabora, Shinyanga,

Mwanza na Singida. Jumla ya miradi ya maendeleo kumi na mbili (12) ilitembelewa na kukaguliwa.

**Mheshimiwa Spika,** miradi iliyotembelewa ni pamoja na mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Jijini Dodoma, mradi wa Jengo la Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili - Dodoma, mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi za Wizara ya Nishati awamu ya II mji wa Serikali, Mtumba, mradi wa TANIPAC Dodoma Mtanana-Kongwa DC, mradi wa ujenzi wa shule ya Sekondari Solya Manyoni DC na mradi wa uboreshaji na ukarabati wa uwanja wa ndege wa Tabora.

**Mheshimiwa Spika,** miradi mingine iliyotembelewa na kukaguliwa inajumuisha mradi wa kutoa Maji ziwa Victoria, awamu ya kwanza na ya pili na mradi wa Kiwanda cha kupaka Rangi Mabomba kwa ajili ya kuweka mfumo wa upashaji joto mabomba katika mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

**Mheshimiwa Spika,** miradi mingine iliyotembelewa ni pamoja na mradi wa ujenzi wa usambazaji wa miundombinu ya barabara pamoja na uunganishwaji wa umeme kwa wateja, awamu ya tatu hatua ya pili kwa vijiji vya Mkoa wa Shinyanga na mradi wa upanuzi na usambazaji maji Shinyanga.

**Mheshimiwa Spika,** miradi mingine iliyotembelewa na kukaguliwa ilikuwa ni pamoja na ujenzi wa hoteli ya kitalii ya NSSF jijini Mwanza, mtambo wa kusafisha dhahabu - Mwanza, ujenzi wa meli ya MV Mwanza, ukarabati wa meli ya MV Victoria na MV Umoja, ujenzi wa vivuko mbalimbali unaotekelezwa na mkandarasi Songoro katika yadi iliyopo Ilemela, Mwanza.

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi wa miradi uliofanywa na Kamati ulihusu pia miradi ya TARURA Mwanza, jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Sekou Toure, ujenzi wa ghorofa za watumishi wa umma za Ghana Kota, Mwanza (Block II), ujenzi na utekelezaji wa miradi ya usambazaji maji katika miji na vijiji vya Tinde na Shelui kutoka mradi wa uendelezaji wa ziwa Victoria, mradi wa utambuzi wa vipande vya Ardhi 13,600 na uandaaji wa

michoro ya mipango miji yenye viwanja 4,492 na ujenzi wa chuo cha VETA Ikungi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia majukumu ya msingi ya Kamati hii, ambayo ni kubainisha maneneo yenye changamoto katika matumizi ya fedha za umma, Kamati imetoa taarifa ya miradi iliyokaguliwa kama ifuatavyo: -

***Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kukagua mradi huu unaotekelezwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa uliopo katika Mkoa wa Dodoma. Mradi huu unatekelezwa na mkandarasi *M/S GROUP SIX INTERNATIONAL LTD* pamoja na wakandarasi wasaidizi kwa kiasi cha cha Shilingi **21,101,174,224** (ikijumuisha **Shilingi 20,431,828,643.50** za mkandarasi na **Shilingi 669,345,580** za mshauri mwelekezi) ambapo pesa zote zilikuwa zimetumika katika kutekeleza mradi.

**Mheshimiwa Spika**,changamoto iliyobainika wakati wa utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa katika eneo la Mlimani Dodoma. Kwa mujibu wa mkataba, mradi ulitakiwa kukamilika tarehe 25 Mei 2023, hata hivyo, baada ya hapo mradi ulipata nyongeza ya pili ya muda wa utekelezaji wa mradi hadi tarehe 30 Oktoba,2023. Kisha nyongeza ya tatu ya muda wa utekelezaji iliridhiwa na kuongeza muda wa ukamilishaji mradi hadi tarehe 30 Aprili, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, wakati ukaguzi unafanyika tarehe 12 Novemba,2023 CAG alibaini kuchelewa kukamilika kwa mradi hivyo kuashiria kutokamilika kwa mradi huu kwa wakati.

***Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu na Ofisi ya Kanda ya Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili***

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa mradi huu ulitangazwa kupitia Zabuni Namba IE/022/2016/W/02/3.Mkandarasi wa Ujenzi ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na mshauri elekezi ni Wakala wa Majengo

Tanzania (TBA) ambao walijenga kwa mkataba mmoja wa kubuni na kujenga (design and build).

**Mheshimiwa Spika,** mkataba ulisainiwa tarehe 14 Juni,2019 na kuanza rasmi tarehe hiyo ambao ulipewa muda wa kipindi cha miezi 42 na ulitazamiwa kukamilika tarehe 15 disemba 2022.Hadi sasa mkataba huu umepewa nyongeza mara nne, sababu kubwa ya nyongeza ya muda wa mkataba ni mkandarasi kutokamilisha ujenzi. Kwa sasa muda wa matazamio ni kuanzia tarehe 03 Mei,2024 kwa muda wa miezi 12 hadi tarehe 03 Mei 2025.

**Mheshimiwa Spika,** fedha za utekelezaji wa mradi huu ni kiasi cha Shilingi **9,064,275,060.04** ikiwa ni pamoja na VAT. Hadi sasa mkandarasi amelipwa hati za malipo *(certificate)* Namba 1 hadi 8 zenye jumla ya **Shilingi 8,136,937,166.8** hadi sasa mkandarasi ana bakaa ya **Shilingi 927,337,893.27**. Hadi wakati Kamati inakagua mradi huu hapakuwa na madai yaliyowasilishwa ambayo hayajalipwa.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto zilizobainika katika mradi huo ni ukiukwaji wa taratibu za malipo kwa mujibu wa dhamana ya utendaji kiasi cha **Shilingi 16,299,428.28** na kuongezwa kwa muda wa mkataba pasipo kuongeza dhamana ya utendaji. Aidha, kazi ambazo hazijakamilika ni nyingi ukilinganisha na muda uliobaki wa utekelezaji wa mradi. Kazi hizo ni pamoja na usimikaji wa mifumo ya teknolojia ya mawasiliano na data na mfumo wa umeme.

***Mradi wa Ujenzi wa Ghorofa za Watumishi wa Umma Eneo la Ghana Kota.***

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na maeneo ya Ghana Kota Mwanza kuwa oevu (prime), Serikali ilielekeza maeneo yote ya Kota yaendelezwe kwa kujenga nyumba za kuchukua familia nyingi pamoja na ukarabati wa nyumba hizo. Maelekezo hayo yameainishwa pia kwenye ibara ya 55(h)(ii) ya ilani ya uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020.Mradi wa Ghana kota (Block I & II) ni mojawapo ya utekelezaji wa maelekezo ya Serikali juu ya uendelezaji wa maeneo ya Kota nchini.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekelezwa kwa kutumia fedha za ruzuku ya Serikali na mapato ya ndani ambapo **Shilingi 7,747,313,193.73** ni gharama za mradi kwa Block I na **Shilingi 6,192,260,778.33** ni gharama za mradi kwa Block II. Hadi Kamati ilipotembelea mradi huu Mwezi Machi, 2024 kiasi cha fedha kilichotumika hadi kufikia wakati huo ni **Shilingi 2,123,159,500** kwa Block I na **Shilingi 500,000,000** kwa Block ya II.

**Mheshimiwa Spika,** mapungufu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa mradi huu ni pamoja na kuanza kutekelezaji wa mradi bila kuwa na kibali cha ujenzi kutoka Manispaa ya Ilemela Block I na Block II na kuanza utekelezaji wa mradi bila kuwa na Cheti cha Tathimini ya Athari ya Mazingira na Jamii "Environmental and Social Impact Assessment" kutoka NEMC kwa mradi wa Block I.

***Mradi wa Ujenzi wa Meli Mpya ya* "MV Mwanza Hapa Kazi Tu"**

**Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) inatekeleza miradi ya maendeleo katika ziwa Victoria ambayo inahusiana na ujenzi wa meli mpya na ukarabati wa meli mbili. Miradi hii ambayo inafadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni sehemu ya mikakati ya kuijengea uwezo MSCL ili kutimiza jukumu lake la msingi la kutoa huduma ya usafiri kwa njia ya maji kwa abiria na mizigo.

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa ujenzi wa meli mpya unaendelea kutekelezwa, kwa sasa ukiwa katika hatua za mwisho na miradi ya ukarabati wa meli mbili tayari ilishakamilika na meli hizo zinaendelea kutoa huduma katika ziwa Victoria. Gharama za utekelezaji wa mradi mzima hadi unakamilika zitakuwa ni jumla ya kiasi cha **Dola za Marekani 49,322,365.40**. Hadi sasa mkandarasi ameshalipwa jumla ya kiasi cha **Dola za Marekani 44,913,462.84** ambazo ni sawa na asilimia 91.06 ya gharama zote za mradi.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto zilizobainishwa katika mradi huu ni pamoja na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) ilianza ujenzi wa meli mpya bila kuwa na taarifa ya dhana ya mradi (concept note), kutokuwepo kwa upembuzi yakinifu wa mradi, ujenzi wa meli mpya bila kitanda cha kujengea meli (slipway) kukamilika,

MSCL haikusimamia uzingatiaji wa utoaji wa boti za uokoaji, uwekaji vibaya wa nyaya za umeme eneo ambalo mizigo ilikuwa inahifadhiwa na ongezeko la muda wa kukamilisha mradi.

***Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto Katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza (SEKOTOURE)***

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza iliingia Mkataba na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), ambapo ujenzi ulianza kwa kufuata usanifu wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) lenye ghorofa mbili. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya mahitaji na matumizi ya jengo la kutoa huduma za wagonjwa wa nje kuwa jengo la huduma ya mama na mtoto, ilionekana halikidhi mahitaji hali iliyolazimu kubadilisha usanifu wa msingi utakaohimili ujenzi wa kubeba ghorofa tano (sawa na sakafu sita).

**Mheshimiwa Spika,** gharama za awali za mradi zilikadiriwa kuwa **Shilingi 10,106,468,902.21** (ikijumuisha VAT) ambapo kutokana na mahitaji kuongezeka gharama za ujenzi ziliongezeka hadi kufikia **Shilingi 13,916,811,260.29** ikiwa na ongezeko la **Shilingi 3,810,342,358.08** Aidha, mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali kwa asilimia 100.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliweza kubaini changamoto kadhaa katika utekelezaji wa mradi huu ikiwa ni kutokamilika kwa wakati kwa ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza (Sekotoure). Kazi ambazo zilikuwa hazijakamilika ni pamoja na kurekebisha dosari zilizobainika, ujenzi wa tenki la maji (kazi zilizobakia ni ufungaji wa pampu ya kusukuma maji), kusimika mifumo ya TEHAMA na kusimika viyoyozi.

***Mradi wa Ujenzi wa Hoteli ya kitalii Yenye Hadhi ya Nyota Tano Jijini Mwanza***

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) unatekeleza mradi wa ujenzi wa hoteli ya hadhi ya nyota tano (Mwanza Tourist Hotel) iliyopo eneo la Capripoint, jijini Mwanza.Ujenzi wa hoteli hii unajumuisha vyumba 168 vya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na sehemu maalumu kwa mapumziko

ya Rais (*presidential suite)* migahawa ya aina mbalimbali, sehemu ya vinywaji ikiwemo sehemu ya juu (*roof top bar*) na sehemu ya viwanja vya michezo (*sport bar*).

**Mheshimiwa Spika,** huduma nyingine zinazopatikana katika jengo hili ni ukumbi wenye uwezo wa kuchukua watu mia tano (500), kumbi nyingine ndogondogo, bwawa la kuogelea, sehemu ya kutua chopa (*helipad*), sehemu ya kufanyia mazoezi (*gym*), sehemu ya huduma za ustawi na kupumzika (SPA), ofisi, maduka na sehemu ya maegesho ya magari.

**Mheshimiwa Spika,** gharama ya mradi huu ilikuwa ni kiasi cha **Shilingi 93,953,214,099.99** ambapo kiasi kilicholipwa hadi sasa ni **Shilingi 63,712,739,572.40** ambapo jumla ya gharama zote za mradi hadi mwezi Machi,2024 ni **Shilingi 98,073,245,748.99** na jumla ya fedha zilizolipwa kwa mkandarasi hadi Machi 2024 ni **Shilingi 66,781,156,132.40**.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto ya mradi huu ni pamoja na kuchelewa kukamilika kwa mradi kwa muda wa miaka 8 ambao hadi wakati Kamati inatembelea ni kiasi cha **Shilingi Bilioni 4.12** kimelipwa kama fidia ya kuchelewa kwa mradi kwa mkandarasi, kuwa na fedha zinazojirudia kwa kazi moja katika mkataba wa mkandarasi mkuu na wakandarasi wadogo na kuanzisha mradi wa ujenzi wa hoteli yenye hadhi ya nyota tano pasipo kuwa na muendesha hoteli.

**Mheshimiwa Spika**, kuanza kwa utekelezaji wa mradi bila ya kuwa na muendesha hoteli kulisababisha NSSF kufanya mabadiliko makubwa ya ujenzi uliokuwa tayari umekamilika, hali hii imeongeza gharama za mradi.

***Mradi wa Ujenzi Barabara kwa Kiwango cha Lami (Double Surface Dressing)***

**Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Mwanza una mtandao wa Barabara wenye urefu wa kilometa 8,586.763 ambapo km 99.892 sawa na asilimia 1.16 ni Barabara za lami, km 11.339 sawa na asilimia 0.13 za zege, km 18.739 sawa na asilimia 0.22 ni barabara za mawe na barabara za changarawe zina urefu wa km 1,797.785 sawa na

asilimia 20.94 ya mtandao wote barabara za udongo ni km 6,659.008 sawa na asilimia 77.55.

**Mheshimiwa Spika**, gharama ya mradi huu ni **Shilingi 1,138,156,210** (bila ya VAT) na hapakuwa na gharama iliyoongezeka kutokana na wigo wa nyongeza *(variation)*. Aidha, bakaa hadi kukamilika kwa mradi ilikuwa kiasi cha **Shilingi 11,599,044**. Kiasi kilicholipwa hadi kipindi cha matazamio kilipoisha tarehe 25 Juni 2023 ni **Shilingi 1,126,557,166**.

**Mheshimiwa Spika**, mapungufu yaliyobainishwa kwenye mradi huu ni usanifu haukuzingatia usalama barabarani, upana wa Barabara haukufikiwa kulingana na matakwa ya usanifu, wakandarasi hawakuandaa mwongozo wa matengenezo ya Barabara (operation and maintaince manual, kurukwa kwa kipande cha Barabara cha mita 500 katika Barabara ya Luchelele na Kwenda kujengwa kipande cha mbele.

***Mradi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Solya – Manyoni, Dodoma***

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu wa ujenzi wa shule ya Sekondari ya Wasichana ya Solya, Wilaya ya Manyoni, Singida ni miongoni mwa shule zinazojengwa chini ya Mradi wa Kuongeza Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP) unaolenga kutoa mazingira mazuri ya kujifunzia kwa wasichana na kuboresha elimu ya sekondari kwa wavulana na wasichana. Shule hii ya wasichana ya Mkoa wa Singida imejengwa katika Wilaya ya Manyoni kata ya Solya.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu wa ujenzi wa shule hii ilitakiwa kuwa jumla ya **Shilingi Bilioni 4. 739. Aidha**, jumla ya gharama ya kazi zilizofanyika hadi Kamati inatemebelea ilikuwa ni **Shilingi Bilioni 4.236**, kiasi cha fedha kilicholipwa ni **Shilingi Bilioni 4.124** na jumla ya madeni ya kazi zilizo fanyika ni **Milioni 113**.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto zilizobainika katika utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na kuchelewa kukamilika kwa mradi ambako kulisababishwa na kuchelewa kukamilika kwa majadiliano ya eneo la kutekeleza mradi. Hivyo mradi ulichelewa

kutekelezwa kwa kipindi cha miezi 3, kwani fedha iliingia Mwezi Januari, 2022 na utekelezaji ulianza Mwezi Aprili, 2022.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto nyingine iliyiobainika katika ukaguzi wa mradi huu ilikuwa kutowepo utaratibu mzuri wa uwekaji kumbukumbu ya vifaa vilivyotumika, uwepo wa fremu za milango zisizo na ubora katika mabweni na kutojumuishwa kwa gharama za usimamizi wa mradi ambazo zilipelekea kukosekana kwa usimamizi wa kutosha wa mradi.

***Mradi wa Ujenzi na Usambazaji wa Miundombinu, Uwekaji wa Transfoma Pamoja na Uunganishaji wa Umeme kwa Wateja Awamu ya Tatu na Hatua ya Pili (REA III round II) kwa Wilaya ya Kahama –Shinyanga***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kutembelea na kukagua mradi huu wa kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa pili (REA III Round II) Fungu Na.27 (Lot 27) unaotekelezwa Wilaya ya Kahama katika vijiji 146. Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi M/s Tontan Project Technology Co Ltd Jv Group Six International kwa mkataba wa miezi 18.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya **Shilingi 46,092,316,042.58** (zimejumuisha kodi ya ongezeko la thamani). Hadi, kamati inatembelea na kukagua mradi kiasi cha **Shilingi 12,951,343,589.58** kilikuwa kimeshalipwa kwa kazi zilizokwisha kufanyika. Aidha mradi hadi unakaguliwa na Kamati ulikuwa umekamilika kwa asilimia 61.46 na fedha iliyolipwa ni asilimia 28.09.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto kubwa iliyobainika katika utekelezaji wa mradi huu ilikuwa ni kasi ndogo ya ujenzi na usambazaji wa miundombinu ya umeme katika vijiji 146 vya Wilaya ya Kahama. Hali hii ilipelekea marejeo ya kipindi cha kumalizika kwa mkataba ambapo miezi minne iliongezwa. Aidha uhakiki ulibaini bado kuna kasi ndogo ya utekelezaji ambayo inaleta mashaka kama mradi unaweza kukamilika ndani ya muda wa mkataba.

***Mradi wa Ujenzi wa Chanzo Cha Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA)***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kutembelea na kukagua Mradi wa Usanifu na Ujenzi wa Chanzo cha Maji Butimba (*Design and Build of Butimba Intake, Raw Water Pipeline and Treatment Plant*) wenye zabuni namba EA/042/2015-2016/W/03c na unatekelezwa na mkandasi M/s. Sogea Santom JV M/s.Vinci Grand Projects. Aidha hadi Kamati inatembelea mradi ulikuwa umekamilika (physical) kwa asilimia 100.

**Mheshimiwa Spika,** gharama za mradi huu ni **Shilingi 71,696,908,539**, hadi kufikia 8 Machi, 2024 kiasi kilichokuwa kimelipwa hadi wakati wa uhakiki ni **Shilingi 64,295,987,031** na kiasi ambacho bado mkandarasi anadai na hakijalipwa (certified works but not paid) ni **Shilingi 5,374,949,143**.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto zilizobainika katika utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na ufinyu wa miundombinu ya usambazaji maji kwenye maeneo mbalimbali kama vile Nyegezi, Buhongwa, Kishili, Kisesa, Luchelele na Fumagila. Aidha Kamati ilibaini changamoto ya uwepo wa mgao wa umeme kwenye eneo la chanzo Butimba na maeneo mengine ya vituo vya kusukuma maji vya Sahwa na Nyegezi.

***Mradi wa Upanuzi wa Bomba la Maji Kutoka Ziwa Victoria Kwenda Katika Miji ya Tinde na Shelui Katika Mikoa ya Singida na Shinyanga***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kutembelea na kukagua mradi huu wa upanuzi wa bomba la maji kutoka ziwa Victoria kwenda katika miji ya Tinde na Shelui katika Mikoa ya Shinyanga na Singida na vijiji 34 vilivyopo pembezoni mwa bomba kuu. Aidha mradi huu unaotekelezwa na Wizara ya maji chini ya ufadhili wa Benki ya Exim ya India. Hadi kamati inatembelea mradi huu ulikuwa umefikia asilimia 100 (physical).

**Mheshimiwa Spika,** gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani 10,637,666** sawa na **Shilingi Billioni 24.47**, hadi kufikia Machi 2024

mkandarasi alikuwa amelipwa asilimia 98.3 ya malipo yote ya mkataba. Aidha gharama ya mshauri elekezi ni **Dola za Marekani 560,014.96** sawa na **Shilingi Billioni 1.3**.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto zilizobainika katika mradi huu ni pamoja na kuchelewa kukamilika kwa mradi, mapungufu katika usanifu wa mradi, usimamizi na ufuatiliaji wa mradi ulikuwa na changamoto kadhaa katika mchakato wa ununuzi na utoaji wa mikataba.

***Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Veta Ikungi***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kutembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa chuo cha VETA Wilaya ya Ikungi ambao unatekelezwa kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA). Mradi huu umetekelezwa kwa fedha za ndani kwa kutumia Force account.

**Mheshimiwa Spika,** gharama za mradi huu ni **Shilingi 3,004,013,405.56** ambapo kiasi cha **Shilingi 2,635,342,538.00** kilikuwa kimelipwa hadi kufikia wakati wa uhakiki *(audit verification)*. Aidha kiasi ambacho bado wazabuni wanadai na hakijalipwa (*certified works but not paid)* ni **Shilingi 18,572,500.00**.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto zilizobainika katika utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na kuchelewa kukamilika kwa wakati kwa mradi huu kutokana na kuchelewa kwa utoaji wa fedha za mradi na ukosefu wa makadirio halisi ya ujenzi (Deficiency in BOQ).

***Uchambuzi wa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2023***

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 29 Oktoba, 2024 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) iliwasilisha Taarifa yake Bungeni kuhusu uchambuzi wa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Ukaguzi wa Hesabu za

Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Kamati cha Mwezi Agosti 2024 hadi Oktoba 2024, shughuli za Kamati zilijielekeza katika kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara na Mashirika ya Umma kama yalivyobainishwa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka wa Fedha unaoshia tarehe 30 Juni, 2023. Aidha, shughuli hizo zilikusudia kufuatilia utekelezaji wa maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa nyakati tofauti kwa kipindi chote cha Mwaka 2023 hadi 2024.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2023, kwa upande wa Serikali Kuu, CAG alikagua na kutoa Hati za ukaguzi kwa Wizara na Idara za Serikali **64**, Balozi **43**, Sekretarieti za Mikoa **26**, Wakala **30** na Mifuko Maalumu **19.** Aidha, katika kundi hilo la Serikali Kuu, Kaguzi za Vyama vya Siasa **19**, Hospitali za Rufaa na Maalumu **34** na Taasisi nyinginezo **266** zilifanyika na kukamilika. Hali kadhalika, ukaguzi ulijumuisha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Hesabu Jumuifu za Taifa (consolidated accounts) na ukaguzi wa awali wa mafao ya wastaafu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023.


**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/23, katika mafungu ya Serikali Kuu, CAG alitoa jumla ya Hati **475** kwa Taasisi ambazo ziliwasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi. Kati ya hizo, Hati **471** zilikuwa zinaridhisha, Hati **1** ilikua Hati yenye shaka, Hati **1** ilikuwa mbaya, na CAG alishindwa kutoa maoni kwa Taasisi **2**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mashirika ya Umma, jumla ya kaguzi **215** zilifanyika, ambapo katika kaguzi hizo Hati zilitolewa kwa Mashirika **215** ambapo kati ya hizo, Hati **211** zilikuwa Hati zinazoridhisha, **4** ni Hati zenye shaka. Kwa mwaka huu tunaoutolea Taarifa hapakutolewa Hati mbaya katika Mashirika ya Umma.

**Mheshimiwa Spika,** katika ngazi ya Kamati, Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za mafungu 19 ya Serikali Kuu, Mashirika ya Umma 20, Taasisi zinazojitegemea 27 na Mifuko Maalumu 4.

**Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa Taasisi zilizofika mbele ya Kamati kwa mahojiano umebainishwa katika Chati Na. 2.2 hapa chini: -

**Chati Na. 2.4 : Mchanganuo wa Taasisi zilizofika mbele ya Kamati kati ya Agosti - Novemba, 2024**




**Chanzo:** ***Uchambuzi wa Kamati Katika Taarifa za CAG kwa Ukaguzi wa Hesabu zilizoishia Tarehe 30 Juni, 2023.***

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lako Tukufu lilipitia na kujadili Taarifa ya Kamati inayohusu Taarifa hizo za ukaguzi kwa muda wa siku tatu (3) kuanzia tarehe 29 Oktoba, 2024 hadi tarehe 31 Oktoba, 2024. Baada ya mjadala Bungeni, Bunge lilipitisha jumla ya Maazimio ya Bunge kumi na tatu (13).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati itaendelea kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Maazimio hayo ya Bunge kuanzia Mwezi Machi, 2025 ili kuhakikisha uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

Kamati ina imani kwamba Bunge litapata fursa ya kujadili tena hali halisi ya utekelezaji wa Maazimio hayo ya Bunge kabla ya kukamilika kwa Mkutano wa Bunge la Bajeti.

**Mafunzo na Semina za Kuwajengea Uwezo Wajumbe**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukurani za dhati kwako wewe binafsi kwa kutoa idhini kwa Kamati ya PAC kupatiwa mafunzo na semina mbalimbali kwa ajili ya kuongeza uelewa, ufanisi na uwezo wa wajumbe katika kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma.

Aidha, napenda kuishukuru Ofisi ya Katibu wa Bunge kwa kufanya uratibu na kuwezesha kufanyika kwa shughuli hizo za mafunzo na semina.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Mwezi Januari, 2024 hadi Mwezi Februari, 2025 Kamati kwa idhini yako ilifanikiwa kupatiwa mafunzo na semina katika maeneo tisa (9). Mafunzo na Semina hizo yalitolewa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na Asasi za Kiraia zinazoangalia matumizi ya fedha za umma. Mafunzo na Semina hizo ziliweka msisitizo katika maeneo yafuatayo: -

a) Uchambuzi wa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

b) Kuongeza uelewa kuhusu hati mbalimbali za ukaguzi zinazotolewa katika Ripoti za CAG;

c) Kujenga uelewa kuhusu mfumo wa usimamizi wa mali za Serikali (Government Assets Management Information System – GAMIS);

d) Kujenga na kuongeza uelewa kuhusu muundo wa Kamati za Ukaguzi wa Ndani na usimamizi wa vihatarishi katika Taasisi za Umma;

e) Kujenga na kuongeza uelewa kuhusu kaguzi mbalimbali zinazofanywa na CAG;

f) Uelewa kuhusu mfumo wa malipo Serikalini (GePG);

g) Kujenga na kuongeza uelewa kuhusu uwazi na uwajibikaji katika kusimamia matumizi ya fedha za umma;

h) Kujenga na kuongeza uelewa kuhusu wajibu wa Mkaguzi Mkuu wa Ndani katika kuimarisha uwajibikaji, usimamizi wa fedha na utawala bora; na

i) Kujenga na kuongeza uelewa kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Taasisi na Mashirika ya Umma.

**Mheshimiwa Spika,** mafunzo haya yameendelea kuwa nguzo kubwa katika kufanikisha majukumu ya Kamati ya PAC. Waheshimiwa Wajumbe waliongeza weledi katika shughuli za uchambuzi wa Taarifa za CAG hivyo kuongeza ufanisi katika kutimiza majukumu yao ya Kikanuni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inategemea kuendelea kupata mafunzo kama hayo na mengine kwa mawanda mapana zaidi ili kuendelea kuboresha utendaji kazi wa Kamati na Bunge kwa ufanisi na weledi mkubwa.

## SEHEMU YA TATU

## MAONI NA MAPENDEKEZO

### Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imefafanua kwa kina shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa kipindi cha Mwezi Januari 2024 hadi Februari, 2025. Shughuli hizo zinajumuisha, uchambuzi wa Taarifa za CAG kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023, uchambuzi wa taarifa za kaguzi za ufanisi na kiufundi, ukaguzi wa miradi ya maendeleo na mafunzo na semina za kuwajengea uwezo Waheshimiwa Wajumbe. Kwa kuzingatia utekelezaji wa shughuli zote hizo, Kamati ina maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

**Maoni**

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kamati yamezingatia jukumu la Bunge kuwa chombo mahsusi cha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Kwa mantiki hiyo, Kamati ina maoni ya ujumla yafuatayo: -

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni ya jumla kuwa Bunge limeendelea kuwa na dhima kubwa ya kusimamia uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma. Aidha, kwa kuzingatia dhima hiyo, ni maoni ya Kamati kuwa kwa kipindi cha Mwezi Januari, 2024 hadi Februari, 2025 Bunge limetekeleza wajibu wa kusimamia uwajibikaji wa fedha za umma kwa weledi na ufanisi mkubwa.

Ni maoni ya kamati kuwa wajibu huu muhimu utaendelea kuimarishwa kupitia maboresho muhimu ya mifumo ya udhibiti katika usimamizi wa fedha za umma ikiwa ni pamoja na kuendelea kuboresha Sheria na Kanuni zinazosimamia fedha za umma ili kuongeza hatua za kiuwajibikaji.

**Mapendekezo**

**Mheshimiwa Spika,** mapendekezo ya Kamati yametolewa kwa kuzingatia dhima ya Kaguzi za Ufanisi na Kaguzi za Kiufundi pamoja na miradi ya maendeleo ambayo kwa kiasi kikubwa ndio imechambuliwa katika Taarifa hii. Kwa msingi huo, mapendekezo ya Kamati yamejilekeza katika kuhakikisha kunakuwepo na tija, uwekevu na ufanisi katika matumizi ya fedha za umma. Naomba kuwasilisha mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo: -

***Kuhusu Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato***

**KWA KUWA,** Taarifa ya CAG imebainisha changamoto kadhaa katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato, ikiwa ni pamoja na dosari katika uandaaji wa mipango na usanifu wa mradi, usimamizi wa mikataba, manunuzi na kuchelewa malipo;

**NA KWA KUWA,** changamoto zilizobainishwa hapo awali zina athari za kifedha kwa Serikali ikiwa ni pamoja na: -

a) Ongezeko la gharama za ujenzi kwa **Shilingi Bilioni 6.97** kutokana na sababu mbalimbali;

b) Adhabu ya riba ya **Shilingi Milioni 322.721** kutokana na kuchelewa malipo kwa wakandadarasi; na

c) Kuchelewa mchakato wa kumpata mkandarasi wa pili (anayehusika na ujenzi wa miundombinu ya majengo mbalimbali ikiwepo jengo la abiria, ofisi, n.k) hali ambayo itapelekea ongezeko la gharama kutokana na nyongeza ya mkataba wa mshauri elekezi anayesimamia ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

a) Serikali ifanye mapitio ya vipengele vya mikataba ya makubaliano ya ufadhili *(financing agreement)* ili kuweka usawa wa malipo ya gharama zinazoongezeka kwa kuhakikisha kuwa upande uliosababisha ongezeko hilo unawajibika; na

b) Serikali ihakikishe Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) wanasimamia kikamilifu mradi na kufanya tathmini ya kina kuhusu hasara zilizotokana na dosari za awali za usanifu, ikiwa ni pamoja na kuweka uwajibikaji wa gharama zilizozalishwa kwa pande zinazohusika na mkataba; na

c) TANROADS ihakikishe kuwa kazi zilizoongezeka na zitakazoendelea kuongezeka zinaidhinishwa na Bodi ya Zabuni kwa mujibu wa maharti ya Mikataba, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyopo ili kudhibiti ongezeko la gharama.

***Kuhusu Ukaguzi wa Kiufundi Katika Ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya na Vyuo vya Ufundi Stadi na Huduma vya Mikoa***

**KWA KUWA,** kupitia uchambuzi wa Taarifa ya CAG katika ukaguzi wa kiufundi wa ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi vya wilaya na vyuo vya ufundi stadi na huduma vya mikoa, ilibainika uwepo wa changamoto kadhaa katika utekelezaji wa miradi hiyo ikiwa ni pamoja na: -

a) Kutokamilika kwa wakati kwa baadhi ya miradi ya ujenzi wa vyuo;

b) Changamoto ya mtiririko wa fedha; na

c) Kutokuwepo hati miliki za ardhi kwa baadhi ya maeneo.

**NA KWA KUWA,** changamoto hizo zimechangia masuala yafuatayo:-

a) Kuchelewa kukamilika miradi kutokana na mtiririko wa fedha kutoenda sambamba na mpango wa ujenzi; na

b) Kutojumuishwa katika ujenzi kwa baadhi ya miundombinu muhimu kama vile miundombinu ya kupambana na majanga ya moto.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

a) Wizara ya Fedha itoe kipaumbele cha kutoa fedha za kukamilisha miradi ya ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi ili vikamilike na kuanza kutoa ujuzi kwa vijana wa kitanzania kama ilivyokusudiwa;

b) Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) zihakikishe kunakuwepo usimamizi thabiti wa miradi ya ujenzi wa vyuo vya ufundi ili kufikia viwango vya ubora vya ujenzi vinavyokubalika; na

c) Serikali ihakikishe kuwa mahitaji yote muhimu ikiwemo mifumo ya kupambana na majanga ya moto inajumuishwa katika ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi na huduma unaoendelea.

***Kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi Katika Udhibiti wa Usambazaji wa Mbolea kwa Wakulima***

**KWA KUWA,** Taarifa ya CAG kuhusu ufanisi katika udhibiti wa usambazaji wa mbolea kwa wakulima imebainisha uwepo wa baadhi ya mbolea na virutubisho vyenye changamoto za ubora sokoni, na uwepo wa baadhi ya maduka ya mbolea ambayo hayajasajiliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA). Vilevile, CAG almebainisha kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania haikuwa na utaratibu na mfumo madhubuti wa kukadiria *(forecasting)* mahitaji halisi na ya kutosheleza ya mbolea;

**NA KWA KUWA,** masuala hayo yaliyobainishwa hapo juu yamesababisha athari zifuatazo: -

a) Upatikanaji wa takwimu zenye dosari kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuzitumia kukadiria mahitaji ya mbolea nchini; na

b) Changamoto ya upatikanaji mbolea ya kutosha na kwa wakati kwa wakulima, kwani kati ya wakulima 3,389,951 waliosajiliwa kwenye mfumo wa ruzuku wa mbolea ni wakulima 838,712 walioweza kutumia mbolea ya ruzuku.

**KWA HIYO BASI,** Bunge liaanzimia kwamba: -

a) Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Mamlaka ya Udhibiti Mbolea Tanzania ziimarishe mifumo ya usambazaji wa mbolea kwa kuzingatia ubora, bei elekezi na kuwafikia wakulima kwa wakati; na

b) Hatua stahiki zichukuliwe kwa wasambazaji wa mbolea ambao watagundulika kuwa wanauza mbolea bila

kufuata miongozo ya usambazaji wa mbolea kwa wakulima nchini inayokuwa imetolewa na Serikali.

***Kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi Juu ya Usimamizi na Ufuatiliaji wa Watoa Huduma za Bima***

**KWA KUWA,** Kamati imebaini uwepo wa changamoto katika usimamizi wa watoa huduma za bima nchini kutokana na doasari katika usimamizi na ufuatiliaji madhubuti wa utendaji wa kampuni za bima nchini;

**NA KWA KUWA,** changamoto husika za usimamizi zimesbabisha kutokutolewa kwa huduma bora za bima ambazo zinatarajiwa kutolewa na Kampuni za Bima na uwepo wa ucheleweshaji wa malipo ya fidia kwa wateja wa huduma za bima pindi wanapopata majanga;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:-

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) ihakikishe inasimamia na kufuatilia kwa uthabiti watoa huduma za bima nchini. Aidha, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima ihakikishe Kampuni za Bima zinawekeza mtaji wa kutosha ili kuwa na ukwasi unaokubalika kisheria na kulinda maslahi ya wananchi na taifa kwa ujumla.

***Kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi Katika Uwezeshaji wa Wachimbaji Wadogo wa Madini Nchini***

**KWA KUWA,**Taarifa ya ukaguzi kuhusu ufanisi katika uwezeshaji wa wachimbaji wadogo wa madini nchini ilibainisha masuala kadhaa yanayopunguza uchangiaji wa sekta hiyo ndogo kwenye mapato ya Serikali. Masuala hayo ni pamoja haya yafuatayo:-

a) Changamoto katika mipango iliyopo ya kuwawezesha wachimbaji wadogo wa madini nchini. Hali hiyo inatokana na upungufu katika upatikanaji wa taarifa za kijiolojia pamoja na upungufu wa vifaa na teknolojia ya uchimbaji na uchenjuaji kwa wachimbaji wadogo wa madini;

b) Vilevile, idadi ya wachimbaji wadogo wa madini waliowezeshwa kifedha, teknolojia na mafunzo ni ndogo kuliko mahitaji, hali iliyosababishwa na uratibu, ufuatiliaji na tathmini zisizojitosheleza na kutotoa kipaumbele kwa masuala ya uchimbaji mdogo wa madini wakati wa maandalizi ya mipango ya mwaka na bajeti;

**NA KWA KUWA,** changamoto hizo zilizobainishwa na CAG zinachangia Serikali kutopata mchango stahiki wa mapato kutokana na shughuli za uchimbaji mdogo wa madini;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:-

a) Serikali ihakikishe Wizara ya Madini na Taasisi zake zinasimamia na kufuatilia kikamilifu shughuli za uchimbaji mdogo wa madini nchini ili kuhakikisha zinatoa mchango stahiki kwenye mapato ya Serikali na kwa jamii kwa ujumla; na

b) Wizara ya Madini ihakikishe Taasisi zake zinazohusika na wachimbaji wadogo zinaratibu jitihada za pamoja katika uwezeshaji wa wachimbaji wadogo ili kuinua hali ya uchumi wao na wa taifa kwa ujumla.

***Kuhusu Ukaguzi wa Kiufundi Katika Ujenzi wa Kivuko Kipya cha Nyamisati – Mafia na Mv Kilindoni na Ukarabati wa Mv Kazi na Mv Nyerere***

**KWA KUWA,** Kamati imebaini kuwa, Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) ulikabiliwa na changamoto katika uzingatiaji wa Kanuni za Manunuzi ikiwemo kutokufanya uhakiki wa kina wa uwezo wa mkandarasi wa ujenzi na ukarabati wa baaadhi ya vivuko husika;

**NA KWA KUWA,**changamoto zilizobainishwa hapo juu zimesababisha athari kadhaa kwa Serikali ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo:-

a) Changamoto za ubora katika ujenzi wa vivuko hali iliyosababisha vivuko vipya vilivyojengwa kuanza kufanyiwa matengenezo ndani ya muda mfupi hasa upande wa injini; na

b) Miradi ilichelewa kukamilishwa kwa wakati kutokana na dosari za usimamizi.

**KWA HIYO BASI;** Bunge linaazimia kwamba: -

a) Serikali ihakikishe Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) anahakikisha usimamizi thabiti wa kazi zote za ujenzi wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa vivuko;

b) TEMESA ihakikishe kila mradi unakuwa na meneja mradi mwenye uwezo wa kiufundi na kiuongozi ili kuhakikisha usimamizi wa ubora wa kazi na kupunguza utegemezi wa mshauri elekezi ambaye anapaswa kusimamiwa na TEMESA; na

c) Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) lihakikishe linafanya mapitio ya usanifu wa kina kwa miradi ya ujenzi na ukarabati mkubwa wa vivuko, kukagua miradi ya ujenzi na ukarabati wa vivuko kwa wakati na kwa kila hatua ya ujenzi na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yanayotolewa katika kaguzi inazozifanya kwenye miradi hiyo.

***Kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi Juu ya Udhibiti wa Vifaa Tiba katika Vituo vya Umma vya Kutolea Huduma za Afya***

**KWA KUWA,** Kamati imebaini uwepo wa mapungufu katika udhibiti wa vifaa tiba na baadhi ya vifaa tiba ikiwa ni pamoja na masuala yafuatayo: -

a) Baadhi ya vifaa kutofanya kazi kwa kutofanyiwa matengenezo kwa wakati;

b) Vilevile Kamati imebaini kuwa baadhi ya vituo vya afya havitengi asilimia 5 ya mapato ya ndani kama sehemu ya bajeti kwa ajili ya kuvifanyia matengenezo kinga vifaa tiba;

c) Kwa upande mwingine, ilibainika kuwa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA) haikufuatilia utendaji wa vifaa tiba katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya ili kuhakikisha vifaa tiba visivyofanya kazi na vile visivyofaa kwa matumizi vinaondoshwa; na

d) Kulikuwa na changamoto ya uzingatiaji wa kutosha wa taratibu za usajili wa vifaa tiba na ukusanyaji usiojitosheleza wa sampuli za vifaa tiba kwa ajili ya usajili wakati wa kuviingiza nchini.

**NA KWA KUWA,** changamoto hizo zinapunguza ufanisi wa kufikiwa malengo ya uwekezaji mkubwa wa Serikali katika ununuzi wa vifaa tiba;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

a) Wizara ya Afya ihakikishe inakuwa na mfumo thabiti wa kutunza kumbukumbu na kufuatilia matengenezo na utendaji wa vifaa tiba katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya;

b) Wizara ya Afya ihakikishe taarifa za vifaa tiba chakavu au vilivyopitwa na muda zinawasilishwa kwa wakati TMDA kwa ajili ya uhakiki na mapendekezo ya uondoshaji; na

c) TMDA iboreshe taratibu za usajili na ukaguzi wa vifaa tiba, ili kuhakikisha uwepo wa rasilimali na nyenzo za kufanya ukaguzi wa vifaa tiba na kuhakikisha kuwa uondoshaji na uteketezaji wa vifaa tiba visivyofaa kwa matumizi unafanyika kwa wakati kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za umma.

***Kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi Hapa Nchini***

**KWA KUWA,** Kamati ilibaini dosari kadhaa katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi hapa nchini. Mapungufu hayo ni pamoja na: -

a) Kufanyika kwa shughuli za uvuvi bila leseni;

b) Kuvua samaki ambao hawajafikia urefu unaotakiwa;

c) Kukosekana kwa uratibu mzuri wa shughuli za uvuvi katika maziwa na bahari nchini; na

d) Kutokuwepo kwa ufungaji wa shughuli za uvuvi kwa misimu maalumu na kutokuwepo kwa doria za mara kwa mara ili kuzuia uvuvi haramu.

**NA KWA KUWA,** mapungufu hayo yanasababisha Serikali kutopata mapato stahiki kutokana na rasilimali za uvuvi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

a) Serikali kuhakikisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa zinasimamia na kudhibiti shughuli za uvuvi haramu zinazochangia upotevu wa fedha za umma; na

b) Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) zihakikishe zinaratibu jitihada za pamoja katika kusimamia shughuli za uvuvi na kuhakikisha uendelevu wa rasilimali za uvuvi nchini ili kuongeza mapato ya Serikali.

***Kuhusu Miradi ya Maendeleo Iliyokaguliwa na Kamati Mwezi Machi, 2024***

**KWA KUWA,** Kamati ilibaini dosari kadhaa katika miradi ya maendeleo iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati Mwezi Machi, 2024. Dosari hizo ni pamoja na: -

a) Usanifu usiojitosheleza wa baadhi ya miradi;

b) Baadhi ya miradi kutokamilika kwa wakati;

c) Ongezeko la gharama kwa baadhi ya miradi;

d) Kuchelewa malipo kwa wakandarasi; na

e) Usimamizi, ufuatiliaji na tathmini isiyotosheleza kwa baadhi ya miradi;

**NA KWA KUWA,** dosari hizo kwa ujumla wake zimesababisha kutopatikana thamani halisi ya fedha za umma iliyotumika kwenye baadhi ya miradi husika;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba;

a) Serikali iingie mikataba mipya ya ujenzi wa miradi pale tu inapokuwa imetenga bajeti na fedha za miradi husika ili kuepuka malipo ya riba kwa kuchelewa kulipa wakandarasi kwa wakati; na

b) Tathmini ya kina na upembuzi yakinifu wa miradi ifanyike kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi ili kuepuka nyongeza ya kazi za ziada kwa miradi mingi hali inayosababisha ongezeko la gharama;

c) Serikali itumie mifumo ya kisasa ya ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha maendeleo ya miradi yanafuata ratiba iliyopangwa;

d) Serikali ichukue hatua stahiki za kinidhamu na kijinai kwa wakati kwa wahusika wote wanaobainika kusababisha ubadhirifu kwenye miradi ya maendeleo na wote wanaosababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi kwa mujibu wa mikataba kwa sababu zisizokuwa na tija.

## SEHEMU YA NNE

## HITIMISHO

**Shukurani**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini na thabiti. Uongozi wako umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo kila mara ulipoombwa kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa. Naomba majina ya Waheshimiwa Wabunge Wajumbe wa PAC majina yao yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1) Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb – **Mwenyekiti**
2) Mhe.Japheti Ngailonga Hasunga, Mb – **M/Mwenyekiti**
3) Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwele, Mb
4) Mhe. Joseph George Kakunda, Mb
5) Mhe. Stephen Lujwahuka Byabato Mb
6) Mhe. Simon Songe Lusengekile, Mb
7) Mhe. Anton Albert Mwantona, Mb
8) Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb
9) Mhe. Juma Othman Hija, Mb
10) Mhe. Idarus Faina Ravia, Mb
11) Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi Mb
12) Mhe. Janeth Maurice Masaburi, Mb
13) Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb

14) Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb
15) Mhe. Condester Michael Sichalwe, Mb
16) Mhe. Nancy Hassan Nyalusi, Mb
17) Mhe. Daudi Protas Venant, Mb
18) Mhe.Issa Jumanne Mtemvu, Mb
19) Mhe. Bakar Hamad Bakar, Mb
20) Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai, Mbunge

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Baraka I. Leonard kwa uongozi wake thabiti wa Sekretarieti ya Bunge ambayo imeratibu shughuli za Kamati kwa ufanisi mkubwa hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndugu Charles Kichere na Maafisa wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT). Aidha naushukuru uongozi wa Wizara ya Fedha kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG), Mhasibu Mkuu wa Serikali (AcGen), Msajili wa Hazina (TR) na Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali (DGAM) na Maafisa wao wote kwa ushirikiano waliotoa katika kuratibu majibu ya hoja za ukaguzi na mahojiano ya Kamati na Maafisa Masuuli.

**Hoja**

**Mheshimiwa Spika,** nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kutoa Hoja.

Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU**
**YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC)**

11 Februari, 2025

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa Waheshimiwa tunaanza uchangiaji na tunaanza na Mheshimiwa Simon Songe, jiandae Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Venant Protas, dakika tano tano.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie Taarifa hii ya Kamati ya *PAC* kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa wa Kamati. Kwanza, nawapongeza sana Kamati kwa taarifa nzuri ambayo imeletwa hapo leo yenye msisitizo kwa maeneo ambayo Serikali inatakiwa kuyaboresha zaidi ili kufika kwenye usanifu na kuona thamani ya fedha kwa miradi ambayo tunaendelea nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naungana na Wabunge wenzangu waliopita kwenye michango yao ya nyuma kupongeza sana Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi uliokaa tarehe 19 Januari kwa kumpitisha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea pekee wa Urais 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana nao, na kwenye hili Wajumbe waliona hamna haja ya kusubiri kwa sababu maendeleo yamefanyika na sisi tumeyaona kwa kweli yamefanyika hatukutaka kusubiri na sisi tunaungana nao, na Busega tupo tayari kwa ajili ya kazi ya kuhakikisha kwamba Mama Samia anashinda tena mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa imezungumzwa hapa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, nami nataka nichangie eneo moja tu juu ya ujenzi wa vyuo vya *VETA*, vyuo 64. Kwa maana, vyuo 63 ambavyo ni vyuo vya wilaya ambazo hazikuwa na *VETA* pamoja na chuo kimoja cha Mkoa wa Songwe kule kwa Mheshimiwa Hasunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti kazungumza hapa kwamba baada ya *CAG* kwenda kuangalia ukaguzi huu, kuna changamoto ambazo zimebainika katika ukaguzi uliofanywa na *CAG* ikiwemo ucheleweshwaji wa miradi hii ya ujenzi wa *VETA*.

Miradi hii imecheleweshwa kwa sababu ya upatikanaji wa fedha kutoka Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii 63 ya vyuo vya wilaya na hiki kimoja cha mkoa, fedha za kwanza ambazo tuliweka kwenye mpango wa 2022/2023 kwenye bajeti ilikuwa shilingi bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa *VETA* hizi, na ujenzi huu ulikuwa ni wa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mpaka kufikia Januari, 2025 fedha ambazo zilikuwa zimeshatoka tayari ambazo zilikuwa ni shilingi bilioni 54 sawa na 54% ambapo sasa kuna baadhi ya *VETA* hizi ambazo ujenzi wake umeanza, zimekaa muda mrefu zikiwa na maboma bila kuwa na vifaa kwa ajili ya kuezeka na vifaa vingine kwa ajili ya kumalizia, ambapo ilikuwa ni kwa ajili ya majengo tisa na awamu ya pili ni majengo nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tukichukulia pale Busega tayari tumeshaletewa fedha za ujenzi wa majengo, lakini ni muda sasa umepita takribani miezi sita hatujapata fedha za kuendeleza miradi, na majengo yamejengwa kwa maana ya maboma, yamekaa pale, lakini miradi hii ilikuwa ni miradi ya kimkakati. Tulipowahoji Wizara ya Elimu, kwa unyenyekevu kabisa walionesha jitihada ambazo zimefanyika kwa ajili ya upatikanaji wa fedha, lakini walikuwa hawajapelekewa fedha na Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale mwanzoni walielekezwa wanunue vifaa kwa mara moja *(bulk)* ikiwemo *cement;* na ilishanunuliwa kwa muda mrefu. Kwa mfano, kuna baadhi ya maeneo mpaka sasa hivi tunavyozungumza tayari maboma yameshakamilika na *cement* ya kuendeleza ipo, lakini hawawezi kuendeleza kwa sababu maboma yale bado hayajaezekwa na ile *cement* sasa inaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mifano, kama kwa pale Busega, tuna mifuko 718; ukienda kule Songwe, kuna zaidi ya mifuko 1,000; ukienda kule Mlele, kuna zaidi ya mifuko 800 ambayo ipo na sasa muda wowote inaweza kuharibika kama hatutapata fedha za haraka kwa ajili ya kunusuru miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuja na wazo la ujenzi wa *VETA* kwenye wilaya ambazo hazikuwa na *VETA*. Ni wazo jema na lina tija kwa Watanzania kwa ajili ya wale Watanzania ambao sasa wanaweza kujiendeleza kwenye *VETA* zetu kwa shughuli ndogo ndogo zikiwemo shughuli za upishi, fundi cherehani na kazi nyingine, kupata elimu kwenye *VETA* zetu… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Dakika tano tayari, ahsante.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa uwe na nidhamu ukiwa kwenye Bunge, naomba sana. Kwanza hurusiwi kuzungumza na mimi kwa mujibu wa Kanuni.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** *(Aliongea nje ya mic)*

**NAIBU SPIKA:** Nawe Mheshimiwa Esther ni Mbunge wa siku nyingi sana, lakini unapenda tu chokochoko. Ukinizingua nitakuzingua. *Behave yourself*. Kama una tatizo na mimi, unamwandikia barua Katibu, *that is how it works.* Kaa chini, kaa kimya. *(Makofi)*

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, Wizara ya Fedha ipeleke fedha Wizara ya Elimu ili miradi hii ikamilike kwa wakati. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda, jiandae Mheshimiwa Protas, jiandae Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Tunapoelekea kukamilisha muda wa Bunge hili la Kumi na Mbili, napenda kukishukuru sana Chama changu cha CCM kwa kunipa heshima ya kuwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nakipongeza chama changu kwa maboresho makubwa ya demokrasia ndani ya chama ambayo hasa tunaenda kuyaona zaidi mwaka huu kwa kuongeza Wajumbe. Mimi peke yangu nitakuwa na Wajumbe zaidi ya 15,000 ambao watanipigia kura za maoni. Kwa hiyo, nawaomba Wajumbe wajiandae muda utakapofika watimize wajibu wao na wale jamaa zangu nawaambia kwamba mwaka huu chama kitarudisha majina kwa hiyo, wawe watulivu waache fujo fujo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana wateule wetu wa ngazi ya Taifa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu; Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi; na Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa uteuzi ambao tuliwapa kwenye Mkutano Mkuu tayari kwa kupeperusha bendera kwenye Uchaguzi Mkuu. Ninawapa hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nalipongeza Bunge lako Tukufu pamoja na Serikali kwa kusimamia vizuri uwajibikaji kama ambavyo amekuwa anashauri *CAG*. Kwa hiyo, kwenye hilo, hongera sana. Katika jukumu hilo, Bunge limetekeleza wajibu wake kwa weledi mkubwa na Wabunge tuna haja ya kujipongeza sana, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dalili za ubora katika uwajibikaji tumeziona tulipotembelea miradi, na mwenzangu Mheshimiwa Songe ametaja miradi ya *VETA,* na tulitembelea na Kiwanja cha Ndege cha Msalato ambapo ujenzi wake unaendelea vizuri. Kwa hiyo, kwa kweli tunawapongeza sana kwa hatua hiyo, hongera sana Serikali na Bunge kwa kusimamia vizuri uwajibikaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushauri katika maeneo machache. Kwanza, mifumo yetu ya udhibiti wa matumizi ya fedha za umma bado tunahitaji kuendelea kuiboresha. Mafunzo ya mara kwa mara ya uzingatiaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu ikiwemo Mifumo ya Kiuhasibu ya Kielekroniki ni muhimu sana tuiendeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo umuhimu wa kuimarisha ufuatiliaji na tathmini na mpaka sasa hivi hatujaambiwa pengine Mheshimiwa Waziri husika wakati anachangia, naye anaweza akatuambia kwamba Serikali imefikia hatua gani katika kuandaa sera ya ufuatiliaji na tathmini pamoja na sheria yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sekta ya uvuvi pia ningependa nichangie kidogo. Inaajiri Watanzania zaidi ya milioni nne. Kwa hiyo, ni sekta muhimu sana. Ukaguzi wa Ufanisi ulionesha kwamba kuna shida ya upatikanaji wa takwimu na shida ya usajili. Napenda kushauri mambo machache kwenye sekta hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, iboreshe ushirikiano na wadau wengine kama vile Wizara ya Maliasili na Utalii. Kuna baadhi ya mito na mabwawa pamoja na baadhi ya maziwa yapo ndani ya hifadhi ili Mtanzania aingie kule kwenye hifadhi kuvua, lazima alipe tozo kubwa sana kwenye *TFS* na TAWA. *TFS* ni shilingi elfu mbili kwa siku. Ina maana miezi mitatu ni shilingi 180,000. Halmashauri ikilipa shilingi 72,000 maana yake ni shilingi 252,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu Mtanzania akilipa shilingi 252,000 ni nyingi sana; na TAWA ni zaidi kidogo inafika shilingi 382,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wadau wa maliasili na utalii wangeshirikishwa vizuri, wakashauriwa, pengine wengeweza kupunguza hizo tozo ili Mtanzania akapunguziwa mzigo wa gharama za kulipa anapoingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho, nashauri sekta ya uvuvi ianzishe ushirika wa uvuvi kama ambavyo kuna ushirika wa wakulima ili kurahisisha usajili wao na ufuatiliaji na upatikanaji wa takwimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kwa hayo machache kwa dakika hizi tano, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Protas, halafu Mheshimiwa Hasunga, Mheshimiwa Byabato na Mheshimiwa Anatropia mjiandae.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nami kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika ripoti hii ya Kamati ya *PAC*. Niungane na Wabunge wenzangu kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais, na vilevile kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kumteua mapema kuwa mgombea wa Urais kwenye uchaguzi ujao na mgombea mwenza Dkt. Emmanuel Nchimbi, lakini bila kumsahau Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Mwinyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Watanzania wanaamini kazi walizozifanya kwa kipindi hiki cha miaka mitano, vilevile, nina imani kubwa watakwenda kupata kura za kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tumekuja kujadili Kamati hii ya *PAC* ambayo imefanya kwa kipindi cha mwaka mmoja, nami kama Mjumbe wa Kamati hii namshukuru Mheshimiwa Spika kwa kuniamini, na nimekuwa kwenye Kamati hii ya kusimamia mashirika na mali za Serikali kwa kipindi cha miaka mitano. Kwa hiyo, amenipa heshima kubwa sana, na nimejua vitu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, leo nikitaka kukutajia watu wanao-*temper* na fedha za Serikali, ninawajua kwa majina na sura zao, lakini wanaofanya kazi vizuri kwenye mashirika nawajua kwa majina na sura zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali, tumekuwa tukisema sana juu ya upotevu wa fedha, lakini kwa kipindi hiki kilichopita, naona sasa kuna mwelekeo mzuri sana, matumizi ya Serikali yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa changamoto, bado zipo, lakini kuna ongezeko kubwa la ufanisi katika majukumu na usimamizi wa fedha za Serikali. Kwa hiyo, nawapongeza sana na hapa leo nilitaka kama wangekuwa wamevuruga tungewataja wezi wote ambao wanaiba hela za

Serikali, lakini kwa hapa tulipofikia tumeona hatua zimechukuliwa na mambo yameenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi yetu kubwa ilikuwa ni kuisimamia Serikali, lakini *CAG* ana kaguzi mbili. Kaguzi ya kwanza ni ya Hesabu za Serikali na kaguzi ya pili ni ya Ufanisi. Kaguzi ya Ufanisi ina maana kwamba, kama tulitenga fedha za kwenda kuhudumia miradi ya *REA* na *REA* imekwenda kupewa fedha, tunahitaji tuone wananchi wananufaika na nishati ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kumekuwa na changamoto moja ndogo ya kuchelewa kwa miradi. Ucheleweshwaji wa miradi, kwanza unasababisha lengo la kuwafikishia wananchi huduma kwa wakati linachelewa. Hiyo ni hasara kwa wananchi, na pili, inaongeza gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tulikwenda kutembelea mradi mmoja wa Kahama, mradi ule umechelewa kwa kipindi cha muda wa zaidi ya miezi kadhaa. Sasa pale tumekuta kuna *variation* iliongezeka kwa sababu ya ucheleweshwaji wa mradi. Moja, kuna matatizo upande wa Serikali na mengine yalikuwa upande wa mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naiomba Serikali, kwa kuwa tunakwenda kwenye kudhibiti fedha za Watanzania ambazo tunazitoa, ni lazima tuwe tunaangalia ni namna gani ya kwenda kuhakikisha, kama tumesaini mikataba kwa miaka miwili, tunahitaji mikataba ile ikasimamiwe kwa ukaribu, ili ikamilike kwa wakati na wananchi wetu wapate huduma. Hii inasababisha mradi kuchelewa na baadaye wananchi wanaingia kwenye hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatolee mfano. Kuna miradi ya *REA* ambayo tulipewa sisi kule, ikaenda kwenye kila Kijiji, na Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo kwamba mwananchi ataunganishiwa umeme kwa shilingi 27,000. Miradi ikiwa kwenye kipindi cha *REA,* mkandarasi anapochelewa kukamilisha kwa wakati wanakwenda kuwakabidhi *TANESCO,* wakati muda ukiwa umebaki mchache. Wanapohamisha tu kwenda TANESCO, kuna

baadhi ya vijiji wamevi-*term* kama miji. Kwa hiyo, wanakwenda kuwatoza wananchi shilingi 321,000 kutoka shilingi 27,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi walikuwa na nia njema, na walikuwa wanahitaji kuunganishiwa umeme, lakini mkandarasi aliwacheleweshwa kwa makusudi. Kwa hiyo, tunapopeleka tu *TANESCO,* wanaenda kuwatoza gharama kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii kelele ya vijiji, kwenye vijiji vyangu kama Goweko, Kingwa na Nsololo ambavyo vinasomeka kama vijiji, lakini wananchi wameshindwa kupata matunda na huduma nzuri ya nishati ya umeme kwa sababu ya ucheleweshaji wa wakandarasi, leo wanatozwa shilingi 320,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, nilishampelekea Mheshimiwa Waziri majina ya hivi vijiji. Kule Kingwa wanahitaji walipe kwa shilingi 27,000 kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Ile shilingi 320,000 itakuja baada ya miaka 15 huko, sisi tukiwa tumeenda kupumzika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo mengi ambayo Mheshimiwa Songe ameyazungumza hapa. Kuna changamoto ya umwagiliaji katika maeneo yetu, Serikali inahitaji kubadilisha kilimo chetu ili kiwe cha kisasa. Tumesaini mikataba mingi ya umwagiliaji kwenye maeneo yetu, likiwemo Bwawa langu la Goweko pale, tangu mwaka 2023. Maelekezo yalikuwa, mwaka 2023, mwezi wa Tisa, uwe umekamilika. Ule mradi mpaka leo uko chini ya 50%. Sasa huu ndiyo ule ucheleweshaji ambao tunauzungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesaini mkataba na tumepeleka fedha za *advance payment,* lakini leo ni miaka miwili, bado miradi hii haijakamilika. Naiomba Serikali ikamilishe miradi hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Mheshimiwa Hasunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Byabato na Mheshimiwa Anatropia, mjiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi ya kuweza kuchangia katika ripoti hii ya Kamati. Naanza kwa kuunga mkono maazimio yote yaliyotolewa kwenye Ripoti ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri ambayo ameifanya. Imeonesha utendaji wake, ndiyo maana hata Hoja za *CAG* zimekuwa zikifanyiwa kazi vizuri na Maagizo ya Bunge yamekuwa yakitekelezwa vizuri kiasi kwamba, mambo yamepungua na yanaendelea kuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Spika, pamoja na wewe na timu kwa ujumla, kwa kutenga muda wa Bunge kuweza kujadili kwa kina Taarifa za Ukaguzi za *CAG*. Taarifa ya ukaguzi wa fedha tuliijadili mwezi Novemba kwa kina kwa karibu siku tatu na leo tunajadili Taarifa ya Ufanisi pamoja na Taarifa ya Ukaguzi wa kiufundi. Ninaweza nikasema hii ni kwa upekee kabisa kwa Tanzania na kwa Bunge kutenga muda maalum kujadili ripoti za kiufundi na za kiufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaiweka Tanzania katika rekodi za dunia kwamba, Tanzania ndiyo moja ya nchi pekee ambazo zinajadili taarifa za kiufanisi. Nchi nyingi hazipati muda wa kujadili taarifa za kiufanisi, lakini sisi tunapata muda wa kujadili taarifa za kiufundi na za kiufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ripoti zote za kiufanisi na kiufundi, sisi kama Kamati, tumezijadili kwa undani na tumeona yale yote ambayo yamependekezwa na *CAG* na tayari Serikali inaenda kuyafanyia kazi. Kwa kweli, tuna haja ya kuipongeza Serikali na kumpongeza *CAG* kwa namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuhusu teknolojia. Sasa hivi ukaguzi ule wa kifedha umebadilika, na hesabu

zinafungwa kwa teknolojia. Sasa hivi nchi nyingi zinahama kutoka kwenye ukaguzi wa kifedha kwenda kwenye ukaguzi wa kiufanisi. Kwa hiyo, naomba *CAG* na timu yake waendelee kuweka uzito zaidi kwenye kufanya ukaguzi wa kiufanisi, kiufundi na ule ukaguzi wa *real time audit* ambao ndiyo utatupa picha ya nini kinaendelea na nini kifanyike, ili Serikali iweze kuboresha katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, hiyo kazi kwa kweli, inafanywa vizuri, lakini ziwekwe *resources* zaidi katika eneo hilo, ili tupate ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, nichangie tu kwenye upande wa ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Songwe ambacho sisi tuliamini kwamba, kikikamilika vijana wengi ambao hawana ujuzi na ambao wanahitaji kujiajiri wangepata maarifa na ujuzi katika chuo kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Wizara ya Fedha watoe fedha wakakamilishe kile chuo kabla ya uchaguzi. Maana yake, kama kitakwenda mpaka baada ya uchaguzi, itakuwa ni *disaster* kwa kweli na tutashindwa kujenga hoja. Ili kusudi mambo yaweze kwenda vizuri, ni vema wakatoa fedha katika kipindi kilichobaki, ili kile chuo kijengwe, kikamilike, vijana waende kusoma pale na kupata aina mbalimbali za ujuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne ambalo nataka kupendekeza ni kwa kuwa, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Marekebisho yake, Ibara ya 143, inamtamka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, angalau mara moja kwa mwaka, kufanya ukaguzi wa masuala ya fedha katika Wizara, Mashirika ya Umma, Wakala za Serikali na taasisi zinazojitegemea. Ibara hiyo inaposema angalau mara moja, maana yake nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kila taasisi lazima *CAG* aipitie angalau mara moja kwa mwaka. Sasa basi, kwa kutekeleza ibara hiyo na sisi Bunge tunahitaji angalau mara moja kwa mwaka kuhakikisha zile ripoti alizozileta *CAG* tunazipitia, kuzichambua,

tunaleta mapendekezo na kuishauri Serikali namna ya kutekeleza hoja mbalimbali ambazo zitakuwa zimebainika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi sisi kama Bunge tumekuwa tukifanya uchambuzi, tunachagua taasisi chache, na kanuni zetu zinasema, tunachagua maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma ambayo yamebainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, sasa hivi hatutakiwi kuzungumzia tu maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma, bali tunatakiwa tuhakikishe kwamba tunapitia kwa undani ili kuhakikisha yale malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa, kuhakikisha ufanisi unakuwepo na kukakikisha kwamba kila taasisi ambayo inatakiwa ipitiwe na Bunge, inapitiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumetekeleza takwa la Kikatiba ambalo Katiba yetu inalitaka. Kwa hiyo, napendekeza Bunge litenge muda wa kutosha kuhakikisha kwamba, kila taasisi ambayo inaguswa na Ripoti za *CAG,* basi Bunge lipate kuzipitia, kuleta mapendekezo yake hapa Bungeni na kuishauri Serikali namna ya kuboresha utendaji. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumetekeleza masuala ya utawala bora na mambo yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono Hoja za Kamati. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Anatropia, halafu Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy ujiandae.

**MHE. STEPHEN L. BYABATO:** Mheshimiwa Naibu Spika, uliniita mimi kwanza. Ulinitanguliza mimi.

**NAIBU SPIKA:** *Sorry, sorry*. Mheshimiwa Byabato, ndiyo wewe, sawa, halafu Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. STEPHEN L. BYABATO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza naanza

kwa kuunga mkono hoja. Pia, naunga mkono hoja za wachangiaji wenzangu walionitangulia, Wajumbe wa Kamati wenzangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, namshukuru sana Mheshimiwa Spika, pamoja na wewe, kwa kunipa nafasi ya kuhudumu katika Kamati hii nyeti kabisa, ambayo inaendelea kutazama namna ambavyo Serikali inatumia fedha za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naungana na wenzangu kumpa pongezi nyingi sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi yetu ambayo tuliifanya tarehe 19 kwake yeye, Dkt. Nchimbi, pamoja na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii imetokana na kazi ya Bunge hili kuisimamia Serikali na miradi ikatekelezwa. Mwisho wa siku, sasa tunaona Watanzania wote kwa ujumla, sisi tukiwa wawakilishi na wajumbe, tunasema Mheshimiwa Dkt. Samia aendelee, na hiyo mitano tena, inasemwa na kila mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninao mchango mmoja tu kwa leo. Katika Bunge la Bajeti, mojawapo ya eneo ambalo nitachangia ni kuomba fedha ya *CAG* iongezwe, ili aweze kufanya kazi yake vizuri zaidi kwa kuwa sasa hivi kazi aliyonayo ni kubwa, kwa sababu ya mambo makubwa ambayo Serikali ya Awamu ya Sita inayafanya. Sasa ni lazima pia tumwongezee nguvu ya kuhakikisha anafika kwenye kila eneo na kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tunafahamu, sasa hivi zaidi inafanywa *technical* na *performance audit* ambayo tunaizungumzia hapa. Nadhani sasa tunahitaji kwenda kwenye kufanya *real time audit* ambayo Mheshimiwa Hasunga ameisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tuhame kutoka kwenye utaratibu wa sasa wa mkandarasi kupewa ushauri na mshauri. Tuwe na *design and build* ya mtu mmoja, ambaye tutaweza kumbana yeye mwenyewe kirahisi. Hii itatusaidia kupunguza

matatizo mengi ambayo Kamati tumeyaona kwenye ucheleweshaji wa miradi, miradi kutokukamilika kwa wakati na mmoja kumsingizia mwingine kwamba kazi haijafanyika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa tunafanya *design and build,* maana yake ni atabeba mzigo wote mtu mmoja, lakini tukiwa na *real time audit*, *auditor* atakuwa anakwenda hatua kwa hatua na kuona ni wapi ambapo tunachelewa na tunaweza kukamilisha kazi kwa wakati. Kwa kufanya hivyo, itatusaidia sasa miradi mikubwa mizuri ambayo tukonayo kwenye maeneo mbalimbali, iweze kuwa na tija na kuwafikia wananchi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona hapa kwenye Uwanja wetu wa Msalato, tuna ucheleweshwaji wa mradi. imeongeza mpaka na fedha zinazodaiwa. Tutakuja kupata shida ya kuzilipa na fedha hizo zingeweza kufanya mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo hiyo, pale Bukoba Mjini, mimi nimepata kujengewa *control tower,* lakini bado haijaanza kwa sababu ya mazingira haya haya ya kuchelewesha, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia tayari ameshatoa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye eneo la mwisho, ili nikimbizane na muda. Mimi kwetu nimepata miradi mingi sana ambayo imetokana na azma kubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia ya kuwahudumia wananchi. Ni jana tu Mheshimiwa Mchengerwa ametupa jeuri na afya mpya, nami nasema, kule kwetu umetangazwa mradi wa ujenzi wa soko jipya, Mradi wa Ujenzi wa Kingo za Mto Kanoni, Mradi wa Ujenzi wa Barabara na Mradi wa Kujenga Stendi ya kisasa, ambayo kwa miaka mingi sana imekuwa ni miradi ambayo haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *inshaallah,* ninaamini Bunge linalokuja nitarudi hapa, kwa sababu, wananchi wangu tayari wameshaona nimefanya kazi vizuri. Sasa, ili niweze kurudi kirahisi na Mheshimiwa Dkt. Samia ametoa fedha na ameshampa *CAG* fedha ya kuanzia, basi tuwawezeshe fedha ya kufanya *real time*

*audit,* ili hii Miradi ya Bukoba Mjini niliyoisema, ambayo niliiahidi kupitia kwa Mheshimiwa Dkt. Samia iweze kutekelezwa na kukamilika, ili wananchi waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu sasa *slogan* ni mpya. Kama unataka kuwa Mbunge wa Bukoba Mjini, utueleze Byabato ameshindwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii ni jeuri ya Mheshimiwa Dkt. Samia. Mimi nasema tumwongezee nguvu *CAG* ili mimi pamoja na wenzangu turudi tuendelee kuwatumikia wananchi kwa misingi ambayo tuliiahidi tangu mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, naunga mkono hoja, na Mwenyezi Mungu atubariki sote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Muda hautoshi, lakini naomba niongee machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, namna pekee ambayo tunaweza kuisaidia Serikali ni kwa kuishauri mambo kadha wa kadha. Namshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kunichagua kuwa mmoja kati ya Waheshimiwa Wabunge ambao tumekuwa tukishiriki katika hii Kamati ya *PAC,* kwani imenipa nafasi ya kuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mjumbe mmoja hapa ameeleza akasema, leo naweza kujua ni wangapi na akina nani wamekuwa wakitumia au wameshindwa kusimamia vizuri fedha za umma au ni wangapi wamefanya vizuri. Namshukuru Mungu nami ni kati ya wale. Kwa hiyo, naweza pia kujua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, kwa sababu ya muda, changamoto kubwa tuliyoiona katika ukaguzi tulioufanya au katika taarifa mbalimbali za *CAG* ambazo tumekuwa

tukizisoma ni changamoto ya usanifu wa miradi. Kumekuwepo na tatizo kubwa sana katika miradi ambayo Serikali imekuwa ikiifanya, imekuwa ikikosewa, na eneo hili ndiyo limekuwa liki-*attract* riba.

Mheshimiwa Naibu Spika, humu ndani tungekuwa tumeongelea ku-*accumulate interest*, miradi na nini, lakini changamoto kubwa ya gharama za miradi kuongezeka, imetokana na changamoto ya usanifu. Mpaka wakati nasoma ripoti, kwa *interest* ya muda, nikajiuliza, hivi wataalam wetu wana shida gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakupa mfano mdogo kwa Mradi wa Msalato. Wanasema wakati wanafanya usanifu, walivyokuwa wanafanya *survey* walitumia *drones* na walivyotumia zile *drones*, wakati zinapita juu kuangalia lile eneo na kufanya *estimate* kulikuwa na vichaka. Eneo lilikuwa halijasawazishwa na halijalimwa. Kwa hiyo, zile *drones* zikakosa *accurate information* na huo mradi ukaongezeka thamani. Sasa najiuliza, hao wataalam wetu walisoma vizuri kuhusu namna ya kufanya hizo *studies? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni lazima tulifanye kazi hili eneo. Kwa sababu hiyo ya kutumia *drones,* wakati hawajasafisha eneo, imeongeza gharama ya zaidi ya shilingi bilioni tatu kwenye huo mradi na mkandarasi akiwa ameongeza fedha zaidi ya shilingi bilioni tano ambapo, hizo fedha tungeweza kufanya usanifu vizuri, zingeenda kuwasaidia wananchi wa Kyerwa ambao kila siku nimekuwa nikiongelea changamoto yao ya maji. Hilo ni eneo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu eneo la pili ni la usanifu wa miradi. Tumefanya ziara na *CAG* tukaona Miradi ya Maji ya Mwanza *(MUWASA)*. Unakuta thamani ya mradi, *let us say* ni shilingi bilioni 30 au mpaka shilingi bilioni 70, lakini wameshamaliza kutengeneza, maji yanapaswa kutoka. Kumbe hayo maji jinsi walivyokuwa *designed* walitegemea umeme wa kawaida wa *TANESCO* ambao una mgao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mradi umekamilika, lakini chanzo cha maji kina mgao, na wananchi hawawezi kupata maji. Sasa katika usanifu wa mradi, hao watu walijiuliza kwamba, ili mradi uweze kurudisha thamani ya fedha, ni lazima tuwe tumeweka *source* ya *power* ili maji yaweze kuwa *generated?* Hiyo ni changamoto nyingine ya usanifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hiyo tu, kuna mradi mwingine ambao unatoa maji Ziwa Victoria kuleta Singida na Shelui, nao una changamoto zilezile, usanifu mbovu. Kwa hiyo, kama naweza kuishauri Serikali kwa neno moja, hebu kama kuna changamoto ya wataalam wa kusanifu miradi, basi tuangalie namna nzuri ya kuwaelimisha ama kuwafundisha ili tupunguze gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni kuhusu usimamizi wa mikataba. Ukija kuangalia eneo ambalo Serikali imepigwa pakubwa na imepoteza fedha nyingi ni kwenye eneo la usimamizi wa mikataba. Sisi haya mambo tunayasema kila siku na tunachoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia masuala yanayotokana na riba nyingi za wakandarasi ambazo tunaongelea ni kwa sababu, wakati unapofika wa kulipwa fedha, hawalipwi kwa wakati, hivyo kunakuwa na *gross interest*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia mfano mmoja wa Mradi wa Msalato, kwa sababu ya kucheleweshewa malipo, huo mradi ume-*attract interest* ya zaidi ya shilingi bilioni 300. Kwa hiyo, sasa ni lazima Serikali isimame vizuri. Kama tunataka kutumia fedha na tupate thamani ya fedha, ni lazima tujipange vizuri kwenye eneo la mikataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni kuhusu taratibu za manunuzi. Humu ndani kichaka kikubwa cha matumizi ya fedha za umma kinachofanya miradi isikamilike na ipigwe, ni kukiukwa kwa Sheria ya Manunuzi. Serikali imekuja na utaratibu, na Maafisa Masuuli wanajua ni utaratibu gani wanapaswa kuutumia kwa ajili ya kufanya manunuzi, lakini taarifa nzima ya mwaka mzima kila tunakopita ni Afisa Manunuzi hajafuata Sheria za Manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nishauri katika haya maeneo matatu. Kama tunataka tufanye vizuri na kama Serikali imekuwa ikikopa fedha ambazo zinalipwa na walipakodi, ikiwa haya maeneo matatu hayawezi kusimamiwa vizuri tutapigwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sijajua kama muda wangu umebaki, lakini tumekuwa na *special audit* mbalimbali na mojawapo ambayo nitaisema, na kwa sababu ya *interest* ya muda, ni *special audit* inayohusiana na vifaatiba. Serikali ilitoa fedha zaidi ya shilingi bilioni 68 kununua vifaa mbalimbali kwa ajili ya zahanati kwenye *local government* zaidi ya 22.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za walipakodi shilingi bilioni 68, lakini *CAG* alivyoenda kufanya hiyo *special audit* aligundua mashine kadha wa kadha hazifanyi kazi, hazijafungwa na hakukuwa na wataalam husika. Kilichoniumiza zaidi, hizi mashine tangu zimetoka huko nje, zimeshushwa bandarini na zimeenda kufungwa kwenye vituo, hazikuwahi kufanyiwa *calibration* au kuwa *tested* kuona *effectiveness* na *efficiency* ya hizo mashine, ukiachana na kwamba bado kuna maeneo mengine yana hivyo vifaatiba, lakini hakuna wataalam. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante Mheshimiwa.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, muda ni mchache. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Namwita sasa Mheshimiwa Ummy, na Mwenyekiti jiandae uje kuhitimisha hoja yako.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Nianze kwa kuipongeza Kamati ya *PAC*. Nampongeza Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Kaboyoka,

Makamu wake Mheshimiwa Hasunga na Wajumbe wote wa Kamati. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nimesikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge na nimepitia Taarifa ya Kamati kwa kina, tunawashukuru sana kwa namna ambavyo wameendelea kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Serikali, chini ya Waziri wangu, Mheshimiwa William Lukuvi, tunapokea maazimio yote ya Kamati hii na tunawahakikishia kuwa, Wizara zote za kisekta zitaenda kuyafanyia kazi, ahsanteni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Karibu Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa muda kidogo wa kuhitimisha hoja ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliotoa michango yao kwa hoja hii muhimu inayohusu uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma. Michango yao imetolewa kwa weledi na uzalendo wa hali ya juu, na kwa vile kuna kipindi cha uchaguzi kinafuata, nimeelewa mengine ambayo labda hayakuwekewa msisitizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Waheshimiwa Wabunge waliochangia wengi ni wa Kamati yangu, sikuona mwingine wa nje, isipokuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ummy; na kwa kuwa, hakuna yeyote aliyepinga hoja nilizozitoa, naomba tu nisisitize kwamba, yale maazimio yote niliyokuwa nimeyatoa ambayo yako pia kwenye taarifa yetu, yote yaingie katika *Hansard*. Pia majina yote ya Waheshimiwa Wabunge, Wanakamati wa Kamati ya *PAC,* yaingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Bunge sasa lipokee Mapendekezo yote ya Taarifa ya Kamati kuhusu Shughuli za Kamati kwa Kipindi cha Kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kuhusu Mapendekezo ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Shughuli za Kamati kwa Kipindi cha Kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa Kipindi cha Kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025 yalipitishwa na Bunge kuwa Maazimio ya Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Wote mmeafiki na sasa Taarifa hii ni rasmi na Serikali imeshaipokea. Nendeni mkaifanyie kazi, majibu mtaleta kwenye utaratibu ambao utawekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati yako ninawapongeza kwa kazi nzuri. Pia, ninawapongeza Wajumbe kwa michango mizuri ambayo mmeitoa. Vilevile, tunawapongeza Ofisi ya CAG kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya. Endeleeni kuboresha na kuwakamata watu ambao wanaitia hasara nchi hii na Bunge litawashughulikia ipasavyo. Ahsante sana.

Ninaahirisha Shughuli za Bunge, mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.02 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 13 Februari, 2025, Saa Tatu Asubuhi)*